Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI

**Kikao cha Sita – Tarehe 5 Februari, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Atakayeuliza swali la kwanza leo ni Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali.

Na. 73

**Miswada ya Bunge Kuwekwa Kwenye Tovuti ya Bunge**

**MHE. DR. ALI TARAB ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa, teknolojia inarahisisha utendaji wetu wa kazi wa kila siku:-

Je, ni lini *soft copy* ya Miswada inayokuja Bungeni kwa majadiliano itawekwa kwenye tovuti ya Bunge ili iwafikie na wananchi kwa ujumla kwa urahisi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YAWAZIRI MKUU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba teknolojia katika nyanja zake mbalimbali, hususani teknolojia hii ya habari na mawasiliano inarahisisha sana utendaji kazi na hususan utendaji wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni muhimu kupata taarifa mbalimbali mapema na kuzitumia ipasavyo ili kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge, kuwa tayari Bunge limekwishaanza utaratibu wa kuweka Miswada kwenye tovuti ya Bunge, mara tu baada ya kusomwa kwa mara ya kwanza. Aidha, Miswada ikiwa katika *hard*

*copy* inasambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge na wadau wengine ikiwa ni pamoja na kuuzwa katika maduka ya vitabu vya Serikali. Uhifadhi wa Miswada na taarifa mbalimbali za Bunge katika Tovuti ulianza mwaka 2002. Hadi sasa kuna Miswada 56 iliyohifadhiwa katika *database* na imewekwa kupatikana katika Tovuti ya Bunge kwa kutumia anuani ya tovuti ya Bunge www.parliament.go.tz.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwamba sasa hivi umeanza utaratibu wa kuanzisha kuweka *bills* hizi kwenye tovuti. Lakini nina swali moja kama ifuatavyo:-

Je, isingelikuwa busara kwamba ile *final draft* ya *bill* yoyote ambayo inaletwa hapa kujadiliwa baada ya kupata *public hearing* na kugawiwa kwenye Kamati ikawekwa kwenye tovuti kabla au angalau siku ile ambayo tunakuja kuichambua hapa ili wadau wajue tunazungumzia *document* gani? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YAWAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyokwishasema katika jibu langu la msingi kwanza tunaweka Muswada wakati tukisoma katika hatua yake ya kwanza. Kwa hiyo, tunaposoma mara ya kwanza tunaporudi sasa kuanza kuuchambua na kuhusisha wadau mbalimbali ndiyo Muswada huo unakuwa tayari umeshawekwa kwenye tovuti. Kwa hiyo, wanapata nafasi ya kuweza kuusoma na kuuchambua na kuweza kutoa maoni mbalimbali. Nashukuru sana kwa ushauri lakini ndivyo tunavyofanya hivyo tayari. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maana ya *first reading* ni kwamba Muswada umekuwa public mtu yeyote na watu wote wanaweza ku-*access* ikishasomwa *first reading.* Kwa kanuni yetu tumesema kwamba hakuna Muswada utakaokwenda ngazi zote katika kikao kimoja ni kwa sababu hiyo kwamba wananchi waweze kuupata kwa nafasi ya kutosha kuisoma na sisi wenyewe tupate ushauri na *public hearing*. Halafu inapokuja *first reading* ni kikao kingine. Labda Muswada uletwe kwa hati ya dharura na hiyo tunataka iwe michache sana kufuatana na Kanuni zetu. Kama itatokea hati ya dharura lazima wathibitishe kwamba kweli ilikuwepo dharura, vinginevyo Miswada lazima isomwe mara ya kwanza iwe *public* itaingia kwenye tovuti halafu baadaye ndipo iendelee katika vikao vinavyokuja.

Na. 74

**Mahitaji ya Wodi za Kulaza Wagonjwa kwenye Hospitali ya Mkoa wa Mbeya**

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA (K.n.y.MHE. BENSON M. MPESYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuwepo kwa Hospitali ya Mkoa wa Mbeya kumesaidia sana kuboresha huduma za matibabu Jijini Mbeya, na hivyo kupunguza msongamano wa wagonjwa kwenye hospitali ya Rufaa Mbeya.

Je, ni lini Serikali itajenga wodi za kulaza wagonjwa kwenye hospitali ya Mkoa wa Mbeya, ili kupunguza msongamano wa wagonjwa kwenye Hospitali ya Rufaa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la kujenga Hospitali ya Mkoa wa Mbeya lilianza mwaka 1987 kwa kutegemea michango ya wananchi wa Mkoa mzima wa Mbeya.

Utekelezaji wa wazo hili ulishindikana kutokana na sababu mbalimbali na hivyo ilipofika mwaka 1990/1991 Serikali ilianza kutoa fedha kidogo kidogo katika Bajeti yake kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo. Hadi kufikia mwaka 2006/2007 jumla ya shilingi 1,022,000,000/= zilikuwa zimetumika kwa ajili ya kazi zifuatazo:-

(i) Ujenzi wa Jengo la Utawala ambapo zimetumika milioni 95,800,000/-.

(ii) Nyumba mbili za Madaktari ambapo zilitumika shilingi 39,000,000/-.

(iii) Stoo ya dawa zilitumika shilingi 54,000,000/-.

(iv) Maabara na *X-ray* zilitumika shilingi 66,000,000/-.

(v) Jengo la *Voluntary Canceling and Testing (VCT)* Shilingi 11,000,000/-.

(vi) Jengo la Huduma za Uzazi shilingi 462,000,000/-.

(vii) Ujenzi wa Wodi ya Wazazi ambao unaendelea shilingi 324,000,000/-.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mpango wa ujenzi wa Hospitali hii kwa kazi zilizobaki gharama zinazohitajika hadi kukamilika hospitali hii ni shilingi 4,844,655,100/=. Ujenzi wa Wodi nne za kulaza wagonjwa ulianza mwaka 2006/2007. Makisio kwa ujenzi wa Wodi hizi zikikamilika ni shilingi 467,106,100/=. Hadi sasa jumla ya shilingi 324,000,000/= zimetumika hivyo bado shilingi 143,106,100/= ili kukamilisha ujenzi bila kuweka gharama za vifaa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukamilisha kwa ujenzi wa wodi hizo ni lazima uende sambamba na kuwepo kwa huduma nyingine kama sehemu za kufulia nguo, jiko na eneo la kuchomea taka, pia kunahitajika vitanda vya kulaza wagonjwa. Kazi zote hizi

zinahitaji fedha nyingi hivyo, Serikali kupitia bajeti ya Mkoa wa Mbeya itaendelea kutenga fedha kadri zitavyopatikana ili kukamisha ujenzi na ununuzi wa vifaa vya hospitali hiyo. Kukamilika kwa ujenzi wa wadi hizi kunategemea sana kupatikana kwa fedha katika bajeti ya Serikali.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri na ya Serikali kwa ujumla nina swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa hospitali nyingi za rufaa ukienda Bugando wanasaidiwa na Seko Toure, ukienda *KCMC* wanasaidiwa na Mawenzi na Hospitali ya Mbeya haina hospitali mbadala ya kuisaidia hospitali hii na kusababisha msongamano na lawana kubwa dhidi ya huduma za hospitali, jambo ambalo linatokana na kuelemewa kwa utendaji wa kazi na hospitali hiyo. Je, Serikali ina mkakati gani wa muda mfupi wa kuhakikisha kwamba Hospitali ya Mkoa wa Mbeya sasa angalau wodi moja, mbili zinaanza kutumika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hospitali nyingi za rufaa zinakuwa na hospitali nyingine ambazo zinasaidia kutoa huduma ili kuweza kuhudumia wananchi. Hospitali ya Rufaa ya Mbeya, Serikali ndiyo maana inajitahidi kutenga fedha kila mwaka ili kuhakikisha mwaka Hospitali ya Mkoa inakamilika.

Ni matumaini yangu kwamba kwa sasa hivi ujenzi unaoendelea wodi nne za wazazi na kufikia mwaka ujao huenda zikakamilika na kuanza kazi kamili. Kwa kweli ni nia nzuri ya Serikali kuhakikisha kwamba hospitali hiyo, inakamilika na itatenga fedha mwaka hadi mwaka. Kwa mwaka ujao itatenga fedha kwa ajili ya kumalizia hizi wodi nne za wazazi ambazo zimeanza kujengwa na sasa hivi ziko katika *stage* ya upauaji.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muanze kufanya mazoezi ya kuuliza maswali kipindi cha Waziri Mkuu, muulize mafupi siyo mnaendelea kutoa hadithi na majibu yawe mafupi.

Na. 75

**Faini ya Tshs. 80,000/= Kwa Magari Yaliyoegeshwa Vibaya Katika Jiji la Dar es Salaam**

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa, miundombinu ya barabara za Jiji la Dar es Salaam haitoshelezi kukidhi haja ya uwingi wa magari yaliyopo, hali inayosababisha kukosekana sehemu za maegesho; na kwa kuwa Halmashauri ya Jiji hutoza faini ya Shs. 80,000/= kwa magari yaliyoegeshwa vibaya:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kutoza faini hiyo wakati hakuna nafasi za kutosha kuegesha magari ni kuwadhulumu wananchi?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kufuta adhabu hiyo mpaka hapo itakapokuwa na uwezo wa kutengeneza *parking* za kutosha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano wa Nane wa Bunge lako Tukufu nilijibu Swali Na. 396 la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, linalofanana na Sali hili. Nilieleza kwamba mamlaka za Serikali za Mitaa Mijini hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sheria Na. 8 ya mwaka 1982 kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 6 ya mwaka 1999 na sheria Na. 13 ya mwaka 2006. Kwa mujibu wa kifungu namba 62 cha sheria Na. 8 kikisomwa pamoja na jedwali katika sheria hiyo, Halmashauri za miji zina jukumu la kudhibiti na kuratibu matumizi ya barabara na mitaa ndani ya eneo lake la utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia wajibu huo wa kisheria na kwa kuwa tatizo la kuegesha magari katika sehemu zisizoruhusiwa ni kero kwa watumiaji wa barabara hasa watembea kwa miguu, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala iliamua kutekeleza sheria ndogo ya maegesho kwa mujibu wa tangazo la Serikali Na. 60 la mwaka 1998 kwa kuyakamata magari yote yanayoegeshwa katika sehemu zisizoruhusiwa.

Wanaokamatwa kwa makosa ya kuegesha vibaya na magari yao kuvutwa na Wakala wa Halmashauri, mwenye gari hupaswa kulipa shilingi 25,000/= kwa kila gari linalovutwa ambapo Halmashauri nayo hupata shilingi 60,000/= na hivyo kufanya jumla ya malipo kuwa shilingi 85,000/= kwa kila gari linavutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dar es Salaam linayo maegesho ya kutosha. Maegesho haya ni pamoja na yale ya kulipia chini ya mkataba wa maegesho, pamoja na yale ya makampuni ya watu binafsi. Tatizo la uegeshaji wa magari katika sehemu zisizoruhusiwa wakati mwingine linasababishwa na ofisi nyingi kuwepo maeneo ya katikati ya Jiji. Katika kunusuru hali hii, Serikali na Uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam umekuwa ukihimiza upanuzi na ujenzi wa ofisi na sehemu za kutoa huduma nje ya mji ikiwa ni njia mojawapo ya kupunguza msongamano wa magari na tatizo la maegesho Jijini. Mfano halisi ni pamoja na ujenzi wa kituo cha biashara cha *Mlima City* ambalo liko Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ujenzi wa Ofisi za Wizara ya Maliasili na Utalii, ambayo iko karibu na makutano ya barabara ya Kawawa na Nyerere, jengo la *TANESCO* Ubungo, ujenzi wa majengo makubwa ya biashara ya *Ubungo Plaza* na *Millennium Tower* na kadhalika Majengo haya yamejengwa kwa kuzingatia mahitaji ya Maegesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, uegeshaji wa magari katika sehemu zisizoruhusiwa ni ukiukwaji wa kifungu cha 17 cha sheria ndogo ya maegesho. Hivyo utozaji wa faini unalenga kuzuia wenye magari wasiendelee kuvunja sheria na siyo kuwadhulumu wananchi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri itaendelea kutoza faini hiyo kwa sababu inalenga kupunguza tatizo la msongamano katikati ya Jiji, kupunguza ajali za barabarani na kulinda usalama wa watu wenye ulemavu na watembea kwa miguu na baiskeli.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Bunge hili lilipitisha sheria ya *traffic offense* ikiwemo kuegesha magari sehemu ambayo hairuhusiwi nao polisi wanatoza faini ya shiligni 20,000.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri haioni kwamba sheria mbili hizi zinagongana kwa kosa moja kwamba kuna watu wawili wanatoza faini kwa suala hili? (*Makofi*)

(b) Pamoja na kwamba kanuni au sheria ndogo ya Jiji iliyotolewa kuhusu uegeshaji wa magari sehemu zisizoruhusiwa na sasa hivi Jiji limebadilisha utaratibu badala ya kulikokota gari na kulipeleka wanafunga *triangle* ili ukalipe faini. Sasa ada ya kutoza au gharama ya kuchukua *breakdown* inakuwa imeondoka na kwa nini wanaendelea kutoza kodi hiyo ya 85,000/= isiondolewe ile kukokota magari? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya *traffic offense* inashughulikia masuala ya ajali na sheria ndogo ndogo za Jiji zinashughulikia *wrong parking.*

Kwa hiyo, sheria hizi mbili hazikinzani zote zinafanya kazi, kila moja inafanyakazi yake na siyo kazi moja kama nilivyosema kuna moja inashughulikia mambo ya ajali na moja inashughulikia tu mambo ya *wrong parking* kwamba gari wameli-*park* vibaya wao wanatoza faini.

Kuhusu utozaji wa faini, utozaji wa faini ni kwamba sheria hiyo au mamlaka husika inaweka wakala yule wakala yeye anachukua asilimia yake na Halmashauri au Manispaa inachukua nayo asilimia yake. Kwa hiyo, mpaka sasa hivi sioni sababu za msingi kwamba ushuru mmojawapo utolewe, kila ushuru una sababu yake na makusudio yake. (*Makofi*)

Na. 76

**Mapambano Dhidi ya Rushwa na Ufisadi Serikalini**

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza:-

Kwa kuwa, suala la rushwa na ufisadi limechukua sura mpya siku za hivi karibuni na kusababisha manung'uniko kwa jamii licha ya jitihada za kupambana na rushwa ambazo zinafanywa na TAKUKURU lakini bado hazijatoa dhamira thabiti ya kupigana kikamilifu na tatizo hilo:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kufuatia kashfa nzito za Rushwa kubwa kubwa zinazohusisha taasisi kama ujenzi wa Benki Kuu, Mikataba ya Madini, Mikataba ya Nishati?

(b) Je, watu wangapi wamefikishwa mbele ya vyombo vya sheria kuhusishwa na rushwa kama hizo?

(c) Je, Serikali inatoa mwito gani kwa jamii katika mapambano dhidi ya rushwa Serikalini na kwenye vyama vya siasa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mbunge wa Busega lenye vipengele (a), (b) na (c) kuhusu mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi Serikalini kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kikao cha Bunge la Bajeti la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 baadhi ya Wabunge waliibua hoja mbalimbali ikiwa ni pamoja na kashfa nzito za rushwa kubwa kubwa zinazohusu taasisi, Wizara na baadhi ya viongozi wa Serikali. Serikali kwa kupitia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, ilishaanza kuzishughulikia tuhuma hizo hata kabla ya tuhuma husika kutolewa Bunge kupitia kikao hicho cha Bajeti cha 2007/2008. Baadhi ya tuhuma hizo nzito ambazo TAKUKURU inazifanyia uchunguzi ni kama ifuatavyo:-

(i) TAKUKURU ilikuwa inafanyia kazi Mkataba wa Ukaguzi wa Hesabu za Makampuni ya uchimbaji madini kati ya *Alex Stewart Assayers* na Serikali na Tanzania.

(ii) TAKUKURU pia, ilikuwa inafanyia uchunguzi Mkataba wa uchimbaji wa dhahabu katika eneo la Buzwagi Shinyanga kati ya Kampuni ya uchimbaji madini ya *Barrick* na Serikali ya Tanzania.

(iii) Mkataba wa machimbo ya makaa ya mawe na mradi wa uzalishaji umeme kwa kutumia makaa ya mawe wa Kiwira Mkoani Mbeya.

Aidha, Taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa inafanya uchunguzi wa tuhuma za matumizi mabaya ya fedha za Serikali katika mradi wa ujenzi wa majengo pacha ya Benki Kuu. Uchunguzi wa tuhuma hizo unaendelea hadi sasa tunapoendelea.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa uchunguzi wa tuhuma hizi bado unaendelea, hakuna mtuhumiwa yeyote alikwishafikishwa mahakamani.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, mapambano dhidi ya rushwa ni jukumu la jamii nzima na siyo la Serikali peke yake. Hivyo jamii ina wajibu wa kushiriki na kuunga mkono jitihada zote zinazofanywa na Serikali katika kuzuia na kupambana na rushwa kwa vile madhara yatokanayo na vitendo vya rushwa vinamgusa mtu binafsi na jamii yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa vyama vya siasa, jamii inatakiwa kufahamu kuwa viongozi wanaochaguliwa katika misingi ya rushwa wanapokuwa madarakani kwa manufaa yao binafsi na si kwa manufaa ya kuleta ya maendeleo ya wananchi kama ambavyo walikuwa wameahidi wakati wa kampeni za uchanguzi. Ieleweke kuwa kiongozi aliyepatikana kwa njia hizo atatumia muda wake madarakani kujilimbikizia mali ili kurudisha gharama alizotumia wakati wa kampeni kwa kuhonga wananchi. Hivyo hatakuwa na ujasiri wa kukemea vitendo vya rushwa na hivyo kufanya jitihada za mapambano dhidi ya rushwa kukosa nguvu. Aidha, ni wajibu wa wanachama wa vyama vya siasa vyote kusimamia ipasavyo mapato na matumizi ya fedha katika vyama vyao ili kudhibiti ubadhirifu wa fedha hizo, na wawe na wawe na ujasiri wa kuwanyima kura wagombea wanaowarubuni kwa kuwapa rushwa au zawadi na ahadi zisizotekelezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wao viongozi wa vyama vya siasa wana wajibu wa kuweka na kusimamia mikakati ya kuzuia na kupambana na rushwa ndani ya vyama vyao. Mkakati wa Taifa wa kupambana na rushwa na mpango wa utekelezaji wa awamu ya I & II ni dira ya mapambano haya. Ni ukweli usiopingika kuwa rushwa hawanyima nafasi wanachama wenye uwezo kugombea nafasi za uongozi kwa sababu tu hawana uwezo wa kuwapa fedha wajumbe wanao wapigia kura.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba mpaka sasa hivi hakuna mtu hata mmoja ameshakamatwa kuhusiana na rushwa nene nene na nono. Wanaokamatwa ni zile rushwa ndogo ndogo.

(a) Hivi kweli dhamira ya Serikali ya kupambana na rushwa inaishia hapo kwa rushwa ndogo ndogo au na hawa wanene? (*Makofi*)

(b) Vyombo vya habari vimechangia sana kuibua maovu katika jamii yetu na Bunge hili limekuwa mara kwa mara likizungumza kwamba mikataba yenye utata iletwe angalau iweze kupitiwa na Bunge hili na yote inakuwa ni siri. Je, Serikali iko tayari sasa kwanza kuunga mkono jitihada za vyombo vya habari kupambana na rushwa na pili kuleta mikataba hii Bungeni ili Bunge liweze kupitia kwa niaba ya wananchi? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mbunge wa Busega, maswali yake mawili kama ifuatavyo:-Kwanza si vema na siyo utaratibu kujadili Bungeni kesi ambazo ziko mahakamani ambazo zinahusu watoa au wapokea rushwa wadogo na wakubwa, itoshe tu kutaja kwamba sasa hivi mahakamani kuna kesi zinazohusu watoa rushwa na wapokea rushwa wadogo na wakubwa.

Pili, kwa hakika Serikali ina dhamira ya kupambana na rushwa. Tatizo ni kwamba matumaini ya wananchi na viongozi wao ni makubwa sana katika jitihada hizi ambacho hatujakifikia ni matumaini makubwa ya wananchi, lakini tumejitahidi kwa uwezo wetu wote kupambana na rushwa ndogo na rushwa kubwa na kuna dhamira ya kweli kweli kwa upande wa Serikali. *Inshallah* ni matamshi mazito ya Mheshimiwa Rais ya Jakaya Mrisho Kikwete. Kuhusu Mikataba kuleta Bungeni mimi nisingependa kuweka mnyororo mbele ya farasi kinachotangulia ni sheria itakayohusu Mikataba kuleta Bungeni kwa hali tuliyonayo sasa hivi Mikataba hailetwi Bungeni, Bunge linaridhia tu mikataba baada ya kutiwa sahihi na wawakilishi wa Serikali. (*Makofi*)

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba TAKUKURU inaendelea kuchunguza jambo linaloashiria kwamba uchunguzi umeisha, ilikuwa maana yake ni kwamba umeisha. Na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema vile vile kwamba hakuna aliyepelekwa hadi sasa mahakamani na kwa kuwa katika taarifa ya Jaji Kisanga watu wengi walioko rumande hadi sasa kesi zao uchunguzi haujamalizika. Serikali inaeleza nini Taifa hili kwamba maelefu ya Watanzania wako rumande kwa miaka na miaka kwa ajili ya tuhuma lakini hawa waliotuhumiwa kwa rushwa kubwa kubwa wanaochunguzwa wao wako nje wanatamalaki katika nchi hii? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, maswali yake kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza, ikumbukwe tu kwamba hatma ya uchunguzi wowote unaelekea katika maeneo matatu kwanza kushauri Serikali. Pili kama inaonekana ushahidi unatosheleza kupeleka shauri mahakamani. Tatu kama inaonekana ushahidi hautoshelezi basi kufunga jalada. Sasa hivi kuna kesi kubwa kubwa ambazo zimeshafikishwa mahakamani. Zingine zimepelekwa Serikali kama ushauri na majalada mengine yamefungwa. Pili, kuhusu raia au wananchi ambao wako mahabusu kwa sababu uchunguzi bado katika mashauri mbalimbali ya jinai hapa itoshe kusema tu kwamba jitihada nyingi zinafanyika ili kusukuma kesi na kwa kweli kwa sasa kama mtuhumiwa hajapelekwa mahakamani katika muda wa miezi sita, basi shauri huangaliwa upya na mtuhumiwa kuachiwa.

**NAIBU SPIKA:** Kwanza tumetumia mudamrefu sana. Muda wa maswali hayo umeshapita. Waziri wa Sheria na Katiba kwa kifupi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utawala Bora, kwa majibu mazuri na kwa maswali mazuri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inafanya kila linalowezekana ili kuona kwamba watu hawakai rumande kwa muda mrefu bila sababu, na nyinyi wenyewe mnakumbuka kwamba hivi karibuni tumepitisha Sheria ya kutenganisha Upelelezi na kuendesha mashtaka ili kuongeza ufanisi pande zote mbili. Lakini vile vile katika kupeleka watu Mahakamani ni vizuri kabisa upelelezi ukakamilika kusudi wasiongezeke watu wa kukaa rumande kwa muda mrefu bila sababu. Napenda kwa kweli kulihakikishia Bunge lako kwa sheria hii mpya ambayo baada ya Mheshimiwa Rais kuridhia *DPP* atakuwa na uwezo wa kwenda rumande na kuona wale ambao wamekaa bila sababu rumande na kuweza kuchukua sababu stahili. *(Makofi)*

Na. 77

**Askari aliyeweza kukataa Rushwa**

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1983 Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alimpongeza *Ex-Senior Police Inspector* Hashim Mganga kwa kumkabidhi hundi ya Shs.100,000/= kwa ajili ya kununua fenicha ya nyumba aliyoahidiwa kujengewa na Serikali kwa kitendo chake cha kukataa kupokea rushwa. Lakini hadi sasa ahadi hiyo haijatimizwa licha ya ufuatiliaji wa karibu unaofanywa lna yeye mwenyewe na Mbunge wa Dodoma Mjini:-

(a) Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya zaidi ya miaka 24 ya kumjengea nyumba askari huyo?

(b) Je, Serikali kwa kutotimiza ahadi yake kwa mhusika haioni kwamba inamvunja moyo na wengine ambao wako mstari wa mbele katika kupambana na adui rushwa?

(c) Je, Serikali haioni kuwa imejishushia hadhi mbele ya umma wa Watanzania kwa kutotekeleza ahadi iliyotolewa na Kiongozi Mkuu wa nchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ephraim Nchemwa Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza rai mapema zaidi za awali kwa ajili ya maelezo marefu kidogo kuhusu suala hili kwa ajili ya unyeti wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Ex-Senior Inspector* wa Polisi Hashimu Mganga, alianza kazi za Upolisi mwaka 1964 na kustaafu mwaka wa 1986 akiwa hapa Mjini Dodoma. Mnamo tarehe 17 mwezi wa nne mwaka19 83 majira ya saa 11 alfajiri huko Msalato, nje kidogo ya mji wa Dodoma akiwa pamoja na askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani wa Kituo cha Polisi cha Kati Mjini Dodoma walikamata lori ikiwa na shehena ya mapipa 14 ya mafuta ya dizeli yaliyokuwa yanapelekwa Kondoa kutokea Mpwapwa, wakati huo kulikuwa na uhaba mkubwa sana wa bidhaa hii nchini na Serikali ilikuwa vitani kupambana na wahujumu wa uchumi.

Mmiliki wa lori hilo alimpa rushwa ya shilingi laki moja ambayo wakati huo ilikuwa kubwa sana lakini Ofisa huyo wa Polisi alikataa na kumkamata mtu huyo aliyekuwa anajulikana kwa jina la Ibrahim Hassan na kumfikisha Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya tukio hilo aliyekuwa Waziri Mkuu wakati huo Marehemu Edward Moringe Sokoine aliahidi kwamba Serikali ingemzawadia *Inspector* wa Polisi Mganga shilingi laki moja kutokana na kitendo hicho cha kukataa rushwa. Ndugu Mganga alikabidhiwa hundi ya shilingi laki moja mnamo tarehe 1 Mei, mwaka wa 1983 Mjini Morogoro na Hayati Mwalimu Julius Nyerere, kwenye kilele cha sikukuu ya Wafanyakazi.

Aidha, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, wa wakati huo alimpandisha cheo Ndugu Mganga kutoka *Sub-Inspector* kuwa *Senior Inspector* hivi sasa Ndugu Hashim Mganga anaishi hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbukumbu kuhusu Serikali kutoa ahadi rasmi ya kumjengea nyumba mhusika bado hazijapatikana. Taarifa zilizopo kuhusu ahadi hiyo zimetokana na mhusika mwenyewe na nakala ya kipande cha gazati chenye picha inayoonyesha akipewa hundi na maandishi yanayoambatana na picha hiyo yanaonyesha kwamba angejengewa nyumba na Serikali. Aidha, nakala mbili za barua alizoandikiwa Ndugu Hashim Mganga kumpongeza moja kutoka kwa Mkuu wa Chuo cha Uandishi wa Habari wakati huo cha Dar es Salaam Marehemu Maganga, kwa niaba ya Jumuiya ya Chuo cha Uandishi wa Habari na Bwana Julius Mkingwa wa Karakana ya Polisi Moshi aliyekuwa anafahamiana vema na Ndugu Mganga. Habari hii pia iliripotiwa katika gazeti la *Daily News* la Mei 8 mwaka wa 1983.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa nimjibu Mheshimiwa Mbunge swali lake kama ifuatavyo:-

Kwanza Serikali mara nyingi inachukua fursa hii kumpongeza Ndugu Hashim Mganga kwa kitendo chake cha kizalendo na uadilifu cha kukataa rushwa aliyokuwa apewe. Kilikuwa ni kitendo cha heshima kwa utu wake na utumishi wake na ndiyo maana Serikali ikampa zawadi ya shilingi laki moja kiasi ambacho alikuwa amekataa alipopewa kama rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali siku zote inatambua na kuthamini mchango wa wananchi walio mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya rushwa na ndiyo maana ilimzawadia *Senior Inspector* wa Polisi Mstaafu Hashim Mganga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haina hulka ya kupuuzia ahadi halali inazozitoa kwa wananchi wake. Hivi sasa tumeagiza kufuatilia vyombo vyetu kufuatilia kumbukumbu mbalimbali kwa lengo la kubaini na kuthibitisha ukweli wa kutolewa ahadi ya kujengewa nyumba kwa askari huyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Madeje swali la nyongeza, na litakuwa hilo tu basi.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yanaleta matumaini kwamba hatimaye ahadi ya Serikali itatimizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kufichua maovu ya rushwa na ufisadi mara nyingine huwa hata yanaweza kuhatarisha maisha ya mtu na maslahi yake na kwa kuwa ni kitendo ambacho kinahitaji ujasiri mkubwa. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuanzisha utaratibu mzuri ambao utawatambua majasiri kama hao na kwa wakati muafaka? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika Serikali ndivyo inavyofanya, isipokuwa suala hili tunasikitika sana kwamba tatizo lililotokea ni kwamba agizo lililotolewa halikueleweka limeelekezwa kwa Idara ipi ya Serikali.

Idara ya Polisi, au Hazina au Ofisi ya Waziri Mkuu. Kazi inayofanyika sasa hivi ni kutambua ni Idara ipi ya Serikali ilikuwa imeagizwa ifanye hivyo wakati huo.

**NAIBU SPIKA:** Nadhani hukujibu sehemu ya pili ya swali lake kwamba je, hamtaona utaratibu wa kufanya motisha?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – UTAWALA BORA:** Samahani Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu motisha. Serikali ina utaratibu huo na ndiyo maana ilimkabidhi *Inspector* Mstaafu wa Polisi Mganga, shilingi laki moja wakati huo ambapo haikuwa haba sana.

Na. 78

**Jengo la Kutunzia nyaraka za askari Wastaafu**

**MHE. AMEIR ALI AMEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa jengo la kutunzia nyaraka za askari wastaafu *PC* limechakaa sana na majalada yamefurika na nafasi imekuwa finyu sana na kusababisha watumishi kushindwa kufanya usafi na hivyo kusababisha kuwepo kwa wadudu wa kila aina na wengine hatari kwa wale wanaohudumia ofisi hiyo na pia usalama wa wafanyakazi na nyaraka kuwa mdogo na kwa kuwa nyumba ya jengo hilo kuna sehemu ya kutupa taka kila siku na kila siku moto unawaka ukiteketeza taka hizo na washughulikiaji wa jalada hilo ni wafungwa:-

Je, Serikali haijaliona tatizo hilo na kama ilimeliona imechukua hatua gani za makusudi kuzinusuru nyaraka hizo na afya za wafanyakazi?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge wa Fuoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa jengo la kutunzia nyaraka za askari wastaafu (*Pension and Gratuity)* limechakaa sana na majalada yalikuwa yamefurika na kusababisha watumishi kushindwa kufanya usafi hivyo kuhatarisha afya za askari na nyaraka zilizokuwemo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua tatizo la uchakavu wa jengo hilo hivyo imeanza kuchukua hatua mbalimbali kwa lengo la kupunguza mlundikano wa nyaraka za Wastaafu katika Ofisi hizo ili kuwawezesha watumishi kufanyakazi katika mazingira yaliyo salama kwa afya zao, hatua hizo ni pamoja na:-

(a) Tumeanzisha programu inayoitwa kwa lugha ya Kiingereza *decongestion* inayohusika na uondoaji majalada ya zamani ambayo hayahitajiki tena na kuyapeleka sehemu nyingine kuhifadhiwa na hivyo kutoa nafasi kwa ofisi hizo kusafishwa na watumishi kupata nafasi ya kutosha kufanyia kazi.

(b) Serikali inakusudia kulibomoa jengo hilo na kujenga Wizara ya Usalama wa Raia ambapo baada ya kukamilika kwa ujenzi huo Idara na Vitengo vilivyopo katika jengo hilo vitapatiwa pia Ofisi za kufanyakazi. Lakini kukamilika kwa Ofisi hizi kutategemea kupatikana kwa fedha zinazokusudiwa kutoka katika Bajeti ya Serikali.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa kwa majibu mazuri aliyoyajibu Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa nyaraka zote za wastaafu zinafikia hapo na kusababisha mlundikano wa mafaili na pia husababisha uchelewaji wa huduma. Je, Mheshimiwa Waziri haoni sasa kuna haja ya kuzitawanya kazi hizi katika Kanda?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kutumia Kanda ni nzuri tu pale ambapo tutaweza kujitosheleza kwa mahitaji

yote muhimu. Hivi sasa Jeshi la Polisi lina mpango maalum wa kuweka mtandao wa kompyuta unaojulikana kama *human resource data base* kwa ajili ya kumbukumbu za watumishi.

Hivyo naamini mara baada ya kumaliza mtandao huu itakuwa rahisi kuwasiliana na Kanda na kufanya malipo ya wastaafu kwa rahisi zaidi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira wakati tukishughulikia tatizo hili.

Na. 79

**Uhitaji wa eneo la Ofisi ya Polisi (W) Manyoni**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa Ofisi ya Polisi Wilaya ya Manyoni iko kwenye majengo ya Halmashauri ya Manyoni – Idara ya Afya:-

Je, ni lini Serikali italipa jeshi la Polisi eneo kwa ajili ya kujenga Ofisi zake za kudumu?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kituo cha polisi cha Wilaya ya Manyoni kiko katika majengo ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ambayo yalikuwa yanatumiwa na Idara ya Afya kama kituo cha Afya. Aidha askari polisi wa kituo hicho wanaishi katika nyumba ambazo zilikuwa zinatumiwa na Idara ya Maliasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi la Polisi kupitia Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida linafuatilia upatikanaji wa eneo rasmi kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Ofisi za Polisi, Wilayani Manyoni, pamoja na Kambi ya Askari.

Maombi ya kupatiwa eneo la ukubwa wa ekari 10 yamekwishapelekwa kwa Ofisa wa Ardhi Wilaya ya Manyoni ili jeshi la Polisi liweze kupatiwa eneo hilo. Wakati tunasubiri kupatikana kwa kiwanja hicho na fedha za ujenzi wa ofisi hizo, jeshi la Polisi Wilayani Manyoni litaendelea kutumia majengo hayo kwa huduma za kipolisi.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa Wilaya ya Manyoni haina tatizo la uhaba wa ardhi. Je, Serikali itakuwa tayari kutenga fedha za kujenga Kituo cha Polisi pamoja na makazi ya askari mara eneo litakapopatikana?

Pili, kwa kuwa majengo hayo yanayotumika sasa kama Kituo cha Polisi cha Wilaya, bati zake zinavuja sana. Je wakati wanasubiri kupatikana kwa eneo Serikali

itakuwa tayari kufanya jitihada za haraka kukarabati mabati hayo ili askari hao waweze kufanya kazi zao kwa usahihi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la ujenzi wa nyumba za askari na Kituo cha Polisi jambo la msingi hapa ni kupatikana kwa kiwanja. Kama nilivyosema katika jibu langu la awali kwamba mara tutakapopata kiwanja taratibu za ujenzi zitaanza pale ambapo uwezo wa Bajeti ya Serikali utaruhusu.

Hata hivyo, hivi sasa Jeshi la Polisi linao mpango maalum wa maboresho ndani ya Jeshi la Polisi na katika suala la maboresho pia linatilia mkazo ujenzi wa vituo vya jeshi la polisi na nyumba za askari. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba programu ipo na mara tutakapopata fedha kazi hii itaanza mara moja kule Singida.

Kuhusu mabati yanayovuja, suala tumelipokea, namwomba Mheshimiwa Mbunge pia ashirikiane nasi katika kusaidiana kutafuta wafadhili mbalimbali hasa kwa njia hii ya Polisi Jamii ambapo watu wengi hujitolea kusaidia jeshi la polisi. Kwa upande wetu Serikali tutafanya kila jitihada kuezeka pale hali itakapokuwa nzuri.

Na. 80

**Miradi ya Umwagiliaji**

**MHE. FELIX N. KIJIKO** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais katika kilele cha siku kuu ya wakulima (Nane Nane) alisisitiza kuwa na mapinduzi ya kijani na kwamba katika kipindi cha miaka saba cha kutekeleza *ASDP* Tanzania ilikusudia kufikisha hekta milioni moja za kilimo cha umwagiliaji lakini mpaka sasa ni hekta 264,388 tu zinazomwagiliwa na kwa kuwa matatizo ya kilimo ni mengi:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba inafaa kuwa na Idara au Wizara ya Maji na umwagiliaji iliyoitwa *WD & ID* ili iwe Wizara moja Wizara tu ya kuendeleza na kusimamia rasilimali ya maji na Wizara ya Kilimo ikabaki kusimamia mazao na Ushirika?

(b) Je, utekelezaji wa mradi wa umwagiliaji wa mabonde ya Ruguzye, Kumngondogondo na Luiche utatekelezwa lini ili kuwapa moyo wananchi wa Mkoa wa Kigoma wanaoishi kwa kutegemea kilimo duni?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mbunge wa Muhambwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, jukumu la uundaji wa Wizara sio kazi ya Wizara, bali ni kazi ya Mheshimiwa Rais ambaye mpaka sasa ameona ni sahihi Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kuwa na Idara ya Umwagiliaji.

Aidha, ningependa ifahamike kwamba katika umwagiliaji licha ya ujenzi wa miundombinu, ufanisi wake unakamilika kwa kuwa na matokeo ya ongezeko la uzalishaji na tija katika mazao.

Aidha, ingefaa ieleweke pia kwamba mafanikio ya *ASDP* hayawezi kupatikana kwa Wizara ya Maji kuwa na Idara ya Umwagiliaji bali ni upatikanaji na uwezo wa kifedha kutekeleza majukumu yaliyopangwa na kupewa kipaumbele.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji wa mabonde ya Ruguzye, Kumgondogondo na Luiche, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa utekelezaji umekwishaanza kufanyika katika mwaka huu wa fedha wa 2007/2008, ambapo hatua zifuatazo zimefikiwa:-

(i) Bonde la Kumgondogondo tayari limefanyiwa upimaji na kutayarisha ramani *(Topographical Map).* Aidha usanifu wa miundombinu unaendelea kufanywa na wataalam wa Kanda ya Umwagiliaji ya Tabora.

(ii) Mabonde ya Luiche na Ruguzye yametengewa fedha za kufanyia upembuzi yakinifu na usanifu kwa mwaka huu wa 2007/2008. Kukamilika kwa kazi hii kutafuatiwa na hatua ya kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika. Nitakuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza kwa kuwa Mkoa wa Kigoma haujawahi kusaidiwa chakula hata siku moja kwa sababu ya jitihada za wananchi wa Mkoa huo. Na kwa kuwa Serikali kuanzia mwaka 80 iliji-*commit* kusaidia miradi miwili mikubwa ya Bonde la Luiche na Bonde la Ruguzye kwa ajili ya kuendeleza miradi mikubwa ya kilimo cha umwagiliaji ahadi ambazo hazitekelezeki ama hazijatekelezwa mpaka sasa. Serikali inatamka nini kuhusu hili ili kuwasaidia wananchi wale?

Swali la pili, je Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba kwa makusudi mazima kuna haja ya kuwa na programu ya kuanzisha ama kuweka Mkoa wa Kigoma kuwa na ghala la chakula la Taifa kwa sababu ni mkoa ambao hauna matatizo ya chakula? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya swali la msingi, mradi wa Ruguzye tayari umeshaanza kufanyiwa kazi.

Hata katika hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Kilimo atauona umo na kwa hivyo Serikali tayari imeshaanza kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya mradi huo wa Ruguzye. Hii ina maana kwamba mradi huo utaendelea hata katika mwaka wa fedha ujao. Kwa hiyo, naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Kijiko.

Kuhusu Luiche, hadithi ni hiyo hiyo kwamba tayari Luiche ilifanyiwa kazi siku nyingi miaka ya nyuma kulikuwa na makampuni yalikwishafanya kazi katika eneo hilo Kampuni ya *TISCO* hata Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimefanya siku za hivi karibuni. Tunachokifaya sasa ni kuangalia zile tathmini zilizokwishafanywa nyuma na kuziongezea zifikie hali ilivyo sasa katika miaka hii. Lakini nataka nimhakikishie kabisa kwamba mradi wa Luiche nao kwanza kwa ukubwa wake utatekelezwa katika ngazi ya Taifa.

Kuhusu swali la pili la Programu ya kufanya Mkoa wa Kigoma kuwa ghala la nafaka. Mimi nadhani hakuna tatizo lolote wala hatungoji Serikali itamke kwamba sasa Mkoa wa Kigoma uwe ghala la Taifa la nafaka. Kinachotakiwa ni Mkoa wa Kigoma kuandaa programu mzuri ya kilimo na programu hiyo mimi ningeshauri kwamba iwe katika sura mbili. Moja, kwa ajili ya wakulima wadogo wadogo kwa sababu wao wataweza kutumia fedha za *DADPs* chini ya *SDP*.

Lakini la pili, ni kwamba lazima kuwe na programu ya wakulima wa kibiashara ambao watakuwa wanalima kilimo chao kwa kutumia fedha zao wenyewe.

Labda nikimalizia naomba niseme kwamba uko utaratibu katika Mkoa wa Kigoma na Mikoa mingine kwa watu kuwa na mashamba makubwa ambayo hayafanyiwi kazi lakini wanasema wana mashamba. Ukienda kutembelea mtu anasema ana eka 1,000 kumbe si shamba ana pori la eka 1,000.

Mashamba haya ni vema basi yaainishwe yaingizwe katika programu ili yaweze kutekelezwa na kwa kufanya hivyo Mkoa wa Kigoma nina hakika tutaufanya kuwa ghala la Taifa. Kwa hiyo, Mkoa wa Kigoma uandaye programu nzuri na nina hakika Serikali ita-*respond*. *(Makofi)*

Na. 81

**Uanzishwaji wa Sekondari za Kidato cha Tano na Vyuo Vikuu nchini**

**MHE. JUMA A. NJWAYO (K.n.y. MHE. RAYNALD A. MROPE)** aliuliza:-

Kwa kuwa kutokana na mafanikio ya mpango wa MMES yamesababisha ufunguzi wa shule nyingi za sekondari nchini hivyo kuwepo kwa uhaba wa madarasa ya kidato cha tano na vyuo vikuu nchini:-

(a) Je, Serikali ina mpango wa kuanzisha sekondari za kidato cha tano (5) za wananchi kwa Wilaya hasa katika Mikoa ya Pembezoni kama Mtwara?

(b)Je, kwa nini Sekondari za Kidato cha Tano (5) za kitaifa kwa mfano Ndanda, *Masasi Girls* na Chidya zilizopo Wilaya ya Masasi zisipewe idhini ya kupokea wanafunzi wengi zaidi kutoka Sekondari za wananchi za maeneo ya Mikoa ya Lindi na Mtwara ili kupunguza kwa kiasi kikubwa hali ya kutokuwepo kwa wanafunzi katika vidato vya juu na vyuo vikuuu nchini kwa wanafunzi wa Mikoa hiyo iliyo nyuma kimaendeleo?

(c) Je, kuna mpango gani wa kuanzisha vyuo vikuu katika maeneo ya Kusini ili kuwepo na uwiano wa wataalam watakaoendesha shughuli za maendeleo tofauti na hali ilivyo sasa ambapo mikoa hiyo ina upungufu mkubwa wa wataalamu wa fani mbalimbali?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI(MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) umekuwa na mafanikio makubwa katika kuongeza nafasi za kujiunga na elimu ya sekondari ya kidato cha kwanza hadi cha nne. Serikali ina mpango wa kupanua nafasi za kidato cha tano na sita kila mwaka kwa nchi nzima kutegemea uwezo wa Serikali. Ili kufanikisha azma hiyo kuna taratibu zilizowekwa kwa baadhi ya shule kupewa hadhi ya kuwa na kidato cha tano. Aidha, kwa kuzingatia agizo la Mheshimiwa Rais kuwa kila Tarafa iwe na angalau shule moja ya sekondari ya Kidato cha tano na sita, Wilaya ya Masasi nayo itanufaika na mpango huo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, shule za kidato cha tano na sita ni za kitaifa na hupokea wanafunzi kutoka sehemu mbali mbali kulingana na ufaulu wao. Sio rahisi kwa kanda moja kutosheleza katika machaguo *(combination)*.

Serikali huwachukua wanafunzi wa kidato cha tano waliofaulu bila kujali wanakotoka. Suala la umbali huzingatiwa ili kuwapunguzia wazazi gharama ya usafiri. Hivyo wanafunzi wanaostahili kujiunga na kidato cha tano kutoka Mikoa ya Mtwara na Lindi hupata nafasi sawa kama wanafunzi wengine nchini kulingana na ufaulu wao.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokuwepo kwa chuo kikuu maeneo ya Kusini siyo sababu ya kuwepo kwa upungufu wa wataalam wa fani mbalimbali katika maeneo yao. Vyuo vilivyopo hapa nchini ni vya kitaifa na kimataifa na si vya maeneo au mikoa ambamo vijengwa.

Hata hivyo, vyuo vikuu vilivyopo nchini hudahili wanafunzi kutoka katika Mikoa yote kulingana na ufaulu wao. Aidha, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kina tawi Mtwara na Lindi.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Lakini hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa hali ya walimu katika shule za sekondari ni mbaya sana kwa mikoa ya Kusini kiasi cha baadhi ya shule kuwa na mwalimu mmoja tu.

Je, kuna mpango gani wa dharura wa kuondoa hali hii?

Pili, kwa kuwa Wilaya ya Tandahimba ilishatengeneza mazingira mazuri ya kuwa na kidato cha tano katika shule za Sekondari ya Mahuta na Tandahimba Mjini. Je, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, inaweza kuliahidi Bunge hili vijana watakaochaguliwa awamu hii kwenda kidato cha tano wakawepo katika shule za sekondari za Tandahimba na Mahuta? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya walimu katika nchi yetu kutokana na ongezeko la shule za sekondari bado kuna upungufu mkubwa na suala hili tumekuwa tukilisema mara kwa mara.

Lakini mwezi huu wa pili walimu watamaliza katika vyuo vyetu vya ualimu, walimu wa *diploma*. Tunaomba kila mkoa ujipange vizuri kuwapokea wale watakaopangwa katika mikoa yao. *(Makofi)*

Kuhusu suala la shule ya Tandahimba na Mahuta kuandaliwa kuwa shule za *A Level*. Kama wameshaomba tayari na kupeleka barua katika Wizara ya Elimu suala hili litachunguzwa tutapeleka Wakaguzi waende wakazikague waone kama kweli zinafaa, zina mabweni na zina vifaa vile ambavyo vinaweza vikatumika na wanafunzi na kama mahitaji haya yatatosheleza Wizara itapanga wanafunzi katika shule hizo, kama wameshaomba tayari. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kunipa nafasi hii na mimi niongezee kidogo kwa majibu mazuri aliyotoa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kuhusu uhaba wa walimu.

Kama alivyosema Naibu Waziri kwamba mwezi wa pili wanatoka walimu wapya wa Stashahada zaidi ya 3,400 na tunategemea pia mwezi wa tano kupata zaidi ya walimu 6,000. *(Makofi)*

Na mpaka mwisho wa mwaka tunategemea kupata zaidi ya walimu 12,000. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria Serikali inachukua jitihada ya kukabiliana na suala hili.

Halafu pia kwa sasa hivi Wizara ya Elimu inaandaa mkakati wa upatikanaji wa walimu ambao nadhani tutautangaza baadaye baada ya kukamilika ili kuhakikishia

Watanzania kwamba shule zilizojengwa za Sekondari na wanafunzi walioko pale wasiwe na wasiwasi Serikali inachukulia kwa uzito unaostahili suala la upatikanaji wa walimu. *(Makofi)*

Halafu pia kuhusu suala la nyongeza la kuhusu shule kuwa *A Level* yaani kupandishwa kuwa *A Level*. Sasa hivi kuna timu kutoka Wizara ya Elimu inazunguka Mikoani kuangalia ni shule gani ambazo zinastahili kupokea vijana wa kidato cha tano ambacho tunategemea shule kufunguliwa tarehe 31 Machi, 2008.

Kwa hiyo, shule hizo hazikuwamo kwenye orodha kama kwa bahati mbaya hazikuomba hazitakaguliwa, lakini kama zimeomba sasa hivi timu inakagua ili ihakikishe kwamba shule zinazochukua kidato cha tano zinastahili. Kwa sababu sifa ya shule za kidato cha tano kwa vyovyote vile sio sawa sawa na kidato cha kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shule hizo zinatakiwa ziwe mahali ambako vijana wanaweza kusoma, walimu wa Shahada tu ndiyo wanaostahili kukaa kule. Ziwe za mazingira ya kuweza kupokea aina hiyo ya walimu na vijana. Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika. *(Makofi)*

**MHE. DR. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, najua si utaratibu kuendelea kuuliza maswali baada ya Waziri kusimama na kujibu ingawaje Waziri angengoja asikie swali langu. Ningependa kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa ni nia ya Tanzania kuendelea kuwafanya Watanzania wawe kitu kimoja, waendelee na ushirikiano na mshikamano; je, Serikali haioni umuhimu wa hizi shule za kidato cha tano na sita zikawa shule ambazo tangu mwanzo zinashughulikiwa na Serikali kikamilifu ili sisi wananchi tubaki na shule za Kata, za sekondari za Kata, za Tarafa, na kadhalika. Lakini hizi za *form five* na *six* ziwe za kitaifa ili wanafunzi waweze kutoka sehemu yoyote ya Tanzania na huko wakaenda kuanza kushirikiana kitafa?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika. Ningependa kuongezea kwa majibu mazuri aliyotoa Naibu Waziri kwamba shule ikishakuwa kidato cha tano, Serikali Kuu inachukua. Kwa hiyo, hata kama wamejenga wananchi kwa kujitolea kwa lengo lile la kujenga utaifa, ikishakuwa na kidato cha tano tayari inachukuliwa na Serikali kuu. Kuanzia chakula, na kadhalika, yote inashughulikiwa na Serikali Kuu. Na kwa lengo hilo hilo la kujenga utaifa, naamini kabisa ziko baadhi ya shule ambazo zilikuwa zinachukua *O Level,* yaani kidato cha kwanza, tutazipunguza ili ziwe *A Level* kwa lengo hilo la kujenga utaifa ili vijana wengi waingie kwenye shule za kitaifa katika kidato cha tano kwa lengo hilo la kujenga utaifa . *(Makofi)*

Na.82

**Tatizo la Uvujaji wa Mitihani**

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALUM** aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo la kuvuja kwa mitihani limekuwa likijitokeza mara nyingi bila kupatiwa ufumbuzi wa kudumu na Serikali; na kwa kuwa taswira inaonesha udhaifu huo unahusisha makundi na ngazi mbalimbali kabla mitihani haijawafikia wanafunzi; na kwa kuwa kigezo cha kuendelea na masomo kwa wanafunzi ni kufuzu mitihani yao kwa kiwango kinachotakiwa:-

(a) Je! ni ngazi gani na shule zipi ziligundulika kushiriki na uvujaji wa mitihani ya darasa la saba, la kumi na la kumi na mbili kwa mwaka 2007 na hatua gani zilichukuliwa kwa wahusika?

(b) Kwa vile tatizo hilo ni la muda mrefu, Serikali ina mikakati gani ya ziada ya kukomesha mapungufu hayo yanayoathiri kiwango bora cha elimu tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salum, Mbunge wa Mtambile, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna uvujaji uliotokea katika mitihani ya mwaka 2007 ya darasa la saba na kidato cha nne inayoendeshwa na Baraza la Mitihani jambo ambalo tunalipongeza sana Baraza. Kilichotokea ni udanganyifu katika mitihani hiyo. Shule za msingi 54, sekondari 58 na vituo 42 vya watahiniwa wa kujitegemea walihusika katika udanganyifu. Watahiniwa waliohusika katika udanganyifu huo wamefutiwa matokeo yao yote ya mitihani. Walimu na wale wote waliowasaidia watahiniwa kufanya udanganyifu wamefikishwa kwenye Mamlaka ya ajira zao kwa ajili ya kuwachukulia hatua za kinidhamu. Uvujaji ulitokea katika mitihani ya kidato cha pili kwenye Kanda ya Mashariki na Kaskazini Mashariki. Mitihani ya kidato cha pili ambayo hutungwa na Wizara na kusimamiwa Kikanda ina lengo la kujua maendeleo ya wanafunzi na kubaini matatizo ili kuchukua hatua rekebishi. Mitihani hii haihusiani na mitihani ya Baraza. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuwafutia matokeo yote ya mtihani wanafunzi waliohusika, mitihani kurudiwa upya na baadhi ya shule na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria waliotuhumiwa kuhusika na uvujaji wa mitihani. Uchunguzi zaidi unaendelea kwa kushirikiana na vyombo vya dola.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati iliyowekwa na Serikali ya kukomesha mapungufu hayo ni pamoja na:-

(i) Kurekebisha utaratibu wa usimamizi ambapo sasa walimu hawaruhusiwi kusimamia mitihani katika shule wanazofundisha.

(ii) Kwa kuwa makini katika kuteua wasimamizi na kutoa semina elekezi kwa wasimamizi wote kabla ya kwenda katika kituo cha kusimamia mitihani.

(ii) Kuimarisha zaidi ulinzi katika hatua zote za uendeshaji wa mitihani kuanzia utungaji, uchapaji, usafirishaji, uhifadhi na usimamizi wa mitihani.

(iii) Kuchukua hatua kali za kinidhamu na kisheria kwa wanaobainika kuhusika na vitendo vya uvujaji na udanganyifu katika mitihani.

(iv) Kuelimisha jamii juu ya athari za udanganyifu kwa mtu binafsi na Taifa.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa matokeo ya mtihani ya kidato cha nne yaliyotolewa wiki iliyopita yalionesha wazi kwamba shule ya *Happy Skillfuls* ya jijini Dar-es-Salaam imefutiwa matokeo, na ilielezwa bayana kwamba walivujisha mitihani kwa taarifa iliyotolewa na Baraza la Mitihani; je, Mheshimiwa Naibu Waziri anatuambia nini juu ya tatizo hili?

La pili, pamoja na matokeo ya mitihani yaliyotolewa juzi na Baraza la Mitihani, kuna idadi ya wanafunzi 2,794 wamesitishwa matokeo yao mpaka pale watakapotoa ada zao; je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kusamehe idadi hii ndogo ya wanafunzi wa familia masikini ili waendelee na masomo yao na hasa pale Rais aliposema kwamba hakuna mwanafunzi atakayekosa masomo kwa sababu ya umasikini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Awali ya yote nimpongeze kwa ufuatiliaji wa makini katika masuala ya elimu, lakini pia nimfafanulie kwamba *Happy Skillful* haikufutiwa matokeo kwa sababu ya uvujaji, udanganyifu. Wale waliopo madarasani wanajua, wanafunzi walikutwa na majibu yaliyofanana na hivyo kutoa kiashiria kwamba ama walikuwa na vitu vinaitwa *"vinondo"* au wenyewe wanafunzi wanaita *"vispea,"* vitu ambavyo wanaingia navyo, majibu wanaingia nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Baraza la Mitihani limesitisha matokeo haya au limeyafungia kwa sababu Baraza linapaswa lilipwe ada, kama halikulipwa ada ni juu ya Mkuu wa Shule kueleza kwa nini? Kwa sababu na lenyewe linajiendesha. Na ili liweze kujiendesha linahitaji ruzuku hiyo ndogo kutoka kwa wale ambao ni wateja wake. Kwa hiyo, uchunguzi unafanyika, ikibainika kwamba wameonewa, ada ililipwa lakini pengine kwa sababu moja au nyingine ama zimetumika vibaya, au hazikufika basi sheria itachukua mkondo wake na wanafunzi watapatiwa majibu yao. Lakini ni baada ya uchunguzi wa kina kufanyika. Hatuwezi tu tukasema tunawasamehe, utaratibu wa kuwasomesha wanafunzi waliotoka kwenye familia duni tunao na mwaka jana katika bajeti tulitangaza kwamba tunawagharimia wanafunzi 42,000. Asante.

Na.83

**Tatizo la Miundombinu – Mbinga Magharibi**

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Jimbo la Mbinga Magharibi, linaambaa kando kando ya Ziwa Nyasa; na kwa kuwa barabara inayoziunganisha Kata na Vijiji ni moja tu, yaani kutoka Lituhi hadi Chiwindi mpakani na Msumbiji; na kwa kuwa ni mwka mmoja tu umepita tangu barabara hiyo ilipotengenezwa kwa kujenga madaraja tangu miaka ya sitini na ndipo watu walianza kusherehekea matunda ya uhuru kwa magari na mabasi kuanza kutoa huduma ya usafiri wa uhakika; na kwa kuwa mvua za vuli za mwaka huu zimevunja tena madaraja hayo yaliyotengenezwa, hali iliyosababisha wananchi kurudia unyonge wao wa kukosa barabara:-

(a) Je, Serikali ina mipango gani ya haraka ya kutengeneza tena barabara hiyo ili kuharakisha maendeleo ya wananchi waishio katika Jimbo hilo?

(b) Je, Serikali itatekeleza lini ahadi yake ya kupeleka meli ya kisasa ili kutatua tatizo la usafiri kwa wananchi wa kando kando mwa Ziwa Nyasa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kapteni John Damiano Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha 2007/2008, Wizara yangu imetenga jumla ya silingi 897,247,720 kwa ajili ya kugharimia kazi mbalimbali katika barabara ya Lituhi, Mbambabay hadi Chiwindi. Kazi zitakazofanyika ni mpamoja na ukarabati kwa gharama ya shilingi milioni 185, matengenezo ya kawaida na ya sehemu korofi (*routine and spot improvement)* zitatumika shilingi 351,112,750 na matengenezo ya dharura kwa gharama ya shilingi 361,118,970. Kazi hizi zitahusisha matengenezo na ukarabati wa tuta la barabara, madaraja *calvats* yaliyoharibiwa na mvua na kufungua mawasiliano ya barabara hiyo.

Ufumbuzi wa kudumu utakaoifanya barabara hiyo ipitike kwa mwaka mzima, ni ujenzi wa *box culvert* na madaraja makubwa kwenye maeneo yote ambayo *culverts* pamoja na *vented drift* zimeshindwa kumudu maji, mawe na magogo makubwa yanayopita. Hivyo basi Serikali itaendelea kutafuta fedha ili kujenga madaraja hayo japo kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Serikali pia inaangalia uwezekano wa kuifanyia upembuzi yakinifu (*feasibility study)* barabara hiyo ili kupata eneo sahihi la

kupitisha barabara na aina sahihi ya madaraja ili kuiepusha barabara na uharibifu wa mara kwa mara unaotokana na mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, kufanya jitihada za makusudi za kuwaelimisha wananchi wanaofanya shughuli za kilimo na kukata miti ya mbao milimani, kuhifandi mazingira ili kupunguza athari zinazotokana na shughuli hizo kwa barabara hiyo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa sasa haina uwezo wa kununua meli ya kisasa kufanya safari zake katika Ziwa Nyasa. Bali inaendelea kuwahamasisha wawekezaji kuwekeza katika ziwa Nyasa kwa kutumia meli za kisasa ambapo hadi sasa hakuna muwekezaji aliyejitokeza kufanya hivyo. Hata hivyo, Serikali kwa kupitia Kampuni ya huduma za meli, *MSC Limited*, inayo meli mbili zinazofanya safari zake katika ziwa Nyasa nazo ni *MV Songea* na *MV Iringa*. Hali ya meli hizo ni nzuri kwa sababu zinafanyiwa matengenezo ya mara kwa mara ili kulinda ubora wake. Kwa mfano, *MV Songea* ilifanyiwa matengenezo mwezi Maei, 2005 na kupandishwa kwenye chelezo cha *Monkey Bay* kule Malawi na mwezi Septemba, 2007 meli hiyo ilifanyiwa matengenezo ya injini pamoja na *gear box* na baada ya matengenezo haya yote meli ilikaguliwa na kupewa cheti cha ubora. Meli hizi zitaendelea kukaguliwa kuhakiki ubora wake kulingana na matakwa ya Sheria ya *Merchant Shipping Act* mwaka 2003.

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimwa Waziri, kwa kuwa meli hizo mbili zina vitu maalum vya kupita ili kurahisisha usafiri katika ziwa Nyasa; na kwa kuwa sasa madaraja yote yale yamevunjika na meli huwezi kuilazimisha ikaenda kwenye kituo chochote kile ili mradi ufike kwenye kijiji; je! sasa lile ombi langu la *Helikopta* lipo tena? Nitapata? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa kapteni Komba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema juhudi zinafanyika ili maeneo haya ambapo madaraja yamekatika tuweze kufanya, tuweze kupashughulikia. Sasa hivi tunachongoja ni mvua hizi ambazo zimenyesha hivi karibuni zipungue ili kazi ya ujenzi wa kukarabati madaraja haya au maeneo haya ya madaraja tuweze kufanikisha. Na kuna maeneo matatu ambayo kwa kweli yana tatizo kubwa kwenye barabara hii.

Sehemu ya Dumbi, Mnywa Maji na Napwachi. Ni maeneo ambayo ndiyo yana ukorofi. Haya meneo ndiyo hela nyingi katika hizi tutajaribu kutengeneza hizi *drifts* ili barabara hiyo iendelee kupitika wakati tunaangalia njia za kudumu za kuweza kurekebisha tatizo la barabara hiyo ambayo kwa kweli ina matatizo makubwa. Sasa suala la *helicopter* sidhani kama ni sera ya Chama Cha Mapinduzi. *(Kicheko)*

Na.84

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege - Nyasurula**

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya kijiji cha Nyasurula Wilayani Musoma ilipima na kudhamiria kujenga kiwanja cha Ndege, je, Ujenzi wa kiwanja hicho utaanza lini?

**NAIBU WAZIRI MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni za udhibiti wa usalama wa anga la Tanzania za mwaka 2003 (*Tanzania Air Navigation Regulations of 2003)* chombo au Taasisi yoyote inaruhusiwa kujenga na kumiliki kiwanja au viwanja vya ndege katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, chombo au taasisi husika inapaswa kuomba kibali cha kujenga kiwanja na kumiliki kiwanja hicho kutoka kwa Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga Tanzania (*TCAA). TCAA* itaruhusu kujengwa kwa kiwanja na umiliki wake baada ya kuzingatia masuala yafuatayo:-

(a) Umiliki halali wa ardhi, yaani chombo au taasisi husika kuonesha hati au ushahidi wa kumiliki ardhi ya eneo linalokusudiwa kujengwa kiwanja cha ndege.

(b) Maombi ya chombo au taasisi kupitishwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na Mkoa husika ;

(c) Maombi ya chombo au taasisi kupitishwa na Kamati ya Mazingira ya Wilaya na Mkoa husika;

(d) Maelezo kuhusu matumizi ya kiuchumi ya kiwanja, uwezo wa taasisi wa kujenga kiwanja na kukiendesha;

(e) Baada ya kuridhika na masuala hayo, Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga Tanzania hutuma wataalamu wake kwenda kwenye eneo husika na kufanya utafiti kwa kutumia vigezo vya kiufundi. Na endapo itabainika kuwa hakuna tatizo la kiufundi, kibali cha ujenzi wa kiwanja cha ndege hutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Manyini, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa haijulikani ni lini ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Nyasurula utaanza, kwani Serikali ya kijiji cha Nyasurula haijawasilisha maombi ya ujenzi wa kiwanja kwa Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga Tanzania na idhini kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachoweza kushauri ni kwa Mheshimiwa Mbunge kuitaka serikali ya kijiji cha Nyasurula kuwasilisha maombi yake kwa Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga Tanzania kama kweli kijiji kinataka kujenga kiwanja cha ndege ili maombi hayo yaweze kushughulikiwa. Maombi ya Serikali ya kijiji yazingatie taratibu ambazo nimezieleza hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaamini kwamba kwa kuwa kijiji cha Nyasurula kimedhamiria kujenga kiwanja cha ndege kitakuwa kimedhamiria pia kutafuta fedha za ujenzi wa kiwanja hicho pamoja na fedha za kukiendesha. Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga Tanzania na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania itakuwa tayari kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu ujenzi huo.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Asante Mheshimiwa Naibu Spika, kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, yasiyoridhisha ningependa Naibu Waziri, ahakikishie Bunge hili kwamba kauli zote zilizokuwa zikitolewa na Serikali kupitia viongozi wake kwamba uwanja ule wa ndege wa Musoma ambao ni mdogo na uko katikati ya mji utahamishiwa katika Wilaya ya Musoma vijijini katika kijiji cha Nyasurula; je, kauli hizo Naibu Waziri anataka kusema ni za uwongo?

Swali la pili, kwa kuwa umuhimu wa uwanja ule unafahamika na pale ulipo ule uwanja wa Musoma kwanza hauna *running way* ya kutosha lakini vilevile uwanja ule ni wa vumbi na wakati mwingine mara nyingi ndege zinashindwa kutua. Halikadhalika gari linalotumika kama zimamoto ni bovu, japokuwa linatembea lakini haliwezi kufanya chochote, ambavyo ni sambamba na vifaa vingine vya usalama. Je, Waziri anatoa kauli gani kuhusiana na uwanja huo sasa ambao kwa kweli unahatarisha maisha ya wananchi wa Mkoa wa Mara na Musoma kwa ujumla.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda nijibu masuala mawili kwa pamoja ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge , kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitofautiane na Mheshimiwa Mbunge, kwamba uwanja wa ndege wa Musoma, unahatarisha maisha sio kweli na sio sahihi. Uwanja wa ndege wa Musoma unashughulikiwa kama vinavyoshughulikiwa viwanja vya ndege vingine vyote nchini. Hapa Tanzania tuna viwanja vya ndege 63 na tuna viwanja vidogo vidogo zaidi ya 300 na vyote vinafanya kazi kama vinavyotakiwa. Na ninapenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kitu cha mwanzo tunachokijali sisi ni usalama wa abiria na usalama wa mizigo yao na saa zote tunahakikisha viwanja vile vinashughulikiwa ipasavyo.

Katika Mkoa wa Mara Mheshimiwa Naibu Spika, tuna viwanja kama sita vidogo vidogo. Kuna Bunda, Busegwa, Tarime, Mugumu, *North Mara* na Shirati Hospitali. Hivi

ni vya *private* na tunahakikisha *TCAA* inavipitia kila mwaka. Isitoshe kwenye masuala ya Musoma *Airport* tunao mpango wa kumalizia uzio, tunao mpango wa kuziba na kutengeneza mashimo. Na hivi juzi tu tumepeleka shilingi milioni 20 kwa ajili ya matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunataka kutanua *VIP Lounge,* na tumeshatenga shilingi milioni 50 kwa ajili ya kazi hiyo. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na nilihakikishie Bunge lako tukufu kwamba Wizara ya Miundombinu kupitia Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga inafanya kazi nzuri sana na ndio maana viongozi wengi katika sekta hii wamepata nafasi ya kujiunga na kuchaguliwa katika *ICAO* ambayo ni chombo kikuu kinachoshughulikia masuala ya usafiri na usalama wa anga. Na kama nilivyomjibu juzi kwamba Tanzania imepata hati safi katika masuala ya usafiri wa anga. *(Makofi)*

Na.85

**Utendaji wa Kazi wa *TASAF***

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO** aliuliza:-

Je, kuna mahusiano gani ya kiutendaji kati ya *TASAF* na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mipango Uchumi na Uwezeshaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Muundo wa utekelezaji wa *TASAF* awamu ya pili umezingatia kuhusisha Wizara na sekta zote husika. Hii inatokana na kwamba *TASAF* inafadhili miradi ya jamii kutoka sekta mbalimbali Tanzania Bara na Visiwani. Kwa utaratibu huo Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, inawakilishwa na mjumbe mmoja kwenye Kamati ya Taifa ya Uongozi ya *TASAF*. Vilevile kuna uwakilishi wa ofisa mmoja kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa masuala ya *TASAF* ya kiutendaji kwenye timu ya wataalamu kutoka sekta mbalimbali *(Sector Expert Teams).* Wataalamu wa sekta husika wameshirikishwa kutoa utaalamu katika miradi inayoibuliwa na kutekelezwa na wananchi ili iwe endelevu na yenye kuzingatia kanuni na viwango vya kisekta. Asante.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Asante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri amethibitisha kwamba *TASAF* inahusiana na Maafisa wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kushiriki katika masuala mbalimbali ya uhamasishaji wa kitaifa. Lakini katika utafiti niliofanya

nimegundua ya kwamba *TASAF* haiwashirikishi Maafisa Maendeleo ya Jamii ambao ndio kiungo kikubwa kwa wananchi katika kuwahamasisha katika masuala yote ya maendeleo katika ujenzi wa vyoo kwa mfano, ujenzi wa mashule, kilimo, na mambo mbalimbali.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka Waziri anieleze, ni sababu zipi zinaifanya *TASAF* isishirikishe Maafisa wa Maendeleo ya Jamii katika Wilaya, badala yake inachukua Maafisa wengine ambao hawana taaluma hiyo?

(b) Kwa kuwa Maafisa Maendeleo ya Jamii ni watu muhimu sana katika uhamasishaji na itakumbukwa kwamba hata wazazi wetu zamani walipoanza kujifungua katika hospitali kazi kubwa ilifanywa na maafisa hawa. Sasa nataka kujua ni wilaya ngapi? Wilaya ambazo hadi leo hazijapata maafisa hawa, Serikali ni lini itasambaza Maafisa hawa Tanzania nzima ili iwasaidie wananchi katika uhamasishaji wa maendeleo?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, naomba kujibu masuala mawili ya Mheshimiwa Chaurembo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika suala la msingi, majibu yangu ya msingi ni kwamba *TASAF* inashirikisha si tu Maafisa Maendeleo ya Jamii, bali wataalamu wote katika ngazi ya Wilaya. Wataalamu wa Elimu, Wataalamu wa Miundombinu, kila aina wanashirikishwa. Wizara yangu haina taarifa kwamba *TASAF* katika ngazi ya Wilaya, na kwa kweli kwa uhakika *TASAF* katika ngazi ya Wilaya inawakilishwa na Halmashauri yenyewe. Hata wale wafanyakazi wameajiriwa na Halmashauri yenyewe. Na kama hakuna wataalamu wanaoshirikishwa, tutafanya utafiti na kuweza kuelewa na kuchukua hatua zinazopaswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wilaya ngapi ambazo hazina Maafisa wa Maendeleo ya Jamii, hili suala linatakiwa takwimu. Ndugu Mheshimiwa Mbunge, nakuomba fika ofisini tutampatia. *(Makofi)*

Na. 86

**Kuinua Hali ya Uchumi wa Watanzania kupitia Mikopo**

**MHE. BERNADETA MUSHAHU** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi nyingi zaidi zilizo maskini wananchi wake huendelea kwa kupatiwa mikopo (*Microfinancing);* na kwa kuwa mfuko wa uwezeshaji Tanzania ulianzishwa ili kuinua hali ya uchumi wa watanzania wengi ambao ni wahitaji:-

(a) Je, ni kiasi gani cha mkopo kilitolewa na kwa wananchi wangapi wa Mkoa wa Kagera katika mwaka 2007?

(b) Je, kwa nini utaratibu wa pili wa Serikalil wa kuipatia *SCULT* na benki za wakulima fedha ili ziwakopeshe wananchi haujaanza?

(c) Kwa kuwa wakopaji ni wengi na pia wale waliokwishakukopa wanarudisha mikopo yao; je, kwa nini benki za *NMB* na *CRBD* haziendelei na utaratibu wa kuwakopesha wajasiriamali wengine?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Katika awamu ya kwanza ya Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi hadi kufikia tarehe 30 Novemba, 2007 Benki za *CRDB* na *NMB* zilitoa jumla ya shilingi bilioni 2.18 kwa wajasiriamali 1,288 katika Mkoa wa Kagera. Kati ya wajasiriamali hao, 317 ni wanawake 971 na ni wanaume.

Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 1.75 kilitolewa kwa benki ya *NMB* na kiasi cha shilingi bilioni 429 kilitolewa na benki ya *CRDB*. Katika Mkoa wa Kagera mgawanyo huo wa mikopo Kiwilaya unaonyesha kuwa Wilaya za Biharamulo, Karagwe na Bukoba Mjini zilipata mikopo juu ya matarajio ya Kiwilaya ya shilingi milioni 250 kila Wilaya. Wilaya za Ngara na Muleba hazikufikia matarajio Kiwilaya ambapo Wilaya ya Bukoba Vijijini na Misenyi hazikupata mikopo kabisa. Kwa ujumla Mkoa wa Kagera umekuwa wa tano kwa kupata mikopo mingi ukilinganisha na Mikoa mingine.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya pili ya Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imekwishaanza. Mpango huu wa awamu ya pili umehusisha asasi 14 kama ambavyo serikali ilijibu swali la namna hii jana. Asasi hizo ni *Akiba Commercial Bank*, Benki ya Posta, *Kagera Farmers Cooperative Bank Limited, Kilimanjaro Cooperative Bank, SCULT (1992) Limited*, Benki ya Wananchi Mbinga, *Pride Tanzania*, Benki ya Wananchi wa Mufindi, *Azania Bank*, Shirika la Dunduliza, *Uchumi Commercial Bank, Presidential Trust Fund* na Benki ya Wananchi Mwanga na Benki ya *CRDB.* Uzinduzi wa awamu hii ulifanyika katika Wilaya ya Kilosa, Mkoa wa Morogoro tarehe 31 Desemba, 2007 ambako *Akiba Commercial Bank* ilitoa mikopo ya kwanza kwa *SACCO* tatu za *MMK SACCOS*, Msowelo *SACCOS, Faraja Women SACCOS* ya Gairo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *SCULT* na benki za wananchi au za jamii ni miongoni mwa vyombo vilivyoteuliwa kutoa mikopo katika awamu ya pili ya mpango huu na zinakamilisha maandalizi ya utoaji wa mikopo hiyo. Inatarajiwa kuwa mara asasi zote zilizoteuliwa zitakapokuwa zimekamilisha maandalizi zitaanza kutoa mikopo bila kuchelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mgawanyo wa fedha za awamu ya pili, kipaumbele kimepewa kwa Wilaya 21 ambazo hazikupata kabisa na Wilaya nyingine

46 zilizopata kiasi kidogo katika awamu ya kwanza ili kila Wilaya iweze kufaidika na mpango huu.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, *CRDB* inaendelea kutoa mikopo kwa wajasiriamali katika awamu ya pili. Aidha, *NMB* kwanza inafanya tathmini ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ili iweze kuamua na kisha itajadiliana na Serikali kuhusu uwezekano wa kuendelea kutoa mikopo katika awamu ya pili.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Asante sana Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwanza kwa kuwa katika awamu ya kwanza Wilaya waliyopata hizi hela za uwezeshaji ni chache na katika Wilaya moja mimi haiingii akilini kwamba mtu fulani kama amekopa basi umaskini unaondoka kwa mtu mwingine. Kwa nini sasa Serikali isiendelee kutoa pesa hizo za uwezeshaji kwa kila mtu katika Wilaya zote? (b)……….!

**NAIBU SPIKA:** Bernadetha, kila mtu kweli?

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Kwa kila mtu anayehitaji.

(b) Kwa kuwa nia ya Serikali ni nzuri na wanaohitaji fedha hizo ni wengi, kwa sababu hiyo sasa imekuwa ni kero, waombaji ni wengi lakini wanaopata fedha hizi ni kidogo. Kwa nini sasa Serikali isiainishe mfuko wa uwezeshaji kati ya vipaumbele sita vya taifa ili kusudi mfuko huu uweze kutengewa hela nyingi za kutosha kutoka kwenye bajeti ijayo?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI (MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO):** Mheshimiwa Naibu spika, kwa niaba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaj, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mushashu, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, azma ya Serikali yetu ni kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo kimsingi inazungumzia juu ya maisha bora kwa kila Mtanzania. Azma hii inatekelezwa kwa azma nyingi, moja ni mikopo kwa wajasiriamali ambao kwa kawaida wasingeweza kupata mikopo hiyo katika Benki. Sasa Mheshimiwa Rais wetu ambaye kwa kweli ndiye ameshika bango hilo kwa kiasi kikubwa aliamua zitolewe hizi shilingi bilioni 21 kila Mkoa. Ukizigawa kwa kila Wilaya unapata wastani wa shilingi 250 kwa kila Wilaya. Ukiendelea kugawa utakuta hizo fedha ni chache sana kadri unavyozidi kuteremka. Lakini Serikali ilisema tuanze na tumethubutu na inavyoonekana kama ni chache. Kama ambavyo Serikali ilivyojibu kupitia Waziri Mkuu, kwamba katika Bajeti ya Serikali ijayo inafikiria kuongeza kiwango hiki kupitia Mfuko wa Uwezeshaji. Ahsante. (*Makofi*)

Na. 87

## Upungufu wa Madaktari Bingwa Wanawake

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu inakabiliwa na upungufu mkubwa wa madaktari bingwa wanawake wa magonjwa mbalimbali; na kwa kuwa magonjwa mengi ya kina mama hasa yale ya uzazi, mfano fistula yamekuwa yakishughulikiwa na madaktari wanaume hali inayosababisha baadhi ya akinamama hususan wa vijijini kuficha magonjwa au kutokuwa wazi hadi wanapoona hali imekuwa mbaya:-

(a) Je, madaktari bingwa wanawake wangapi wanafanya kazi hapa Tanzania?

(b) Je, madaktari hao wako katika hospitali zipi?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani za kusaidia wanafunzi wa kike wa masomo ya sayansi ili waweze kujiunga na vyuo vya utabibu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAMI WA JAMII** alijibu:

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kuna jumla ya madaktari Bingwa wanawake 21, wanaofanya kazi hapa nchini:-

(a) Madaktari hao wapo katika hospitali zifuatazo:- (i) KCMC 1; Hospitali ya Tumbi Kibaha 1; Hospitali ya Mkoa wa Morogoro1; Hospitali ya Wilaya *St. Francis* Ifakara 1; Hospitali ya Mkoa wa Tanga 1; Hospitali ya Mkoa wa Arusha 2; Hospitali ya Taifa Muhimbili 7; Hospitali ya Mikocheni *Mission* 1; Hospitali ya MOI 2; Hospitali ya Mkoa wa Dodoma 2; Hospitali ya Mkoa wa Mara 1; na Hospitali ya Mkoa wa Ruvuma 1.

(b) Hatua zinazochukuliwa kusaidia wanafunzi wa kike kwa masomo ya sayansi wasome utabibu ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kupunguza alama zinazotakiwa ili kuchaguliwa kujiunga na masomo ya juu;

(ii) Kuwahamasisha wanafunzi wa kike kuchukua masomo ya sayansi;

(iii) Kujenga hosteli karibu na shule ili kuwawekea mazingira mazuri ya kujisomea kwa wanafunzi wa kike ikiwa ni pamoja na wale wanaosoma masomo ya sayansi ili waweze kufanya vizuri katika masomo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, duniani kote isipokuwa katika nchi chache, hususan zile zinazoongozwa na misimamo ya kidini, wanaume kwa wanawake wanaruhusiwa kusomea fani mbalimbali za afya ikiwa ni pamoja na udaktari bingwa na kuwahudumia wagonjwa bila masharti yoyote. Wataalamu hawa hula viapo vya kutumikia taaluma zao pamoja na kutunza siri za wagonjwa. Aidha, zipo sheria zinazowabana wanaotenda kazi zao kinyume na viapo walivyokula. Sheria hizi zinasimamiwa na Mabaraza ya taaluma husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashauri akina mama wote nchini wasisite kuwaona madaktari wa kiume pale wanapokuwa na matatizo mbalimbali ya kiafya ikiwemo *fistula* ili waweze kupata huduma. Ahsante.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba maswali mawili kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa tatizo hili la uchache wa madaktari hapa Tanzania ni la muda mrefu:-

(a) Je, Wizara sasa ipo tayari kuanzisha *paramedical trainee* kwa wanafunzi wale wa kike wanaopata *division three* ili waweze ku- *specialize* kwenye huduma hii ya *fistula*? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa katika majibu ya msingi ni Mikoa michache sana, 10 ambayo ina mabingwa akina mama kwa ajili ya magonjwa ya akina mama na ni Wilaya chache sana; je, sasa Serikali haioni umuhimu wa kuchukua juhudi za haraka na za makusudi kuhakikisha kwenye mgawo wake angalau kila Mkoa unapata daktari mmoja bingwa na baadaye hata iende angalau kila Wilaya? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAMI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba madaktari ni wachache kama nilivyosema. Mpango wa kuwafundisha (*paramedical)* ili waweze kufanya huduma ya *fistula* kwa kweli ni mgumu sana, unahitaji ubingwa kwa sababu tiba ya *fistula* ni tiba inayohitaji bingwa ambaye atakuwa na uzoefu wa kuweza kutibu kwa sababu tatizo la *fistula* ni kubwa. Lakini katika fani nyingine *paramedical* sasa hivi wanatolewa, wanapata mafunzo na wanaendelea kutoa huduma katika maeneo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, kwamba huduma zipelekwe kufika mpaka Wilayani na kwamba kufanyike mpango wa haraka ili kuweza kukidhi mahitaji, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi na nilivyosema pia katika swali la pili ni kwamba huduma za *fistula* zinahitaji watalaamu bingwa na mtalaamu bingwa anahitaji kuwa muda mwingi sana wa kusoma aweze kuwa bingwa. Kwa hiyo, hatuwezi kuifanya haraka au kufanya kama *crush program* ili kuweza kumpata mtalaamu wa kuweza kufanya hii huduma ya kutibu *fistula*. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge. Ahsante, maswali yamekwisha na muda pia umekwisha. Kwanza kabisa leo ni sikukuu ya kuzaliwa Chama cha Mapinduzi, kwa hiyo, ni *happy birthday* kwa Chama cha Mapinduzi kwa leo. Pili, baada ya

matangazo yangu haya mkiangalia *order paper* tunalo azimio la kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa sababu ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *AU*. Kwa hiyo, ni mategemeo yangu kwamba wote mtatulia. Itakuwa ni *ceremony* ndogo tu halafu tutaendelea na Muswada ambao tulianza. Kwa hiyo, nategemea mtatulia kipindi hicho wote.

Tangazo la pili, napenda niwatangaze wageni tulionao. Leo tuna wageni wengi kwa mujibu wa kanuni hasa, tuna wageni hapa Bungeni, Mabalozi wa nchi za *Norway* na *Sweden,* yupo Balozi Jan Bomei wa *Norway* na yupo Balozi *Staffer Henstrain* wa Sweden. Halafu amefuatana na *First Secretaries* wao. *Can you all raise please! First Secretary from Sweden and another one from Norway. Thank you very much. (Makofi)*

*Then,* tuna wageni wengine Wabunge kutoka Afrika Kusini *Eastern Cap Province Members of Parliament*, tunaye Mheshimiwa Mulabandile Diksokwase. I am *not sure whether I am pronouncing it correctly. (Makofi)*

*Then we have* Mheshimiwa Lito Suka. *We have* Mheshimiwa *Hope Helen* Malgasi. *Then we have* Mheshimiwa Pindiwe Clalibe Makuku. *Then we have* Mheshimiwa Bulelwa Tunyiswa, *then we have* Mheshimiwa Hens S.Tandiroso Sogoni na wamefuatana na maafisa wa Bunge kutoka Afrika Kusini, Bwana Donald S. Nyile. Tena tunaye Bwana Jerome Godfrey, *then we have B. Unathi Milie, so you are all welcome to the Tanzania House and I am sorry for pronouncing your names incorrectly because some of them are very difficult to pronounce. Together with our guests then* tuna vijana 21 wa *TAYOA* waliokuwepo jana, karibuni tena! Kama kuna wageni wengine sijawatamka sikuwa na majina yao. Kuna wageni wengine hawakuwepo. Kwa ujumla tunakaribisha wageni wote katika ukumbi wetu, ni utaratibu wetu kwamba wananchi wanaweza kushiriki shughuli za Bunge kwa wakati wao.

Pamoja na matangazo haya kuna matangazo ya kazi. Kwanza kabisa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu Mheshimiwa Mohamed Misanga anaomba wajumbe wake wakutane leo tarehe 5 kwenye chumba 231 saa tano asubuhi, nadhani baada ya azimio hilo kupita. Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara Mheshimiwa Shellukindo anaomba wajumbe wa Kamati yake wakutane leo saa tano katika ukumbi 428 baada ya azimio.

*Then* Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita, anaomba wajumbe wa Kamati yao wakutane leo tarehe 5 saa 9 alasiri kwenye ukumbi 231.

Halafu Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, naomba wajumbe wakutane saa tano na nusu katika chumba 227 baada ya Azimio. Halafu Katibu wa Kamati ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, anaomba kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM kuwa kikao cha tarehe 5 Februari, sasa kitafanyika tarehe 6 Februari siku ya Jumatano saa mbili usiku yaani baada ya kuahirisha kikao cha Bunge katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine. Waheshimiwa Wabunge, tumepata taarifa ya msiba, mwenzetu Mheshimiwa Richard Nyaulawa amefiwa na mama yake na hivi sasa yuko njiani anaelekea kwenye shughuli ya mazishi. Kwa niaba yenu tunawapa pole familia na yeye mwenyewe kwa msiba huu. Baada ya kusema hayo tunaendelea na shughuli zingine.

## AZIMIO LA BUNGE

## AZIMIO LA BUNGE LA KUMPONGEZA MHESHIMIWA RAIS JAKAYA MRISHO KIKWETE KWA KUCHAGULIWA KUWA MWENYEKITI WA UMOJA WA AFRIKA

**MHE. MUSSA A. ZUNGU – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NCHI ZA NJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha Azimio la Bunge la kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi za Afrika kwenye Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wabunge wote, kwa kunipa fursa hii ili niweze kutoa salamu za pongezi kwa Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti mpya wa Umoja wa Nchi za Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa kuletwa kwa pongezi hizi unatokana na imani kubwa waliyoonyesha viongozi wa Afrika kwa Rais wetu na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waheshimiwa Wabunge mtakavyokumbuka, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika wa Kikao cha Kumi cha Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika kilichofanyika kati ya tarehe 31 Januari hadi 2 Februari 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchaguzi wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ni matokeo ya uamuzi uliochukuliwa na wakuu wa nchi 53 za Umoja wa Afrika wakati wa Kikao cha Nane kilichofanyika Mjini Addis Ababa, Januari, 2007. Kufuatana na utaratibu wa Umoja huo wa kupokezana uongozi wa kanda zake tano hususan kanda ya Kaskazini, Kusini, Kati, Magharibi na Mashariki, Kanda ya Mashariki ina nchi 14 ambazo ni Tanzania, Burundi, Comoro, Eritrea, Kenya, Egypt, Ethiopia, Madagascar, Shelisheli, Uganda, Somalia, Rwanda, Mauritius na Sudan.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa mwaka 2007 ilikuwa ni Kanda ya Mashariki mwa Afrika kumpendekeza Mwenyekiti. Kanda hiyo haikuweza kufanya hivyo kwa sababu Ghana iliomba ipewe heshima hiyo kama ishara ya Bara la Afrika kutambua mchango wa Ghana kama nchi ya kwanza kupata uhuru wa nchi zilizo Kusini

mwa Jangwa la Sahara na kusheherekea miaka 50 ya uhuru wa nchi hiyo. Pamoja na mchango wake katika kuleta ukombozi wa nchi za kiafrika na kujenga mshikamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakuu wa Nchi za Umoja za Afrika walikubali ombi hilo na kuagiza kuwa mzunguko wa Uenyekiti urekebishwe na Kanda ya Mashariki ipewe nafasi hiyo mwaka 2008. Aidha, Wakuu wa *AU* waliamua kuwa Kanda ya Mashariki yenyewe impendekeze Mwenyekiti wa Kikao cha Kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uamuzi huo Wakuu wa Nchi za Kanda ya Mashariki mwa Afrika walikubaliana kwa kauli moja kumwomba Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kukubali kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika kwa mwaka 2008. Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete alikubali ombi hilo. Hatimaye Viongozi wa Nchi za Kanda ya Mashariki walifikisha uamuzi wao mbele ya Viongozi wengine wa Afrika ambao nao kwa kauli moja waliafiki pendekezo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uchaguzi huu, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete aliendesha shughuli za Kikao cha Kumi cha Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika kilichomalizika tarehe 2 Februari, 2008 kwa ufanisi mkubwa. Ataendelea kuongoza shughuli za Umoja huo hadi kikao cha 12 cha Wakuu wa Umoja wa Afrika kinachotarajiwa kufanyika Januari, 2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa kuipokea taarifa hii ya heshima kubwa aliyopewa kiongozi wa nchi yetu na kumpa Mheshimiwa Rais msaada ili kumwezesha kutekeleza majukumu mazito yanayomkabili kama kiongozi wa Bara la Afrika kwa ufanisi. Aidha, wananchi wote wanaomba kumuunga mkono Mheshimiwa Rais, katika shughuli hizi kwa sababu heshima hii pia ni kwa nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nina heshima kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Azimio lifuatalo:-

Azimio la Bunge la kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi za Afrika.

KWA KUWA nchi yetu inaongozwa kwa misingi ya kidemokrasia yenye kufuata uongozi bora, unaodumisha amani, umoja na mshikamano miongoni mwa wananchi na nchi jirani;

NA KWA KUWA Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi za Afrika alikuwa apatikane kutoka miongoni mwa nchi wanachama Kanda ya Mashariki;

NA KWA KUWA nchi wanachama wa Umoja huu waliona ni vema nafasi hiyo sasa ikiongozwa na Watanzania na hivyo wakaridhia kumchagua Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete;

NA KWA KUWA nchi wanachama wana imani kubwa na Mwenyekiti Mpya katika kutafuta utatuzi wa matatizo mbalimbali yanayolikumba Bara letu la Afrika kama migogoro ya kisiasa, njaa na umaskini;

NA KWA KUWA Mwenyekiti Mpya ameikubali nafasi hiyo na kuahidi kushirikiana na viongozi wa nchi wanachama kwa kuweka mahusiano mema ya kisiasa na kiuchumi na kujenga Afrika mpya yenye kudumisha upendo, amani na mshikamano baina ya wananchi na viongozi wake;

KWA HIYO BASI Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lililoanza tarehe 29 Januari, 2008 na linaloendelea na Mkutano wake wa Kumi hapa Dodoma linapokea na kukubali pendekezo la kutoa pongezi maalumu kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti Mpya wa Umoja wa Nchi za Afrika na pia Bunge hili linaahidi kumpa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza majukumu hayo makubwa aliyokabidhiwa na viongozi wa Afrika katika kipindi hiki cha uongozi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa kuliunga mkono Azimio hili na kuomba Wabunge wenzangu wote tuliunge mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijalichangia hili Azimio ningeomba nitoe mfano mmoja wa tendo ambalo lilinitokea mimi mwenyewe. Siku moja nilikuwa katika ibada ya hijja, Maka, nikamwambia Sheikh mmoja mbona wale viongozi kule wanakaa peke yao wanawaacha wafuasi wengine huku peke yao? Yule Sheikh akaniambia hiki kidole kimoja unawaonyesha wale lakini vitatu vinakutizama wewe, kwa hiyo, jibu maswali yako kwanza kabla ya kuwanyoshea wengine. Katika Bara la Afrika hakuna hata kiongozi mmoja wa kisiasa aliyewahi kukubali katika nchi yake kwamba ana matatizo ya kisiasa. Ukimuuliza atakwambia ana matatizo ya uhalifu, uchumi na kadhalika. Ni Rais Jakaya Mrisho Kikwete aliyekuja katika Bunge hili akakubali kwamba yeye mwenyewe analo tatizo la kisiasa na atalikabili, atalitatua. Nasema huo ni mfano peke yake. Kwa sababu hiyo tuna kila sababu Watanzania kumpongeza kwa kuwa na kiongozi ambaye anakubali yeye mwenye mapungufu kwanza kuunga mkono kwamba yeye ni kiongozi anayeweza kutatua matatizo ya wenzake. (*Makofi*)

Maana usipokubali wewe mwenyewe mapungufu yako basi huwezi ukatatua matatizo ya mwingine. Kwa hilo kwanza nasema tumpongeze Rais wetu kwa kuwa shujaa wa kukubali matatizo yetu tuliyonayo na kwamba na yeye yuko tayari kusaidia wenzake kuweza kuyatatua matatizo waliyonayo. Nasema hilo ni jambo la heshima kwa

Rais wetu na ni vizuri tukampongeza kwa kitendo hiki. Lakini Azimio hili liendane na vitendo kama alivyosema Rais juzi Pemba, tunahitaji kuangalia viashiria ambavyo vitavunja umoja wa Taifa letu, mshikamano wa taifa letu. Na viashiria hivyo alianza kuvitaja, baadhi yake moja, kama ufisadi alisema kwamba vinaweza kuashiria kabisa uvunjaji wa amani ya nchi yetu. Lakini hakuishia hapo Mheshimiwa Rais akasema atashirikiana mwaka huu ni mwaka wa kushiriana na kufanya kazi na vyama vya upinzani. Nasema katika Bara la Afrika mambo haya huyakuti, unayakuta Tanzania peke yake na kwa sababu ya kiongozi tuliyenaye nawaomba ndugu zetu wenye migogoro waje wajifunze kwa Rais Kikwete, wajifunze Tanzania. (*Makofi*)

Sasa sisi Wabunge na wananchi kwa ujumla tunahitaji kuungana na Rais wetu maana yeye peke yake hawezi kufanya lolote bila ushirikiano wetu, tushirikane naye katika yale ambayo ni viashirio vya kuvunjika kwa umoja wetu, ni viashirio vya kumpunguzia yeye nguvu asiweze kushughulikia matatizo ya wenzetu. Pale ambapo tunaona kuna taasisi au asasi yoyote haiwatendei haki Watanzania ni wajibu wetu tusimame kidete pamoja kumsaidia Rais wetu ili haki itendeke na raia wapate haki zao. Pale ambapo tunabaini kabisa kuna huduma ambazo hazipatikana kwa raia wetu kinyume na matakwa na utashi wa Rais wetu ni vizuri tusimame kidete kumsaidia na kufanya kazi naye pamoja. Kwa ajili hiyo tuna kila sababu. Mwaka huu tumepata JK namba *two.* Tulikuwa na JK namba *one senior* alikuwa Mwenyekiti wa *OAU.* JK mwingine amepata kuwa Mwenyekiti wa *AU*, wa kwanza *OAU* sasa *AU* ni heshima kubwa kwa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bara letu la Afrika lina migogoro mingi. Jana ndugu zetu wa Kenya walikuja kwa Rais wakimwomba tena asaidie matatizo yao waliyonayo, sio kazi rahisi, ni kazi kubwa na yeye alipoupokea umoja huu alisema kwamba anaona si matatizo tu ya magomvi ya kisiasa lakini matatizo makubwa zaidi ya kiuchumi na kijamii. Na yote anataka kuyashughulikia lakini bila kutatua matatizo ya kisiasa maendeleo ya kiuchumi nayo yana matatizo. Tumeshuhudia Kenya inavyoporomoka kiuchumi kwa sababu ya matatizo ya kisiasa yaliyomo. Tujitahidi sisi Watanzania tuhakikishe nchi yetu inabaki kuwa ya amani tufanye kazi pamoja tuaminiane tusiwe na chuki baina yetu na kama alivyosema Rais tushirikiane katika ku-*promote democracy* katika nchi yetu. Naamini tutashirikiana na Rais, pale ambapo kuna matatizo hatujayamaliza basi yamalizike bila ya matatizo yoyote ili tumsaidie Rais wetu aende kifua mbele katika kupigania maendeleo na ufumbuzi wa matatizo ya Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na wewe pamoja na Wabunge wenzangu kukitakia Chama cha Mapinduzi *Happy Birthday*, leo tarehe 5. Nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuunga mkono kwa dhati hoja hii iliyotolewa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge inayoshughulikia mambo ya nje katika kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwake kwa kipindi cha mwaka mmoja kuwa Mwenyekiti wa nchi za Umoja wa Afrika. Hoja hii ambayo imewasilishwa kwa umahiri na utaalamu wa hali ya juu na Mheshimiwa Azan Zungu kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje na

kuungwa mkono na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, naiunga mkono asilimia mia kwa mia. Kwa bahati nzuri mimi ni miongoni mwa Wabunge wa zamani ambaye nilibahatika kufanya kazi na Mheshimiwa Rais, wakiwemo wewe mwenyewe, akiwemo Mheshimiwa Jackson Makweta, na Chrisant Mzindakaya. Nakiri mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa nimewahi kufanya kazi na Mheshimiwa Rais katika Chama cha Mapinduzi na Serikali kwa takribani miaka 30. Mimi namfahamu vizuri tangu alipojiunga na utumishi wa chama mwaka 1975 wakati nikiwa Katibu Msaidizi wa Chama cha TANU. Wakati huo Idara ya elimu ya siasa makao makuu ya TANU na baadaye nikafanye kazi naye katika Serikali ya awamu ya kwanza, pili na ya tatu kama Waziri mwenzangu. Hivyo kwa kuwa namfahamu, ninayosema ni ya uhakika na ya ukweli kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipaji cha uongozi wa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kilianzia tangu akiwa shuleni na hasa alipokuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, mwaka 1973-74. Aliwahi kuwa mwanaharakati mkubwa na akawa Makamu wa Rais wa Serikali ya wanafunzi katika Chuo hicho. Na katika kipindi chote hicho mimi ninavyofahamu alisimamia kidete na kutetea sana harakati za ukombozi katika Bara hili la Afrika na alipata nafasi ya kuzunguka Afrika nzima na duniani akitetea haki hasa kwa vijana. (*Makofi*)

Uwezo na uzoefu wa uongozi wake akiwa katika Baraza la Mawaziri, mimi binafsi nalisema kwa wazi nilivutiwa na kufaidika sana na uongozi wake na hasa alipokuwa akitetea hoja katika Wizara zake alizokuwa amekabidhiwa na Mheshimiwa Rais. Nikitoa mifano michache, akiwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini wakati huo alianzisha utaratibu wa kutoa leseni ya kununua madini na kuisaidia Serikali kuokoa fedha nyingi zilizokuwa zikipotea bure kwa watu waliokuwa wakiendelea na magendo katika nchi hii. Alipohamia Wizara ya Fedha alifanya kazi nzuri sana ya kurejesha uhusiano wa wafadhili na wahisani ambao walikuwa wamesusa kuisaidia Tanzania. Lakini kutokana na diplomasia yake aliirejesha nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali na wakati huo huo akapelekea kupendekeza kuzaliwa kwa wazo la kuundwa kwa *TRA* (*Tanzania Revenue Authority*), mamlaka ya mapato ambao wote ni mashahidi, imetufanyia kazi nzuri sana hata hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunaelewa jinsi Rais Kikwete wakati akiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa alivyolivalia njunga suala la kutetea amani katika eneo la maziwa makuu hususan Burundi na Kongo *DRC* na hatimaye katika majadiliano ya kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa msingi huo, nina imani kabisa kuwa kazi kubwa na kwanza iliyo mbele yake itakuwa ni kupatanisha nchi za Afrika kuondokana na mizozo mbalimbali na hasa majirani zetu wa Kenya, kazi ambayo tuna uhakika ataimudu vizuri sana. Huyu ni kiongozi mpenda amani, utulivu na maisha bora kwa wananchi wake na hasa Bara lote la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huu, ninaomba nitumie nafasi hii, kuwapongeza sana viongozi wa nchi za Umoja wa Afrika kwa kauli moja kumchagua Rais wetu katika kipindi hiki kigumu cha machafuko katika Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wao huo, ni imani kubwa walinayo juu ya Rais wetu. Sote tunaelewa kuwa Rais peke yake bila Bunge na wananchi kumuunga mkono, hawezi kufanikiwa katika azma yake hiyo. Kwa kuwa yeye ni sehemu yetu, hatuna budi kuendelea kumuunga mkono kwa kauli na matendo yetu ili Watanzania tuendelee kusifika kama kisiwa cha amani na utulivu katika Dunia hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninadiriki kusema kuwa chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais wetu, kama kweli tutafuatilia kwa makini nia na madhumuni ya maagizo yake ya mara kwa mara kwa watumishi na wananchi na kwa kweli tukitekeleza kwa vitendo yale yote yaliyomo katika maagizo anayoyatoa, tutaweza kufikia hatua nzuri sana ya maendeleo ya watu wetu. Tatizo bado lipo kwa baadhi ya viongozi ambao bado hutoa viapo kwa kushika vitabu vitakatifu lakini wakiwa na mikono michafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni sawa na Wakristo wanaojidai wameokoka lakini wanatenda uchafu mtupu. Lakini wenzetu Waislam mtakubaliana na mimi kwamba mtu anapoenda msikitini bila kutawaza, ni kosa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini tukisaidiana wote kwa pamoja huwezi kushindwa lazima tuendeleze imani chini ya Rais wetu ili tutekeleze azma ya Serikali ya Awamu ya Nne ya kuendeleza dola kwa misingi ya utawala bora, uwajibikaji ili wanaovuruga wawajibike na kuwajibishwa bila kuwaonea aibu. Lazima tuzingatie pia agizo la utawala wa Sheria unaoheshimu na kulinda haki za binadamu na kuendelea kupambana na vita dhidi ya rushwa, ufisadi bila uoga wala kuonea mtu yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiweza kuyatekeleza hayo, nina imani kwamba maisha ya watu wetu mahali popote walipo yatakuwa mazuri na heshima ya Tanzania itaendelea kutukuka ndani na nje ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sipendi kurudia yale maneno yaliyosemwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje na maelezo ya ufasaha aliyotoa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Msemaji wa Kambi ya Upinzani ambaye kwa bahati nzuri niliwahi kufanya kazi pamoja naye, naye amefanya kazi na Rais wetu. Mimi nina imani kabisa ameyasema hayo kwa nia nzuri na nina imani kwa kushirikiana na pande zote, tutaweza kufanikiwa kuleta maendeleo ya watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa msingi huo, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wote kwa kauli moja, tuunge mkono hoja hii muhimu kwa heshima ya Rais wa Tanzania na Afrika kwa ujumla na tusikubali wenye nia ya kutuvuruga waendelee kuturudisha nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa moyo wangu wote, ninamuomba Mwenyezi Mungu ambariki Rais wetu, Jakaya Mrisho Kikwete na kumuongoza katika kila kazi anayoifanya ili aweze kutekeleza mapenzi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wabunge, ni kwa msingi huo basi, ninawashukuru kwa kunipa heshima hii lakini pia tuendelee kumuombea Rais wetu ili afanikiwe katika kazi nzito iliyo mbele yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa heshima na tahadhima, ninaomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuunga mkono hoja ambayo iko mbele yetu ambayo inatoa pongezi sana kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 62 (1) cha Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inataja uwepo wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini inataja Mheshimiwa Rais kama sehemu ya Bunge tukiwemo na sisi Wabunge wa Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo basi, heshima aliyopewa Mheshimiwa Rais wetu kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, si tu kwamba ni heshima yake yeye lakini pia Bunge letu limepata heshima kubwa sana katika Bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini heshima hiyo pia inahama kutoka kwetu sisi Wabunge na kwa kuwa sisi ni wawakilishi wa wananchi wa nchi hii ya Tanzania na kwenda kwa wananchi wa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, historia ya Bara letu la Afrika, inatuonyesha wazi kwamba Bara letu la Afrika katika miaka mingi limekuwa na historia ya kuwa na umoja. Haya yanajidhihirisha kabisa katika mifumo mbalimbali ya uongozi wa Bara letu la Afrika na namna tulivyopata Uhuru lakini hata lugha zetu ndani ya Bara la Afrika ziliashiria toka mwanzo kwamba Waafrika wote ni wamoja kwa kila namna.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata maendeleo ya Bara letu la Afrika, yanaonyesha kabisa kwamba yalienda kwa kasi sana kabla ya Uhuru. Katika karne ya 12, tunaona kabisa hata dhana hizi za teknolojia mbalimbali zilianza katika Bara letu la Afrika. Mfano dhana ya umwagiliaji maji tunakumbuka ilianza katika Mto Nile katika Bara la Afrika, teknolojia ya maandishi na hesabu za kalenda zilianza katika Bara letu la Afrika. Hivyo tuna kila sababu ya kuona uteuzi na uchaguliwaji huu wa Rais wetu, kwa kweli unataka kupandisha sauti yetu Waafrika kutokea katika nchi yetu ya Tanzania na kudhihirisha kwamba sasa tumedhamiria kwenda mbele na kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha kuingia kwa ukoloni ndicho kilichotugawa Waafrika lakini leo basi nchi nyingi za Afrika baada ya kupata Uhuru kwa miaka mingi tunashuhudia nchi yetu ya Tanzania kupitia Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, anapewa kazi na dhamana kubwa ya kuanza kusimamia maendeleo ya Waafrika wote na kutufanya tuwe kitu kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni heshima kubwa sana kwa nchi yetu kama nilivyosema ni kwa sababu nchi yetu imekuwa na historia kubwa ndani ya Bara la Afrika lakini na ulimwengu mzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu yanayomkabilia Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ndani ya nchi yake ya Tanzania lakini kama Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika yana changamoto kubwa. Nisingependa kurudia yale yaliyosemwa na wenzangu lakini nisisitize kwamba tumeona ni kwa kiasi kikubwa sana Mheshimiwa Rais wetu amekuwa na changamoto ndani ya nchi yake lakini sasa changamoto hizo ni lazima ashughulike nayo katika Bara zima la Afrika ili kuhakikisha kwamba nchi yetu pamoja na nchi nyingine za Afrika zinapambana na tatizo kubwa la kukuza uchumi na pia kuondokana na umaskini uliokithiri katika nchi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete imefanya mambo mengi katika kupambana na masuala haya lakini sasa changamoto hiyo inatakiwa ihamishwe na ipelekwe katika Umoja wetu wa Bara la Afrika. Lakini wenzangu wamesema masuala ya migogoro ya kisiasa na mingine mingi imekuwa bado inaturudisha nyuma lakini pia Bara letu bado linakabiliwa na magonjwa kama ugonjwa wa UKIMWI na vile vile njaa, uharibifu wa mazingira na majanga mengine mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu, wakati wa hotuba yake ya kukubali kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, amesema kwamba bado tuna changamoto ya kuboresha miundombinu katika Bara letu la Afrika tukianzia katika nchi yetu ya Tanzania ili kuonyesha ni namna gani tunamuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya na mengine yote yanatuhitaji sisi Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuanze kwa kumuunga mkono leo lakini tuonyeshe kwa matendo kumuunga mkono Mheshimiwa Rais katika kusimamia vizuri mipango ya Serikali yetu ndani na vile vile tutampa nguvu yeye kutumia mifano hii kutoka ndani ya nchi yetu kuipeleka kule katika Bara la Afrika na hivyo basi nafasi yake ya Uenyekiti atachukua hatua ambayo italeta heshima kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo, Waafrika wote ni wamoja si tu kwa kufanana kwetu kwa rangi au kwa namna tunavyoishi lakini historia ya machungu tuliyoyapata katika nchi zetu katika kupigania Uhuru na kupambana na mifumo mingi ya kiulimwengu ambayo imekuwa kwa namna moja au nyingine inaturudisha nyuma katika harakati zetu za kutuletea maendeleo ya kiuchumi, kijamii na hata ya kiutamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakiri na kusema, viongozi waliokubali kwa pamoja na kumchagua Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, hawakufanya makosa, walipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu ni shujaa, Rais wetu ni jasiri, Rais wetu ana moyo wa kuthubutu, tunaamini kwa kutumia sifa hizo alizonazo ataweza kufanikiwa katika nafasi hiyo aliyoipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa furaha kubwa, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kuchaguliwa kwake lakini vile vile ninaomba nimtakie baraka nyingi na baraka za Mwenyezi Mungu ziwe pamoja naye katika majukumu hayo mazito yakiwemo ya ndani ya nchi yetu na hayo aliyokabidhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile, ninaomba niseme kwamba nchi yetu nayo sasa iamue kwa dhati kabisa kubeba jukumu hili la Uenyekiti wake kuwa ni jukumu la Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme ninaunga mkono Azimio hilo kwa asilimia mia moja na ninaomba Bunge lako liunge mkono Azimio hilo na hivyo basi kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kuteuliwa na kuchaguliwa kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kueleza nini kilitokea huko.

Lakini kabla ya hapo, nimshukuru sana Mheshimiwa Spika wetu kwa kuniteua kwenda kwenye mkutano huu, kwa kweli nilijisikia vizuri na ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kifupi nitaeleza nini kilitokea huko. Tarehe 26, ujumbe wa Tanzania ukiongozwa na Waziri wetu, Mheshimiwa Bernard Membe, tulielekea Addis Ababa na kule tulifika jioni. Tulipofika tu Uwanja wa Ndege, viongozi wengi sana walikuja kumwona pale pale Mheshimiwa Bernard Membe na kumwambia bwana sisi kwa heshima na taadhima, tunaomba Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, agombee Uenyekiti wa Umoja wa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania waliokuja kutupokea, vile vile walitupa ujumbe huo na sisi tukaanza kushangaa kumbe tunaelekea kwenye mambo makubwa huko Addis Ababa. Wengi walisema kwamba sasa hivi Afrika ina matatizo makubwa lakini kufuatana na tunavyomfahamu Mheshimiwa Rais, ana uzoefu mkubwa wa kutatua migogoro katika Bara la Afrika wakati akiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na wakati akiwa Rais, sasa ni wakati muafaka kwa sisi viongozi wa Afrika. Tunaomba mfikishe ujumbe huu ili atakapofika agombee hiki kiti.

Sasa tarehe 27, tulipoingia pale kwenye ukumbi wa mkutano wa *AU*, tulishangaa, nchi moja ambayo ilikuwa inataka kugombea kiti hicho ikimjia Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa kwetu, Mheshimiwa Bernard Membe na ujumbe wao kusema jamani sisi tunainua mikono na tunaachia kiti hiki kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete. Kwa hiyo, ile nchi ikajitoa kabisa kukabakia nchi moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 28 ile nchi iliyokuwa imebakia kwa kutotegemea, wakamwita Mheshimiwa Bernard Membe, akatuomba tena sisi ujumbe wa Tanzania kuungana naye na kuwasikiliza. Wenyewe wakasema jamani sisi kwa sasa tunajitoa, tunamwachia Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, aweze kugombea kiti hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tarehe 29/1/2008, tulivyompokea Mheshimiwa Rais, ujumbe Mheshimiwa Bernard Membe aliompa ni kwamba viongozi wote Mheshimiwa Rais wetu wanaomba ugombee hiki kiti. Mheshimiwa Rais alipokea huo ujumbe akasema basi mimi nitaona tarehe 30 asubuhi kesho nini kitatokea. Tulipofika kwenye ukumbi ule mimi nilikuwepo pale, viongozi wengi walikuja wanasema usikatae ni wakati wako chukua kiti hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi ile muda sio mrefu kulikuwa na *cross session* na haikuchukua *round* ameingia kule, Mwenyekiti aliyekuwepo akamwambia Mheshimiwa Rais tunakuomba uchukue kiti hiki na Mheshimiwa Rais hakusita, akachukua kiti hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuliokuwepo tulifurahi sana kwa heshima Rais wetu aliyopewa lakini pia heshima nchi yetu iliyopewa na kwa kweli tulijisikia vizuri mpaka wengine tulikuwa tunashindwa hata la kusema, kwa kweli Mungu ametubariki sana Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo ambayo mimi na wenzangu tuliyashuhudia, ninapenda sasa kuunga mkono Azimio la Bunge na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa heshima kubwa ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mchango mkubwa Tanzania ilioutoa wakati wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika kulikomboa Bara la Afrika kutoka kwa wakoloni sasa tena historia ya Tanzania imejirudia kwa Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika ili Tanzania tena iweze kusaidia katika kutatua migogoro ya vita vya wenyewe kwa wenyewe vinavyoendelea hivi sasa katika baadhi ya Nchi za Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nasema Mungu ambariki Rais wetu, Mungu aibariki Tanzania, Mungu aibariki Afrika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda na mimi nichukue nafasi hii kwanza niseme ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuunga mkono hoja hii, ninapenda Waheshimiwa Wabunge wote tuelewe kwamba sasa Rais wetu tunampeleka kwenye hali ya juu na kwamba haya matatizo ya ndani ya Tanzania tuyashughulikie sisi wenyewe yeye ashughulikie mambo ya Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda niseme neno moja tu rahisi kwamba upinzani katika Afrika uko wa aina mbili. Uko upinzani ambao ni *constructive* na uko upinzani ambao ni *destructive*. Sasa kuna upinzani ambao ni kama mtoto umembeba, mtoto ukimbeba abebeke lakini mtoto mama umembeba mgongoni kaweka miguu hivi, huyu mtoto ataanguka tu. Sasa kwa siasa yetu ya ndani, *I hope* watoto tutakaokuwa tunawabeba, watabebeka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninapenda niende kwenye suala zima la heshima ya Tanzania katika Bara la Afrika. Ni kweli kabisa kwamba kwa Tanzania kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *African Union* na hasa Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, amepewa kazi ngumu na kwa hiyo tumpongeze kwa kuchaguliwa kwake. Amechaguliwa wakati Bara la Afrika likiwa na matatizo mengi, matatizo ya jirani zetu wa Kenya, matatizo ya muda mrefu sana ya jirani zetu Rwanda na Burundi, matatizo ya Congo, matatizo ya Chad na kadhalika na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika hali ya namna hiyo lazima sisi Watanzania tumuombee Rais wetu, tumsaidie Rais wetu katika kupambana na kutatua matatizo yaliyopo katika Bara la Afrika. Mimi sitaona tena Watanzania wengine wakianza kusema kuwa Rais wetu anasafiri sana, haya ni matatizo makubwa yatahitaji asafiri sehemu nyingi sana na hali kadhalika kwa kubeba mzigo huu ni lazima Watanzania tutabeba kwa kiasi fulani kwa sababu kutakuwa na matumizi ya baadhi ya mambo haya ambayo yatabidi yabebwe na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo nakuja kwenye sifa ya Tanzania katika suala zima la *non alignment*. Ndugu zangu, ninapenda niwahakikishie jambo moja ambalo limetupa Watanzania heshima kubwa sana ni wakati wa vita baridi kwa kutokufungamana na upande wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakumbuka Baba wa Taifa, tarehe 14 Desemba, 1961, wakati Tanzania ikifanywa kuwa Mwanachama wa Umoja wa Mataifa, alitoa hotuba yake na ninapenda ninukuu baadhi ya maneno hayo aliyoyasema kwa Kiingereza anasema:-

*"We from Tanganyika have come to the United Nations with an open heart. Those who will expect us to run in the corridors of the United Nations either to join those who are East or West; they will waste their time because Tanzania will be neither. We will judge all the issues which came before us on their merit and not because they are supported by a certain big power" (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hivyo tu, Tanzania katika suala zima la ukombozi, Kamati ya Ukombozi ya Umoja wa Mataifa ilipoundwa mara ya kwanza Desemba mwaka 1962 ikiwa ni Kamati ya Nchi 17, Tanzania ilikuwa mojawapo ya hizo nchi 17 na baada ya hapo Tanzania ilikuwa ni nchi mojawapo ya *founder members* wa *OAU* ambao walienda kutia saini Addis Ababa kwa mara ya kwanza mwaka 1963 na katika *summit* ya kwanza ambayo ilifanyika Cairo mwaka 1964, Tanzania ilikuwa katika mstari wa mbele kujaribu kueleza Waafrika umuhimu wa sisi kuwa na chombo cha kusaidia Uhuru wa Bara la Afrika kwa zile nchi zilizokuwa bado ziko chini ya mkoloni, ndio *Liberation Committee* ikaundwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, mtakumbuka kwamba na wakati huo lazima tukubali kwamba *Liberation Committee* haikuwa rahisi mtu kukubali kuwa katika nchi yake. Nakumbuka majina yalipotajwa ya nchi nyingine, walikataa kwa sababu walijua kuwa na *Liberation Committee* katika nchi yako ni kutafuta ugomvi na Muingereza, kutafuta ugomvi na Mfaransa, kutafuta ugomvi na Muitaliano, kutafuta ugomvi na Mspanishi, kutafuta ugomvi na Mreno lakini Tanzania tukasema, *came what may*, sisi tutakuwa na *Liberation Committee*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi sana mtu ukipata *platform* kama hii, ni rahisi kuanza kusema maneno mengi lakini kilichoniacha nisimame ni kuunga mkono hoja ya kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu. Kwa moyo wa dhati kabisa, ninaomba Bunge hili, wote kwa pamoja, tumpongeze Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa *AU.* Tumuombee kwa Mwenyezi Mungu ampe nguvu zote na uwezo wote na ampe hekima yote na baada ya hapo sisi wote kwa pamoja yale yote yatakayowezekana, tumsaidie Rais wetu kufaulu. Kila mmoja wetu awe tayari kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kusema ninaunga mkono hoja iliyoletwa mbele yetu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja ameleta hoja yake kwa maandishi anasema msisahau pia Mheshimiwa Rais amekuwa mtetezi wa haki za wanawake katika nchi yetu. Mheshimiwa mtoa hoja, Mheshimiwa Mussa Zungu. (*Makofi*)

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kwanza kuwashukuru na kuwatambua Wabunge wote waliochangia katika hoja hii nikianza na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha na Mheshimiwa mzee wetu, Mheshimiwa John Malecela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nichukue nafasi hii, kwanza kuwashukuru Wabunge wote waliounga mkono hoja hii. Kwa pamoja imeonyesha *spirit* ya nchi yetu na hasa *spirit* ya nchi yetu kuanzia katika Bunge letu, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua wachangiaji wengi walitaka kuchangia lakini wote tulikuwa tunaenda na *spirit* moja ya kuunga mkono na kushukuru namna Rais wetu alivyochaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *AU*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mzee John Malecela, amezungumza jambo la muhimu sana kwamba wakati Mheshimiwa Rais wetu atakapokuwa anajadili migogoro akiwa nje ya nchi yetu, sisi tumsaidie kuendesha nchi yetu kuleta amani, utulivu na kujenga Taifa letu kwenye misingi ile ambayo tumekubaliana nayo.

Ninamshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kwa namna alivyotoa sifa nzuri ya Rais wetu, kwa namna Rais wetu alivyoweza kutambua umuhimu wa kukaa na Upinzani ili kujenga Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Paul Kimiti kwa namna alivyoelezea alivyomjua Rais wetu toka hapo zamani kwa upendo wake na upenzi wake wa Taifa letu.

Ninamshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa hayo yote aliyosema. Pia nimshukuru Mheshimiwa Dr. James Wanyancha ambaye alipata bahati ya kwenda Addis Ababa na kushuhudia na kuiwakilisha Kamati yetu katika kupiga debe na nini, hakika maneno yake na umbile lake lililokuwa pale limefanya nchi zingine kuondoka na kumwacha Rais agombee peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Afrika ni Bara tajiri lakini migogoro tunayoletewa na watu wa nje ni kwa makusudi ili tubakie kuwa maskini. Tushirikiane, tuache migogoro ya tamaa, tuache migogoro ya upendeleo ili tuweze kujenga Bara letu ili liweze kupata sifa katika Mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mataifa ya nje yanaitambua Afrika kama ni sehemu ya migogoro na wanatujua sisi kwa migogoro na si kwa mazuri ambayo tunayo, mazuri ambayo tunayo wanakuja kutuibia na kutunyonya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa Norway, nilisoma gazeti moja ambalo lisema kwamba "*Africa is a passive recipient of aid and not an agent of his own development*". Kwa maana ya kwamba sisi ni watu wa kupokea tu misaada lakini hatuna changamoto ya kwenda mbele kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu akiwa Mwenyekiti, ataanza sasa kutatua migogoro na kuimaliza ili Afrika iwe katika picha ya ulimwengu kwani ni Bara ambalo linajiweza na *Africa can deliver*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana wote waliochangia na wote waliounga mkono Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Azimio la Kumpongeza Rais lilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Kwa hiyo, Azimio la kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa bila kupingwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa nchi za Afrika, limepitishwa na Bunge hili. Ahsante sana na sasa tunaendelea na shughuli nyingine.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Utalii wa Mwaka 2007
### (*The Tourism Bill, 2007*)

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika orodha yangu ambayo imefungwa ninayo majina yafuatayo:-

Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Samuel M. Chitalilo, Mheshimiwa Diana M. Chilolo na Mheshimiwa Castor R. Ligallama.

Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, karibu!

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nianze kwa kutoa pongezi kwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kuleta Muswada huu. Pia ninawashukuru Watendaji wote ambao kwa njia moja au nyingine wamechangia katika kukamilisha Muswada huu.

Nakubaliana kabisa na Waziri kwamba Sheria zile mbili yaani Sheria ya Hoteli na Sheria ya Wakala wa Utalii zilizotungwa tangu mwaka 1960, zimepitwa na wakati na haziwezi kutosheleza kuujenga utalii endelevu. Hivyo, nawashukuru kwa kuwasilisha Muswada huu na ninasema umekuja kwa wakati unaofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada huu, sehemu ya pili, Kifungu cha 6(1)(p) kinasema kwamba:-

*“The General functions of the division shall be:-*

*(p) To promote domestic tourism”*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa kuweka kipengele hiki kwani Tanzania yetu ina utajiri mkubwa sana lakini watu wengi hawajui vivutio vilivyopo Tanzania pamoja na kwamba wapo Tanzania. Wakati mwingine unakuta vivutio hivyo

viko kwenye maeneo yao lakini watu hawavitambui au hata kama wanavitambua basi hawavithamini au hawajui thamani yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana nyingine unakuta Watanzania tulio wengi hatufanyi utalii, tunafikiria kwamba utalii ni wa watu wa nje kama Wazungu lakini hii ni sababu ya umaskini na kutokuwa na elimu ya kutosha juu ya hivi vivutio. Utakuta watu wengi wanaokwenda kwenye utalii ni wale ambao labda wamealikwa kwenye semina au makongamano basi makongamano hayo ndio yanawagharamia wanakwenda kwenye utalii lakini ile tabia ya mtu ku-*save* ili mwisho wa mwaka badala ya kwenda kutembelea mahali fulani aende kwenye utalii bado haijajengeka kwa Watanzania walio wengi. Je, ni mikakati gani imewekwa ili kukuza utalii wa ndani? Kwenye Muswada huu sikuona kipengele chochote kinachoonyesha ni kwa jinsi gani hiyo *domestic tourism* inaweza kuendelezwa na kusimamiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Kifungu cha 56(1), kinachobainisha Kanuni mbalimbali ambazo Waziri atakuja kuziandaa pindi Sheria hii itakapokuwa imeshapitishwa hakuna *regulations* yoyote iliyoanishwa ambayo inahusiana na *domestic tourism*. Kwa hiyo, naishauri Serikali kuwa eneo hili litiliwe mkazo, watu waelimishwe juu ya vivutio vilivyopo na washawishiwe ili kusudi waweze kwenda kufanya utalii katika nchi yetu. Kwa kufanya hivyo, itaongeza kipato cha sehemu hizo na hivyo kuchangia kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 46(1)(2), yameainishwa makosa na adhabu mbalimbali. Ninapenda nieleweshwe kwamba je, hiyo faini ya shilingi milioni 10 ya waendesha utalii kama wakifanya makosa ni kwa waendesha utalii wote wadogo na wakubwa? Ninapendekeza kwamba wangeainisha maana kuna wale wanaoendesha hizi shughuli ambao ni wadogo sana, sina uhakika kama wanaweza kulipa hiyo faini ya shilingi milioni kumi. Kwa hiyo, napendekeza kwamba wangeainisha hiyo faini ya shilingi milioni kumi ni ya watu gani kama ni ya wote tujue, kama na wale wadogo watapata adhabu yao tujue.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya utalii bado ina fursa kubwa ya kuweza kuchangia zaidi katika pato la Taifa na kuondoa umaskini kwa Watanzania walio wengi. Naipongeza sana Wizara kwa kazi nzuri mliyokuwa mnaifanya ya kuendelea kuitangaza Tanzania na kuendelea kutangaza vivutio vilivyopo. Sasa hivi tunayaona matangazo yenu kwenye *TV*, tovuti, kwenye magazeti na majarida mbalimbali hata ya nje. Najua labda ndiyo maana ikawezekana hata nchi yetu ikawa ya pili kwa maeneo yaliyotangazwa kuwa na urithi wa dunia. Labda matangazo hayo mliyoyatoa ndiyo yamechangia mpaka Mlima Kilimanjaro na Serengeti vikawekwa kwenye vivutio 50 vya utalii kwa mwaka huu, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninachosema, sekta hii inaweza kuongeza sana pato la Taifa lakini tatizo lililopo ni kwamba mme-*concentrate* kwenye yale maeneo ya zamani, ili mradi kuna Mlima Kilimanjaro na Serengeti basi ni hukohuko. Ninashauri muangalie na Mikoa mingine kwa mfano Bagamoyo. Bagamoyo kuna utajiri mkubwa sana wa historia ya utumwa, historia ya dini ya Kiroma ilipoanzia au Makanisa ya

kwanza, hata kitanda kilichobeba maiti ya Livingstone kiko pale, kuna Kaole Ruins, kuna nyumba ambazo zimejengwa kwa sementi ya asili ambazo sasa hivi zinaachiwa zinaanguka tu lakini Bagamoyo hiyo hiyo tayari ina ina hoteli kubwa za kitalii. Ninapendekeza sasa badala ya kuangalia zile *traditional areas* zilizokuwa kwenye utalii tungefungua milango tukaangalia mikoa kama hiyo ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna mkoa wa Kagera. Mkoa wa Kagera unavyo vivutio vingi lakini kinachohitajika pale ni kuboresha miundombinu kidogo ili watalii wengi waweze kuja. Kuna *Game Reserve* ya Biharamulo, Buriji, Ibanda na hata Rumanyika. Maeneo haya yakitangazwa, yanaweza yakavutia watu wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokwenda kutembelea kwenye nchi za wenzetu, wanatupeleka kwenye maeneo yao ya utalii unakuta hakuna mambo makubwa ni mambo madogo lakini wameboresha miundombuni. Humo kwenye *Game Reserve* ya Rumanyika kuna mti mmoja ambao unasadikiwa kwamba ulimtibu Livingstone, watu wengi wangependa kuja kuuona.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kagera una Pori la Kimisi ambalo lina tembo wakubwa sana kuliko sehemu yoyote ya Tanzania. Mkoa wa Kagera katika Wilaya ya Karagwe kuna Mtagata ambazo ni chemchem za maji ya moto hata ukitaka kuchota na kupika chai hapohapo unaweza, nina uhakika wengi wangependa kwenda kuona. Katika Mkoa wa Kagera, kuna *historical sites* nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siyo hilo tu, utamaduni wa wakazi wa Mkoa wa Kagera ni mzuri sana na mnauelewa. Kuna ngoma mbalimbali, nyumba na jadi zetu, namna watu wanavyopika na kula na kadhalika, nina hakika hivi ni vivutio tosha vingeweza kuvuta watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Ziwa Victoria, wengi wangependa kuona Ziwa ambalo ni la pili kwa kubwa katika dunia lenye maji yasiyokuwa na chumvi. Kuna maporomoko ya Bugonzi na Rusumo.

Vilevile Mkoa umebahatika kuwa na msitu mmoja mkubwa sana unaoitwa Minziro katika Wilaya ya Misenyi ambao una aina ya mimea mingi na ambayo ni tofauti na mingine, haipatikani katika East Afrika, ni zaidi ya *species 100* na ina vipepeo wengi na wazuri sana lakini kwa sababu hatujatangaza vivutio hivyo basi watu wengi hawavutiwi kuja huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile kuna Nyakijoga ambayo iko Misenyi. Waumini wengi wa Dini ya Kikristo huwa wanakuja pale kuhiji kila mwaka. Sasa vitu kama hivyo vikitangazwa, nina hakika sekta hii itakua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao Mto Kagera ambao ni chanzo cha Mto Nile. Ikitangazwa hii, ikaeleweka kwamba chanzo cha Mto Nile kiko Mkoani Kagera, nina hakika watalii wengi watakuja.

Vilevile kuna hoteli za kitalii nyingi kama *Wogard Hotel, Copling Hotel, Yasira Talk* na kadhalika. Lakini siyo hilo tu bali Mkoa wa Kagera uko *strategically placed* kwa sababu unapakana na Kenya kupitia Ziwani, Uganda, Rwanda, Burundi na Congo. Kwa hiyo, miundombinu ikishaboreshwa, Mkoa ukafunguliwa, hivyo vivutio vikatangazwa, tunaweza tukawa tumeboresha sekta hiyo ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Waziri na Naibu wake kama inawezekana waje wautembelee Mkoa wa Kagera ili tuwaonyeshe vivutio hivyo. Muwalete wataalamu wenu ili waweze kuviorodhesha kwenye orodha ya vivutio vilivyo Tanzania ili kusudi na Mkoa wetu uweze kupata watalii wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naishauri Serikali iweke mikakati ya makusudi ya kuitambua Mikoa yote katika Tanzania ambayo ina vivutio yaani viorodheshwe kwenye orodha moja kusudi viweze kutangazwa na watalii wengi waweze kuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mtawaona Wenyeviti wa Kamati mahali popote, muwataarifu kwamba saa nane kuna Kikao cha Uongozi cha dharura na Serikali mnaarifiwa. Kikao hiki kinahusisha Wenyeviti au Makamu Wenyeviti.

Tunaendelea na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, karibu!

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na Serikali kwa ujumla kwa kuleta Muswada huu, bado hatujachelewa lakini inabidi tupige hatua za haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio mbalimbali yanayojitokeza Duniani, Tanzania haina budi kuchukua fursa hizo ili waweze kuwahi katika masuala mazima ya utalii na hatimaye kuweza kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichangie mambo machache tu ambayo yapo katika Muswada huu na ninataka nizungumze kwa ujumla. Kuna suala zima la kushirikisha wataalamu katika kuishauri Kamati katika masuala ya utalii. Kamati ya Ushauri ya Watalaamu ilibainisha mambo mengi katika utalii lakini kuna jambo moja ambalo nataka nilisisitize. Mheshimiwa Waziri hili naomba ulitazame kwa makini linaweza likatusababishia kuchelewesha maendeleo yetu hususani katika kukuza utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku hizi kuna msamiati, ni msamiati ambao unaeleweka na mimi sipingani nao lakini umefika mahali unaweza ukaturudisha nyuma

katika maendeleo yetu. Kuna kitu kinachojulikana kama *Environmental Impact Assessment*. Sina tatizo na msamiati huo au hatua zinazochukuliwa na wataalamu juu ya *Environmental Impact Assessment* lakini imefika mahali jambo hili la kufanya tathmini ya mazingira imeanza kuonekana inatucheleweshea maendeleo. Ni jambo zuri sawa lakini sasa hivi hakuna jambo lolote la maendeleo linaloweza likafanyika mpaka tupate taarifa ya *Environmental Impact Assessment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta tunazungumzia utalii, unahusisha wanyamapori na misitu na kila kitu, suala la *Environmental Impact Assessment* ni sahihi kabisa lakini imekuwa ni ucheleweshaji wa kuendeleza miradi hiyo kwa sababu ya kusubiri taarifa hizi na mtaalamu yule anaweza akakataa mradi ule usiende kwa sababu ya *report* yake ya *Environmental Impact Assessment* kwamba utaathiri hiki na hiki na hii nchi tunayo na hiyo sehemu iko miaka na miaka. Kwa mfano, tunataka kupitisha barabara ya lami katika Mbuga ya Wanyama, kunakuwa na *Environmental Impact Assessment*, kigezo kikubwa wanachokataa mradi huu usipite pale wanasema wanyama wetu watakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sababu za kufa wanyama wetu ziko nyingi, kuna wawindaji haramu hawa ndiyo wanamaliza wanyama kwa kiasi kikubwa sana. Kama ni *Environmental Impact Assessment*, hawatoi ufumbuzi wa kutosheleza kwa kusema kwamba ikipita barabara katika Hifadhi ya Taifa itaharibu mazingira, mazingira gani wakati barabara ile haipo katika kiwango cha lami na wakati barabara ipo? Suala ni kwamba gari haziendi kwa kasi na sasa tukitia lami gari zitakwenda kwa kasi lakini yapo mambo ambayo tunaweza tukazuia magari haya yasiende kwa kasi. Wao ni wataalamu, tukitengeneza barabara hatuharibu misitu, tukitengeneza barabara hatuharibu mazingira pale, kwa kiasi kikubwa ni eneo la barabara peke yake ambalo halizidi zaidi ya mita 20 kwa upana wake, ukichukua na *reserve* ya barabara. Sasa kwa sababu tu ya kugongwa mnyama, wananchi wa eneo lile wanakosa maendeleo ya haraka kwa sababu barabara ya lami imekatazwa na watalaamu wa *Environmental Impact Assessment* wanaotoa taarifa hiyo.

Mheshimiwa Waziri, katika masuala ya utalii, watalii wanapenda waende katika maeneo ya utalii kwa haraka na wengine wana wiki moja, wengine wana siku tatu, wanataka wapumzike siku mbili au tatu kama barabara ni mbovu hawaendi, tunakosa mapato kwa sababu wana hamu ya kwenda kwenye maeneo yale kwa sababu yanavutia lakini sasa hawaendi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna bahari na wanyama, huo ni mfano wa Saadani ninakupa. Sasa hivi wataalamu wamekwishatuambia barabara ya kutoka Tanga au kutoka Bagamoyo mpaka Horohoro ikifika maeneo ya Saadani wanataka waipindishe isipite katikati ya mbuga wakati barabara ya asili ndiyo inapita pale. Kwanza kwa kufanya hiyo barabara i-*divert* itaongeza kilomita 45 ya ziada, je, Serikali inazo pesa kwa ajili ya kuongeza hizo kilomita 45 za lami wakati hapa kuna upungufu huo? Barabara ilikuwa na kilomita 66 katika eneo hilo na sasa hivi itakuwa na kilomita 107.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu chukua mfano wa kilomita 45 gharama zake ni kiasi gani, hii ni kwa sababu ya *Environmental Impact Assessment*. Tunaweza tukafika mahali hiyo barabara isijengwe kabisa kwa kiwango cha lami kwa sababu Serikali itasema hatuna fedha za ziada za kuongeza hiyo *diversion* ya barabara. Unaona athari zake zinavyokuja hapo kwa sababu ya suala zima la *Environment Impact Assessment.* Kigezo cha *Environmental Impact Assessment* iwe ni *logic* kabisa lakini kwa sababu tu ya kugongwa mnyama, hiyo mimi napata wasiwasi, tunaweza tukaweka matuta hata mia 200 gari ipite pale kwa muda wa saa nzima na mnyama hagongwi, kwa nini hatuzungumzii hayo?

Mheshimiwa Waziri, Wizara yako itapata taabu katika utekelezaji wa kuvutia watalii ili wafike katika maeneo ya utalii kwa haraka na kuweza kurudi haraka katika maeneo yao ya kazi kwa sababu ya *report* ya *Environmental Impact Assessment* ambayo inaweza ikaturudisha nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka nizungumzie ni kuhusu madaraja ya hoteli, hili ni muhimu. Madaraja ya hoteli ni kigezo kimojawapo cha kuwapata watalii. Ni lazima tupate watalii wenye pesa watakaoingiza fedha hapa nchini, kuna wale watalii kama akina mimi tunaokwenda siku moja au mbili tunatafuta *Guest House* za kukaa, hao siyo watalii ambao tunawahitaji kwa kiasi kikubwa Tanzania, watalii wengi wana pesa zao wanakuja Tanzania ili waweze kutumia. Ni lazima wakae katika hoteli ambazo zina madaraja mazuri kuanzia *Three Star, Four Star au Five Star*. Tusisitize kwamba maeneo yale yenye mvuto mkubwa kwa watalii, tujenge hoteli zenye madaraja mazuri ili waje watalii wenye pesa na waweze kutumia pesa zao na hatimaye nchi yetu iweze kunufaika katika pesa hizo zinazokuja na hatimaye kuweza kukuza uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, hiyo pia itaweza kusaidia kuwanufaisha wale wananchi wanaozunguka maeneo ya utalii na vijiji vilivyoko jirani pamoja na Halmashauri husika ziweze kupata kipato kizuri kutokana na hoteli hizi ambazo zinalaza wageni ambao ni wa daraja la juu.

Sasa unajenga hoteli katika fukwe ya bahari ambayo ukuta wake ni makuti, paa lake ni makuti, sisi tunaita ni *full suit*, wanasema tu aaaah! Kwa sababu Wazungu wanapenda kuishi huko, mtu mwenye hela yake hawezi kuja kukaa huko, atakuja yule ambaye ana pesa kidogo. Tujenge hoteli ambazo zitavutia watu ambao wataweza kukaa pale na kuweza ku-*spend* pesa zao kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hayo mawili ambayo nilitaka kuchangia katika Muswada huu, Wizara ya Maliasili ijitahidi kuna vikwazo vingine vinaweza vikakwamisha maendeoeo ya utalii kwa sababu ya taarifa mbalimbali za kitaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa nitamwita Mheshimiwa Samuel M. Chitalilo.

**MHE. SAMUEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuweza kuwa mchangiaji kwa siku hii ya leo katika Muswada huu wa Sheria ya Utalii.

Nachukua nafasi hii vilevile kuipongeza Wizara na kumpongeza Waziri pamoja na Watendaji wake wote kwa kuandaa Muswada huu ambao umekuja wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema Tanzania maana yake ni nini? Tanzania maana yake ni mbuga hizo za Serengeti, Ngorongoro na hata Manyara ambapo kuna wanyama na ndege wazuri na kila kitu. Kwa hiyo, tunayo sababu ya kujivunia kwamba tunavyo vivutio vya watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Victoria pamoja na mambo mengine yote niliyoyataja, ni kivutio tosha kwa watalii kutoka nje kuja kuona Tanzania kuna nini. Kuna nchi nyingine hazina vitu hata kimojawapo kama hivi nilivyovitamka lakini sisi tunavyo. Nafikiri ni kuvitumia vizuri ili kuboresha uchumi wetu uweze kupanda zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nimefurahishwa sana na Muswada huu kuletwa wakati huu, lakini kuna mambo mawili au matatu hivi nataka kuyazungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mazuri yote hayo bado tunazidiwa sana na majirani zetu Kenya katika suala la kutangaza mambo yetu mazuri yaliyopo hapa Tanzania. Kenya walitumia nafasi hii na wanaendelea kutumia nafasi hii kutangaza vivutio vilivyopo Tanzania kwamba vipo ndani ya nchi yao au vipo Tanzania lakini ili kufika kwa urahisi pitia Kenya. Kwa hiyo, nasema kwamba huu ulikuwa ni uzembe wetu Tanzania kwa sababu kwa nini tusubiri Taifa lingine la jirani ndiyo lije litangaze, lipate mapato na sisi tupo tumelala?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hapa imeainisha yenyewe kwamba hali hiyo ilitokana na Sheria na Sera mbovu za Utalii tulizokuwa nazo, bado hatujavitangaza vivutio vyetu vingi ndani na nje ya nchi na pia hatuvitunzi vivutio vyetu ili vidumu. Vile vile amesema kwamba kuna uhaba wa hoteli, ujenzi holela wa hoteli, hatujasomesha Watanzania wengi kwenye fani za utalii na hoteli kutokana na uhaba wa vyuo vya kimataifa. Sasa kama sababu hizi tunazo basi tuziboreshe. Kama hivyo ndivyo vigezo ambavyo vinafanya tusipate pesa kwenye utalii basi tuboreshe vitu hivi ili utalii wetu uwe na maana kwa Tanzania kwa maana ya kukuza uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hawa *Tour Guides* ambao wanawasaidia watalii wetu kwenda sehemu mbalimbali ikiwemo mlima Kilimanjaro na sehemu nyingine ambazo huwezi kufika ukiwa mgeni, tusiwaachie wageni kabisa. Ninashukuru kwa sababu Muswada wenyewe unasema hivyo. Ninaomba tusiwaachie wageni wakaendelea kuendesha biashara hizi. Ninaomba biashara hii, leseni apewe Mtanzania au mzawa lakini awe na ubia wa kufanya biashara hiyo na huyo mgeni. Aidha kwa

sababu huyu mzawa atakuwa hana kipato cha kuweza kutosheleza huo mtaji basi tuwashirikishe wageni lakini ni lazima wafanye kazi pamoja na hawa wazawa wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote ni sawa na kusema kwamba Tanzania tuna sehemu kubwa tu ya utalii hata Buchosa kule Jimboni kwangu kuna sehemu nyingi tu za utalii kwa mfano kuna visiwa zaidi ya 10 kimojawapo ni Maisome. Kuna mawe mazuri ambayo unaweza ukaweka ndani ikawa kama vigae, nayo ni sehemu ya utalii. Kuna kisiwa cha Kome unaweza ukaona miti mizuri na hata baadhi ya wanyama wadogowadogo. Kuna visiwa vingi vya uvuvi kama Ziragura, nayo inaweza kuwa ni sehemu ya utalii. Kwa hiyo, tuna sehemu nyingi tu za utalii siyo Serengeti peke yake wala Ngorongoro. Tuna Kisiwa cha Iyozo, Chamagati, Chembaya na Nyamangu. Katika visiwa hivi vyote, visiwa vikubwa kupita vyote ni Maisome na Kome. Maisome ina Kata moja ambayo watu wanakaa kabisa na upande mwingine kuna wavuvi. Kwa hiyo, hizo ni sehemu tu ambazo zinaweza zikawa za utalii kwa sababu Maisome iko jirani kabisa na Hifadhi ya Rubondo ambapo Rubondo wanakwenda watalii. Kwa hiyo, hata Maisome watalii wanaweza wakaja. Kwa hiyo, tuna sehemu nyingi tu ambazo tunaweza tukazitengenezea njia zikatuboreshea pato letu la Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na haya yote, inapofika wakati wa kutafuta kura kwa wananchi, tunawajali sana wananchi wetu lakini mimi kwangu Buchosa tuna tatizo moja. Wizara inaposema ina sehemu ya Hifadhi sawa kuna Hifadhi mbili yaani kuna Kisiwa cha Maisome ambapo kuna sehemu ya hifadhi na sehemu moja ya Kisiwa cha Kome nako kuna kisiwa cha hifadhi kule Mchangani ambako kuna wavuvi lakini zaidi ya watu 1000, 2000, 3000 na hata 4000 wamekaa kwenye hizi sehemu za uvuvi ambazo ni ndani ya hifadhi, wako sehemu moja lakini hadi leo hawaruhusiwi kujenga nyumba za kudumu kama pale Mchangani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 22/1/2008, nilikuwa na mkutano maeneo yale, watu wanalalamika, wengine wamezaliwa pale, wamekuwa na umri hata wa miaka 40 na 50 lakini hadi leo hawaruhusiwi kujenga nyumba za kudumu kwamba wao pale ni watu wa muda tu na baadaye watafukuzwa. Kwa sababu hata ukiangalia msitu wenyewe unaodaiwa kwamba kuna hifadhi pale hakuna hata mti mmoja wa maana wala hakuna hata kitu chochote pale ambacho unaweza ukasema pale kuna hifadhi. Naomba Wizara hii ya Maliasili iangalie uwezekano wa watu hawa wa Mchangani kupewa ruhusa ya kujenga nyumba zao za kudumu. Mpaka leo hii tunavyozungumza, kila mara moto unatokea kwenye nyumba zao kwa sababu wametengeneza nyumba za miti na makaratasi haya ya *plastic* juu ya nyumba. Kwa hiyo, kila siku ni kubadilisha na kuuungua na wanapata matatizo.Watu hawa ni wapiga kura wetu wazuri sana na wapiga kura wangu wazuri. Kutokana na kwamba wengine wamezaliwa pale hawana mahali pengine pa kwenda na hiyo ni hifadhi na hawa wanasaidia kutunza ile hifadhi. Kwa hiyo naomba kabisa Mheshimiwa Waziri yeye na watendaji wake wanielewe na walifanyie kazi suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishajaribu kuzungumza hapa hata kwenye maswali kipindi kilichopita kwamba hata pale Maisome, wakati ule Serikali inagawa viwanja kwa watu ili waweze kuishi kwenye kile kisiwa, watu wale walikuwa wachache, sasa

wameshazaliana wamekuwa wengi. Kwa hiyo, watu wale wanalalamika kwamba wameshakuwa wengi lakini bado wanabanwa kwamba kuna hifadhi wakati hifadhi hiyo hakuna hata mti mmoja wa maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja niliomba hapa kupitia maswali kwamba watu hawa sasa wagawiwe eneo kubwa ili waweze kulima. Kwanza ni wazalishaji wazuri wa chakula. Kwa Mkoa wa Mwanza, Jimbo la Buchosa huwa na chakula kingi. Sasa naomba mambo haya yazingatiwe pamoja na kwamba kuna Sheria inayotaka wananchi wasiingie hovyo kwenye hifadhi lakini kuna mahali tunabanwa na watu wetu au wakazi wetu wa sehemu hizi na hawa ndiyo waliotuweka madarakani. Kwa hiyo, lazima tuwafikirie mapema zaidi. Pamoja na kwamba tunataka tuboreshe mambo ya utalii, tupate fedha nyingi lakini tufikirie sana watu hawa kwa sababu nao wana shida katika maeneo yao wanayokaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingeweza kuweka ubishi hapa kama tungekuta labda Mchangani kule kisiwa cha Kole kweli ni hifadhi, ina kitu ambacho kinaitwa hifadhi ya Taifa, lakini ukiangalia pale ni ardhi tu na hata miti yenyewe ukienda kuangalia hakuna mti wowote wa maana. Kwa hiyo, naomba Wizara iangalie mambo haya kwa mapana zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kipengele kimoja nimekiona hapa, watu wengi wanasema sehemu ya utumwa ni sehemu ya kwenda kuangalia kama sehemu ya utalii lakini kwa upande wangu nafikiri tungeiacha kama ni sehemu ya masikitiko kwa sababu kwanza ndugu zetu waliteswa, walinyanyaswa kwa kupitishwa hizo njia. Nafikiri ile sehemu isiitwe ya utalii, iitwe sehemu ya masikitiko kwa sababu babu zetu walinyanyaswa na waliwekwa minyonyoro. Kwa hiyo, nisingependa sehemu hii ikaitwa ya utalii kwa sababu tutakuwa kama tunaenzi watu wale kwa jinsi walivyowafanyia mababu zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, kwa sababu Rais Bush anakuja nchini kwetu, kwa sababu lile ni Taifa kubwa, naomba matangazo pamoja na kwamba yapo lakini yaendelezwe sana pale Arusha sasa na kwenye runinga yaonekane kila mara kuitangaza Tanzania ilivyo nzuri, kutangaza wanyama wetu walivyo wazuri, kutangaza na kujivunia kabisa kwamba tunazo mbuga. Tunapojivunia Tanzania, nafikiri tunajivunia pamoja na hizo *assets* zetu tulizonazo za mbuga. Kwa hiyo, tufanye matangazo kwa kina na kwa ndani zaidi ili hata mtu anapokuja anaona Tanzania sawa bado ipo nyuma kwa mambo mengine mengine hivi lakini Mungu nisaidie kwa miaka mingine ijayo itakuwa juu kwa sababu inavyo vitu vingi vya kusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sehemu moja nataka niizungumzie labda siku moja Waziri na timu yake kwa sababu ni mtandao mkubwa wa maliasili hata kule Nzega kuna mtandao wa maliasili. Namwomba Waziri, kuna sehemu moja inaitwa Matinji, kuna jiwe moja niliwahi kulitembelea miaka iliyopita, jiwe hilo ni refu, limeundwa kama treni hivi na huwezi kusema hili ni jiwe au ni nini, limetengezwa utafikiri kama lilitengenezwa kwa sementi kwa kulizunguka hivi, ni refu sana hilo jiwe, lakini hilo jiwe kuna muda

fulani linacheza, linatikisa ardhi yote sehemu hiyo. Kwa hiyo, tunazo sehemu nyingi, hatuwezi kuzitaja zote hapa na tukazimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote niliyoyatamka lakini kuna jambo hapa nataka kulizungumzia. Kuna Sheria fulani tulizipitia hapa Bungeni, Serikali ilipanga bei mpya ya uwindaji, ikazileta hapa Bungeni na tukazipitisha lakini hadi leo Wizara inasema Sheria hizi hazifanyi kazi, sasa tulipitisha kitu gani? Kwa hiyo, naomba vitu kama hivyo vifuatiliwe na tunapopitisha kitu hapa kifanye kazi vizuri kwani kupitisha Sheria hii ilikuwa ni kuongeza uchumi wetu wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mambo muhimu yote niliyozungumza yafuatiliwe hususani ya wananchi wangu wa Buchosa hasa lile la kuwaongezea ardhi kule Maisome wapate sehemu kubwa ya kuweza kulima kwa sababu hawana viwanda kule wala kitu chochote. Pia naomba watu hao wanaoishi Mchangani wakifanya shughuli ya uvuvi na wao wanachangia uchumi wa Taifa hili basi wapewe ruhusa mapema kabisa ikiwezekana kabla sijaondoka hapa Bungeni au Bunge halijaisha Waziri anijibu kwa maandishi kwamba ametoa kibali kile mara moja, simshinikizi lakini namwomba kwa sababu wale ni wapiga kura wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja lakini mambo yangu muhimu niliyoyazungumza, naomba yazingatiwe, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuungana na Wabunge wenzangu kutoa mchango wangu juu ya Muswada wa Sheria ya Utalii.

Vilevile naomba nitumie nafasi hii, kumpongeza Waziri wa Utalii, Mheshimiwa Profesa Maghembe, Naibu Waziri, Mheshimiwa Zabein Mhita, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa Muswada huu wa Sheria ya Utalii ambao umekuja wakati muafaka na wenye lengo zuri la kuinua uchumi wa nchi hii. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi, sasa naomba nijaribu kutoa mchango wangu kwa baadhi ya maeneo. Nitaanza kuchangia kuhusu Waandishi wa Habari. Waandishi wa Habari ni sekta muhimu sana katika kutangaza vivutio vilivyopo Tanzania ili watalii waweze kutambua viko maeneo gani lakini Waandishi hawa wa Habari hatujawawezesha kiasi cha kuweza kuifanya kazi yao ipasavyo. Naamini tungewawezesha Waandishi wa Habari tungefanikiwa kwa sababu ndiyo pekee wenye nyenzo za kutangaza vivutio vyetu na vikajulikana Kimataifa na wala si Kitaifa. Waandishi wa Habari wana magazeti yanayosomwa nchi yote na katika nchi zote za Kimataifa. Vilevile wana redio mbalimbali na sio redio tu, wana televisheni lakini watu hawa wanashindwa kuitangaza nchi yetu, wanashindwa kutangaza vivutio vilivyomo nchini mwetu kwa sababu ya kukosa nyenzo za kufanyia kazi. Naomba sana Serikali iwathamini Waandishi wa Habari ili waweze kui-*promote* nchi yetu kwa kutangaza vivutio ambavyo vipo ambavyo vingine vipo vijijini sana mahali ambapo hawawezi

kufika lakini endapo tutawathamini Waandishi wa Habari na kuwawezesha wataweza ku-*promote* nchi yetu kwa kutangaza vivutio mbalimbali ambavyo vipo katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia hilo, naomba nizungumzie sehemu ambayo ni katikati ya Tanzania. Inasemekana kwamba katikati ya Tanzania ni Dodoma lakini katika kufuatilia kwangu kuna alama iliyowekwa na Wajerumani katika Mkoa wa Singida, Wilaya ya Manyoni, Tarafa ya Kilimatinde, Kata ya Sorya, Kijiji cha Sukamahela, alama hiyo mpaka leo ipo pale, iko juu ya mawe, Wajerumani walipima wakasema hapo ndipo katikati ya Tanzania, sijui kama Serikali inatambua hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali itafuatilia na kutambua hilo, hicho nacho ni kivutio pia cha watalii. Inaweza kuwashawishi watalii kwenda kuona *centre* ya Tanzania ilipo na waje kuona ni alama gani waliyoweka pale kwa sababu ni eneo ambalo wala si rahisi kupanda, ni juu ya mawe na jiwe ambalo halipandiki lakini nashangaa Wajerumani sijui walipandaje wakaweka alama hiyo ambayo mpaka sasa hivi ipo, imewekwa pale haitoki. Nitashukuru sana kama Serikali itafuatilia suala hilo ili tupate uhakika katikati ya Tanzania ni wapi, naamini *centre* ya Tanzania ipo Singida, Wilaya ya Manyoni, Tarafa ya Kilimatinde, Kata ya Sorya na Kijiji cha Sukamahela.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, basi naomba nizungumzie suala la kudhibiti wanyama wakali. Ni kweli tuna mbuga za wanyama ambazo tunapata faida kutokana nazo, tuna vitalu vya uwindaji ambavyo tunapata faida kutokana navyo lakini vilevile bado kuna tatizo kubwa la wanyama ambao wanatoroka katika hifadhi hizo na kukimbilia kwenye makazi ya Watanzania wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sikosei, juzi hapa, Wilaya ya Manyoni tumepata tatizo la simba kuua watu. Mpaka sasa wameshafikia watu watatu waliouawa na simba na sio simba tu, hata tembo wanakwenda ovyo. Mimi naiomba Serikali pamoja na kwamba wanyama hawa tuna maslahi nao lakini kuwe na utaratibu wa kuwadhibiti ili wasiende ovyo kwa sababu wanapokwenda ovyo inakuwa ni tabu kwa wananchi wanaokwenda kwa miguu kwa sababu si wananchi wote wanaoweza kusafiri kwa magari na si wananchi wote wenye uwezo wa kutembea kwa usafiri ambapo hawatakutana na wanyama, wengi wao wanatembea kwa miguu, kwa baiskeli, kwa pikipiki na hivyo vyombo wakati mwingine vinaharibika na kukaa porini wakihangaika na usafiri wao lakini hatimaye wanakutana na hao wanyama wakali. Nitashukuru sana kama Serikali itaona umuhimu wa kudhibiti wanyama hao ili wasikae kwenye makazi ya watu na kuwadhuru Watanzania hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo, naomba nizungumzie suala la usajili wa vyuo vya utalii na hoteli. Ni ukweli usiojificha, vyuo hivi sasa hivi ni vingi sana, kuna utitiri wa vyuo, napata wasiwasi, je, vinatoa taaluma inayotakiwa ya Kimataifa? Naomba Serikali ifuatilie vyuo hivi na kuangalia taaluma inayotolewa je, ni ya Kimataifa, ni hiyo hiyo silabasi moja ama kila chuo kina silabasi yake? Hii ni ili wale watakaopata taaluma hiyo waweze kufanya kazi vizuri katika taasisi mbalimbali ambazo zinapokea watalii na ili waweze kuifanya ipasavyo kwa lengo la kuwavutia watalii wetu wanapofika hapa kwa

kupata huduma ipasavyo kwa sababu watakuwa wamepata taaluma inayostahili na ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda nizungumzie kuhusu vivutio vya watalii ama maliasili zilizopo Singida. Singida ni kati ya Mikoa ambayo ina vivutio vingi vya watalii. Mheshimiwa Msindai jana alisema hapa kwamba kuna mpaka makalio na nyayo, tena hivyo vipo juu ya mawe. Sasa utashangaa mpaka unyayo wa binadamu unaonekana kwenye jiwe, je, jiwe hilo zamani lilikuwa teke? Kama lilikuwa gumu hivyo hivyo, unyayo huo umepatikanaje? Hivyo vyote ni vitu ambavyo vinaweza kuwavuta sana watalii. Naomba basi Wizara ya Utalii iangalie kwa kuwaruhusu wataalamu wafike kwetu kuja kuona vivutio hivi ili viweze kuingia kwenye maeneo ambayo yanafaa kupelekwa watalii kwa lengo la kuinua pato la nchi yetu na kuinua pato la wana-Singida pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio nyayo tu na makalio, vilevile kuna mawe yaliyojipanga, yenye kutoa maumbo mbalimbali, yenye kuvutia watalii. Sio hivyo tu, ukienda Wilaya ya Manyoni, Tarafa ya Nkongo, Kata ya Iseke kuna jiwe moja kubwa lenye sura ya malaika, kama sio malaika, sisi Wakristo tunaamini Yesu, unaweza kuona kama picha ya Yesu hivi, ni kitu ambacho kina mvuto sana. Kuna padri mmoja wa Kizungu kila mwaka alikuwa na tabia ya kwenda kufanya sherehe katika jiwe hilo ambalo lina sanamu inayofanana na Yesu lakini toka alivyoondoka Padri huyo wa Kizungu sherehe kama hizo hazipo. Naomba Serikali ifuatilie vitu kama hivi ili tupate maeneo mengi yenye kuwavuta watalii kwa lengo la kuwaleta Singida kama wanavyokwenda kwenye maeneo mengine kwa sababu vivutio vilivyoainishwa ni vichache sana wakati nchi yetu ina vivutio vingi kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mkuu wangu wa Mkoa, Mheshimiwa Parseko Kone. Toka amefika Singida amejitahidi kuanzisha ujenzi wa kituo cha makumbusho. Kituo hicho watu wa Singida tumekipokea na tumeanza kukifanyia kazi. Kila Wilaya ina Kamati ambayo inaibua maliasili ambayo ilisahaulika, mila na desturi, silaha za zamani walizotumia wenzetu, mavazi ya asili na vyakula vya asili tumevipeleka pale. Naamini Mikoa yote ikiiga mfano huo, tutakuwa tumeweka kumbukumbu ya mambo mengi ya kale ambayo pia ni kivutio cha watalii. Nampongeza sana Mkuu wangu wa Mkoa. Naamini Serikali ikifika Singida, itaona jinsi tunavyofanya, wanaweza kutumia mfano huu na Mikoa mingine ikafanya hivyo ili kutunza kumbukumbu, mila, desturi, mavazi, silaha zilizotumika na vyakula tulivyokula zamani ambavyo ni kumbukumbu ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, naomba nizungumzie suala la kudhibiti uingiaji wa watalii. Watalii kwa kweli wanaoingia ni wengi mno lakini wapo wanaoingia kinyemela. Naomba kuwe na udhibiti wa kutosha kuhakikisha watalii wote wanaoingia nchini mwetu wanafahamika na hata wanapotoka kujulikane na wajulikane wameondoka na nini. Inawezekana kukawa na watalii wanaoingia bila Serikali kuwa na taarifa ama bila taratibu na wakaondoka na vivutio vyetu bila kulipia, kitu ambacho kitakuwa kimepunguza pato la Taifa na hiyo ni namna fulani ya wizi. Naomba sana Serikali iweke udhibiti wa hali ya juu sana kwa hawa watalii wanaoingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, nizungumzie kuhusu Bodi hizi za Mbuga zetu. Naomba sana katika Bodi hizo akinamama tukumbukwe, akinamama tunaweza. Mheshimiwa Maghembe niteue hata mimi naweza na sio mimi tu hata wanawake wenzangu walio humu wana uwezo. Bodi hizi basi zisiwe za wanaume tu. Kuna wengine wanasema ohoo, wenye taaluma na nini. Kwani taaluma ni nini? Si mtu kutumia uzoefu! Unafika pale unawakuta wenzako wanaelewa na wewe unajifunza pale pale. Huyo mwenye uzoefu alianza na nini? Si alianza kwa kujifunza baadaye akafahamu. Naomba yeyote mwenye sifa apewe Bodi ili tuweze kumsaidia Waziri wetu na Naibu wake katika kuboresha hizi mbuga zetu za wanyama na sekta mbalimbali za utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo, sasa nizungumzie kuhusu asilimia ya uwindaji. Kwa kweli na mimi naunga mkono hoja za wenzangu kwamba asilimia saba ni ndogo. Wakati huu ni wakati ambao pesa imepanda, kwa hiyo, naomba asilimia nayo ipande tufike angalau asilimia kumi au zaidi ili iweze kusaidia miradi ya maendeleo katika maeneo ambayo yana vitalu vya uwindaji au yenye mbuga za wanyama ama yenye vivutio vyovyote ambavyo vinazalisha wakati watalii wanapoingia hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu kuwasaidia hawa wataalam wetu. Wataalam wengi wa Maliasili na Utalii hawana vitendea kazi ukizingatia wanafanya kazi katika mazingira magumu. Naomba wasaidiwe vitendea kazi na sio vitendea kazi tu hata mavazi. Nni vizuri wakawa na mavazi rasmi yenye kuwavutia hata watalii wanapowapokea, wanapowahudumia wanaonekana kweli ni wafanyakazi waliokamilika, wenye sifa na wenye kuvutia. Sio hivyo tu, vilevile wafanyakazi hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu. Niambie huyo mtaalam anayeongozana na watalii porini au kwenye misitu, nilishawahi kushuhudia mfanyakazi mmoja amegongwa na nyoka, naomba tuwawekee Bima ya Afya hawa watu. Kama Madaktari na Wauguzi wanakuwa na fungu la mazingira magumu kwa nini hawa tusiwawekee Bima ya Afya? Wanapata matatizo, wengine wanakufa kwa sababu wanakuwa wapo kazini na ni lazima waongozane na watalii wetu, huwezi kumwacha mtalii akaenda peke yake, naomba sana hawa watu wawekewe Bima ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia hilo, sasa nizungumzie kuhusu hoteli za kisasa. Singida hatuna hoteli ya kitalii hata moja sijui kwa sababu hatuna barabara. Naomba Serikali itutafutie wawekezaji waje Singida. Sisi kule ardhi ni tele haina hata gharama, kama ni tatizo la barabara basi Mheshimiwa Profesa Maghembe, hebu shirikiana na Mheshimiwa wa Miundombinu, Mheshimiwa Chenge, kile kipande cha barabara kilichobaki akikamilike. Nasikia mmeshapata mkandarasi, kama mmepata mkandarasi, namshauri na nitaendelea kushauri siku zote mkandarasi huyo awe na wahandisi wengi, wengine waanzie Manyoni na wengine waanzie Suna ili wakutane katikati kuongeza kasi ya kukamilisha ile barabara ili watalii waweze kufika Singida kwa barabara ya lami. Inawezekana barabara ni kikwazo cha kuwafanya watalii wasifike Singida na kuwafanya wawekezaji wasifike Singida. Nitashukuru sana Mheshimiwa Profesa Maghembe kama atamshauri mwenzake ili kasi ya kipande kile cha barabara ionekane na sisi tuweze kunufaika kama Mikoa mingine inavyonufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo, naomba niongelee hili la ujio wa Rais George Bush. Ndugu zangu hii heshima tuliyopata ni kubwa, tuanze kuitangaza leo. Naomba tutumie mbinu mbalimbali kutangaza hii bahati tuliyoipata ili angalau ifahamike Kimataifa kwamba George Bush anakuja Tanzania, hiyo ni sifa mojawapo. Huyu mwenzetu haendi nchi nyingi, ukiona anakwenda mahali ujue kwamba lazima ameridhishwa na nchi hiyo na nina hakika ameridhishwa na nchi hii na pia ameridhishwa na utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda niongelee mambo mawili tu. Ukichukua michango ya Wabunge wote, utakuta kila mtu ameeleza Wilaya yake ina vivutio gani vya utalii, ina rasilimali gani ambazo zinaweza kuendelezwa katika dhana nzima ya utalii, napendekeza kwa Waziri pamoja na kwamba tunapitisha Sheria hii ya Utalii ni vizuri waweke kitengo katika Wizara cha sekta hii ya utalii ambacho kitakusanya hivi vivutio vyote katika Wilaya na Mikoa na Tanzania nzima ili waweze kuvifanyia kazi na kuvitangaza lengo kubwa ni kujitangaza. Hapa tumepata vitu vingi sana ambavyo Wabunge wametoa lakini havijulikani, hatuvijui Kitaifa, wala Kimataifa. Kwa hiyo, nashauri kuwe na Kitengo ambacho kazi yake kubwa itakuwa ni kutangaza tu utalii wetu wa humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ukiongelea habari ya utalii, watu wengi watakwambia nenda Mikumi kuna wanyama au Serengeti. Utalii hapa tafsiri yake kubwa ni wanyama lakini katika utalii kuna vitu vingi ambavyo tukitangaza ndiyo watu watajua. Wengi wametaja haya mawe na kadhalika lakini bila kutangaza, hatutaweza kuendeleza sekta hii ya utalii. Kwa hiyo, Sheria hii pamoja na kwamba tutaipitisha, kuwe na kitengo maalum cha kutangaza utalii ili watu wa Kimataifa au humu nchini ili waweze kujua nini kilichopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuongelea suala la Milima ya Tao ya Mashariki ambako ndiko ninakotoka. Sehemu mojawapo ya Milima ya Tao ya Mashariki, ni Milima ya Udzungwa. Katika milima hiyo, wanabaiolojia wanaweza kwenda kufanya utalii wa kisayansi kwa sababu kuna *biodivest* kubwa ya mimea, kuna mimea ya aina mbalimbali. Lakini tukitangaza, wasomi mbalimbali na hata vyuo, wanaweza kuja kujifunza sio lazima wanyama, pale tuna wanyama wachache ambao ni *unique* kama mbega weupe, wapo, hata vijiji vyetu fulani imebidi tuwahamishe watu ili kuwapisha hao mbega weupe. Sasa kama tunaweza kuhamisha watu ili kupisha mbega weupe wakae, bila kutangaza wale mbega weupe, watu watajuaje kama wapo? Maana ya kuwahamisha watu wetu ilionekana kama kuna watu watakuja kuwaona hao mbega weupe sasa basi dhana hii ya *publicity* au utangazaji wa vivutio vyetu iwe kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Milima hiyo hiyo ya Udzungwa, kuna hawa vyura wanaozaa. Wote tunajua *life cycle* ya vyura. Chura anataga mayai, wanatokea *tadpoles*, baadaye anakuwa chura kamili, lakini hawa wanazaa. Kitu gani kitakachomleta mtalii? Ni kule kujua kwamba alaah, kuliko ninavyojua mimi kwamba chura anatakiwa

atage mayai, apitie *tadpole* ndiyo awe chura, hawa wanazaa, wakoje? Kitu kinachomleta mtalii mahali popote ni *curiosity,* kwa Kiswahili tunaweza kusema ni kitu umekisikia sasa unataka uhakikishe ni kweli au si kweli yaani unaridhisha moyo wako kwamba je, ni kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, watalii sidhani kama wanakuja kuona Mlima wa Kilimanjaro kwa sababu ni mrefu, wanakuja kuangalia Mlima Kilimanjaro kwa sababu upo kwenye nchi za *tropical* na nchi za *tropical* hali ya hewa ni joto lakini juu ya mlima huo kuna theluji. *Curiosity* yao ni kwamba je, itawezekana kuwe na theluji juu ya mlima, ndicho kinachowaleta, wanakidhi *curiosity* yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ile kujua tu kama Milima ile ya Udzungwa ambako kuna vyura wanaozaa badala ya kutaga mayai ni *curiosity* kubwa ambayo inaweza kuleta watu wengi wakaja hapa na tukapata pesa. Inavyoonekana hapa, maeneo yale ya Kusini kama walivyosema wenzangu *souther tourism circuit* haikufanyiwa kazi, sisi hatuna miundombinu mizuri ya barabara, tunaongea hapa pengine yataishia hapa hapa lakini kuwe na dhana kubwa ya mwendelezo wa mambo haya ili tuweze kukuza utalii vizuri sana kwa kutangaza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, nimewahi kufanya kazi Serikalini. Katika sekta hii ya maliasili, ndiko nilikoajiriwa kwanza kabla sijawa *Development Banker*, nilikuwa Wizara ya Maliasili na Utalii, Kitengo cha *Fisheries*. Nilifanya kazi Mkoa wa Mbeya kama *Regional Fisheries Officer* miaka ya sabini, *late seventies*. Siku moja nilipata barua kutoka kwa mtu ambaye yuko Kano, Nigeria kutokana na kusoma na kusoma kumekuja baada ya kutangaza kwamba kuna samaki *trout* in Africa. Sasa wenzangu wa Mbeya wako hapa, *trout* wapo katika mto Kiwira. *Trout* ni *sport fish*, ni samaki wa michezo, analiwa ndiyo, lakini ni *sport fish* kwa maana kwamba kama wewe ni mvuaji kwa kutumia ndoano yule samaki ni *resistant* kutoka kwenye maji. Kwa hiyo mtakuwa mnacheza, kwa hiyo una-*enjoy,* atatoka *eventually,* lakini ule mchezo unavutana naye watu wana-*enjoy,* ndiyo *sport fish*.

Mheshimiwa Naibu Spika, yule Mzungu akaniandikia kwamba mimi nataka kuja Tanzania kutoka Kano Nigeria, *is there any trout in Africa*? Hakuamini. Amekuja Mbeya nimempokea, nikampeleka Isongole kule kulikukwa na *Trout camps*, sijui kama wanaziendeleza wenzetu wa Mbeya. *Trout camp* ilikuwa Kiwira, Isongole, nikampeleka, amekaa pale *one week*, anacheza na wale samaki. Sasa bila kutangaza nani atakuja? Lakini wamesoma tu kwenye jarida kwamba *there is trout in Africa*, wale samaki ni wa *temperate countries* lakini wamepandikizwa na wakoloni pale Kiwira lakini kama tusipotangaza utalii hautakuwa. Mimi nimesimama hasa kuzungumzia utangazaji kuwe na kitengo kikubwa kwenye Wizara ya Utalii cha utangazaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukikusanya yote yaliyozungumzwa na Wabunge katika nchi hii, nafikiri tuna hazina kubwa ya kukuza utalii, *not only* kwa kwenda *beach*, kwa wanyama, kwenye biolojia lakini kwenda kwenye vitu kama hivi nilivyozungumza vya vyura wanaozaa, kwenda kwenye samaki kama hao *trout* ambao wapo Mbeya na

siajabu pengine tuko hapa nchini hata baadhi ya Wabunge hawajui kama tuna *trout* pale Mbeya. Samaki huyu ni mzuri hata kwa kuliwa ni mzuri sana, ukishamvua ni mzuri sana ana mfupa mmoja tu katikati ana minofu tu. Lakini ile tu kuchezacheza naye kwenye maji ndiyo kunafanya sifa ya watalii kuja kumwona. Yule bwana alikuja akafurahi sana, amekaa wiki moja na amevua pale wale samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi, mchango wangu ulikuwa kuhimiza katika Idara ya Utalii kwamba kuwe na kitengo maalum cha utangazaji ili dunia ijue kwamba tuna rasilimali hizi na vivutio hivi. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu kwa asilimia mia. Naomba kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge katika kuchangia Muswada wa Sheria ya Utalii, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Godfrey Zambi, ameelezea sifa za Mwenyekiti na wajumbe wa Bodi ya Leseni wanaoteuliwa na Waziri ziainishwe. Hii itazingatiwa wakati wa kutengeneza kanuni. Vilevile wajumbe wa Bodi hii watateuliwa kutoka kwenye asasi ambazo shughuli zake zinagusa masuala ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Dr. Rhaphael Chegeni, wao wamesema chombo cha rufaaa katika Muswada huu kiwe kimoja tu. Chombo cha rufaa ni kimoja tu, hakuna utata kati ya Kifungu cha 20 na Kifungu cha 51. Kifungu cha 51 Waziri anatoa maamuzi ya Rufaa kuhusu masuala ya usajili ambayo yanafanywa na Idara wakati Kifungu cha 20 kinasimamia rufaa za leseni za utalii zinazotolewa kwenye mamlaka ya rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na hoja kuwa *WMA* zitambuliwe kisheria na ziongezwe. Hii imechangiwa na Wabunge wengi. Naomba nisiwataje kwa sababu ni wengi. Hili litazingatiwa kwa kutumia Sheria ya Wanyamapori. Wizara inatoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, kuhamasisha kuwepo kwa utaratibu wa *WMA* kwenye Majimbo yao kwa kuwa utaratibu huu una manufaa makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba Wizara ihakikishe hoteli zinatumia bidhaa zilizozalishwa hapa nchini. Amechangia Mheshimiwa Juma Kaboyonga na Mheshimiwa Lucy Owenya. Wizara itashirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kuelimisha na kuhamasisha wajasiriamali wadogo wazalishe bidhaa bora zinazokidhi viwango na wapate maeneo ya kuuza bidhaa zao karibu na vituo vya utalii ikiwa ni pamoja na hoteli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Slaa alikuwa na hoja kwamba kuna baadhi ya hoteli za kitalii mfano Ngorongoro zinawakataza wafanyakazi kukaa na familia zao, Wizara itashughulikia suala hili kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana na Chama cha Wafanyakazi wa Majumbani na Mahotelini ili kuhakikisha kuwa

suala la haki za familia linapewa kipaumbele ili kuzingatia haki za msingi za binadamu, hii ni muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala kwamba kuna hofu ya kuwa mradi wa uchimbaji madini katika Ziwa Natron utakuwa na athari mbaya. Hii imeelezwa na Mheshimiwa Martha Mlata. Uchimbaji na utayarishaji wa madini ya magadi katika ziwa hili hautaathiri mazingira ya ziwa hili kwa kuwa utafanyika kwa kuzingatia njia sahihi za utunzaji wa mazingira na mazalia ya viumbe hai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mlata, pia alikuwa na hoja kwamba kijengwe kituo cha utalii kitakachoonyesha mila, desturi na tamaduni za Watanzania. Kituo cha kuendeleza utamaduni yaani *House of Culture* tayari kinajengwa Dar es Salaam, eneo la Makumbusho ya Taifa. Aidha, siku ya utalii duniani inaadhimisha kila tarehe 27 Septemba ya kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Juma Killimbah, amesema Maafisa Utalii wapelekwe Wilayani. Wizara inazihamasisha Halmashauri za Wilaya zote nchini kuajiri Maafisa Utalii ili kusaidia kusimamia utalii katika maeneo yao kama ilivyo kwa Mkoa wa Iringa, Wizara inaupongeza sana Mkoa wa Iringa kwa hatua ambayo imechukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Godfrey Zambi, alikuwa na hoja kwamba kifungu cha 12(2) kiongezwe maelezo kuhusiana na sababu zitakazofanya shughuli za utalii zisisajiliwe tena au usajili kubatilishwa. Kisheria, maelezo yaliyotolewa kwenye kifungu hiki yanajitosheleza. Kutaja masharti yote kunaweza kuleta athari kubwa, aidha, pindi yatakapojitokeza masuala mengine itakuwa vigumu kutekelezwa kisheria.

Pia alikuwa na hoja kwamba Kifungu cha 53, kinampa uwezo Mkurugenzi wa Utalii kuingia maeneo mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake hususani ukaguzi. Kifungu kidogo cha 4, kinaweka sharti kwa Mkurugenzi kupata idhini ya kuingia kwenye eneo husika. Wasiwasi ni kwamba kwa kuomba idhini mhusika atapata taarifa na kutumia mwanya huo kuficha maovu. Mkurugenzi wa Utalii hahitaji idhini kuingia katika maeneo ya utalii kwa ajili ya kufanya ukaguzi isipokuwa anatoa tu taarifa kwa mhusika wakati anataka kuingia kwenye eneo la mhusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Juma Kaboyonga, yeye alikuwa na hoja kuhusu *car rental* kwamba iingizwe kwenye ubia. Hivi sasa kazi hii inafanywa au biashara hii inaendeshwa na Watanzania na haijaleta matatizo yoyote. Mpaka tarehe 25/7/2007 kulikuwa na makampuni yaliyokuwa na leseni ya *car rental* 22 ambayo yote yanamilikiwa na Watanzania. Miaka iliyopita kampuni kubwa ilikuwa ikifanya shughuli za *car rental* ni *Co-cabs* mbali ya *Co-cabs* makampuni makubwa ya Kimataifa ya kukodisha magari kama *HERTS*, *AVIS* na Euro *Car* pia yalikuwa yakitumiwa na Watanzania kwa mtindo wa *Franchise* au *commission* ambapo nembo za kampuni hizo zilitumiwa na kutoa ushuru kidogo kwa makampuni hayo. Hivyo, Wizara inatoa wito kwa Watanzania wengi kujitokeza katika kufanya biashara hii ili tatizo la usafiri kwa wageni na watalii wetu lisiwe ni kikwazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena, naomba kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka mpaka sasa tumechangia zaidi ya watu 30, mchana tumpe Waziri saa nzima ili aweze kujibu hoja na tuingie katika vifungu vya Muswada.

Napenda kutoa taarifa kwamba saa 8.00, Kamati ya Uongozi itakaa. Kamati ya Uongozi maana yake Wenyeviti, kama Mwenyekiti wa Kamati hayupo basi Makamu wake, kutakuwa na kikao saa nane kwenye ukumbi wa mkutano wa Spika.

Halafu nimepewa vi-*note* kwamba mbele hapa leo wapo *gender* moja tu, siku zote wakikaa *gender* nyingine hawaonekani, leo wamekaa hawa wanaonekana, lakini ipo siku na Mpambe naye atakuwa mwenyewe mpaka huku juu. Kwa hiyo, tusubiri siku hiyo itatokea kwa sababu sasa hivi tuna hawa wapambe akinamama karibu watatu, kwa hiyo siku itatokea, Naibu Spika, Makarani hapa na Wapambe watakuwa hao hao. Kwa hiyo msishangae ndiyo maisha yenyewe haya. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.40 Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipositisha Shughuli za Bunge saa 7.00 mchana, tulikuwa tumeanza na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, kujaribu kutoa maelezo kwa hoja zilizoanza. Sasa nitamwita mtoa hoja, ambaye atatumia muda wake wa saa moja kujibu hoja hizo. Mheshimiwa mtoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninapenda kukushukuru sana wewe binafsi, kwa kutupa muda mrefu na wa kutosha wa kujadili Muswada huu wa Utalii, ambao upo mbele yetu. Tumepata muda mrefu, kila mmoja wetu ambaye alipenda kuchangia na wengi wamechangia michango yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe mwenyewe jana mchana ulipokuwa unasitisha Shughuli za Bunge, ulitupatia mchango wako, tunakushukuru sana. Ninapenda ninukuu maneno ya Mheshimiwa Mbunge wa Kigoma Kusini, aliyesema kwamba: “Sisi wa Wizara ya Maliasili na Utalii, tumekuwa na bahati kubwa, kwa sababu Bunge hili limetoa michango mingi sana na michango mizuri kweli kweli na kujigeuza kuwa Kamati ya Ufundi.” Mheshimiwa Manju S. Msambya, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, michango ilikuwa mingi na sote tutakubaliana, ilikuwa michango mizuri sana. Tulipata nafasi ya siku tatu ya kufundishana na ninadhani kila mmoja wetu, kama mimi ambavyo nimejifunza mambo mengi sana, ninawashukuru sana wenzangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutajaribu kutoa maelezo ya hoja zote ambazo zimetolewa, kadri ambavyo muda utaruhusu. Endapo itatokea muda kuwa kikwazo, basi yale yote ambayo hatutayajibu, tutayajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge 88, ambao wamechangia hoja hii. Wabunge 34, wamechangia kwa kuongea hapa ndani ya Bunge. Ninaomba kwa ruhusa yako, niwataje na kuwashukuru kwa michango yao mizuri sana. Wa kwanza ni Mheshimiwa Halima M. Mamuya, aliyewasilisha taarifa kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, wa pili ni Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Riziki S. Lulida, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi, Mheshimiwa Pindi H. Chana na Mheshimiwa Dr. Guido G.Sigonda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Manju S. Msambya, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Anna R. Lupembe, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah, Mheshimiwa Samuel M. Chitalilo, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Castor R. Ligallama na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zabein M. Mhita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge walioleta maoni yao kwa maandishi ni 54, nao ni wafuatao: Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mheshimiwa Mwanawetu S. Zarafi, Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mheshimiwa Samuel M. Chitalilo, Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Suzana A. J. Lyimo, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa

Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili na Mheshimiwa Dr. Samson F. Mpanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mheshimiwa Magalle J. Shibuda, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Mizengo K. P. Pinda, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Elietta N. Switi, Mheshimiwa Dr. Christine G. Inshegoma, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Mohamed S. Sinani, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Yona S. Kevela na Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi. Ninawashukuru nyote kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nitajaribu kutoa majibu ya jumla, halafu nitarejea kwenye majibu yale ya mmoja mmoja ili kujaribu kutoa maelezo kwa kila hoja ambayo imetolewa katika hizi siku mbili na nusu ambazo wamejadili Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi sana, waliongelea juu ya vivutio vingi ambavyo tunavyo nchini kwetu na mimi ninakubaliana na wingi na uzuri wa vivutio ambavyo Mwenyezi Mungu, ametuzawadia sisi Watanzania. Tunazo mbuga za wanyama 16, lakini kati ya hizo ni tano tu ndizo ambazo kwa sasa zinatumika kwa wingi sana na watalii wengi sana; ni nzuri sana, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema, kutokana na sababu mbalimbali na si kutangaza peke yake, kwa sababu tunatangaza vivutio vile vikubwa kama hizo Mbuga za Wanyama karibu zote, lakini kutokana na sababu mbalimbali za miundombinu na nyingine za kihistoria, hifadhi hizo bado hazijatumika vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili pia ni moja ya zile sababu ambazo zinatufanya tutangaze utalii zaidi, kwa sababu uwezo wa kuwapokea na maeneo ya kuwaonyesha bado tunayo mengi na mazuri sana. Kwa mfano, tunavyo viumbe vya wanyama ambavyo vimegunduliwa siku hizi hizi. Kiumbe kimojawapo kimegunduliwa wakati tukiwa hapa Bungeni tunajadili Muswada huu. Kwanza, tunaye samaki yule ambaye ni jamii ya *dinosaurs*, waliopotea miaka mingi sana iliyopita. Tunaye samaki mwingine anayeitwa *Colocamze*, yupo kwenye maeneo ya Kilwa na Tanga, huyu bado hatujamgusa kabisa kumtangaza kama mnyama wa ajabu, ambaye yupo Tanzania, ambaye watalii wangependa sana kuja kumwangalia. Yupo mnyama aliyegunduliwa juzi na jana, Shirika la *Reuters* na *BBC* walikuwa wanatafuta Waheshimiwa Wabunge wengi sana hapa, kuwauliza kama wamemwona mnyama huyo, ambaye ni jamii ya Kakakuona, lakini amefanana sana na tembo na ni mnyama mpya kabisa kwa jinsi ambavyo wanyama wamepangwa katika makundi yao ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika Milima ya Udzungwa kuna aina ya nyani mpya kabisa, amegunduliwa katika eneo lile anaitwa kipunji magambi. Huyu kipunji magambi alikuwa hafahamiki kabisa katika *classification* ya wanyama na kule Kagera wapo wanyama kutokana tu na kuwa katikati ya wanyama wa Savannah kwa upande wa

Mashariki ya Afrika. Upande wa Magharibi, wanyama wale ambao wanakaa kwenye *Congo Forest*. Wanyama waliopo Kagera katika maeneo ya Karagwe na maeneo ya Msitu ule wa Minziro ni wa aina ya pekee kabisa, ambao nao watu wengi duniani hawajawaona japo ni tembo, lakini ni wakubwa sana au wanyama wa aina nyingine ambao wana rangi tofauti kabisa na zile ambazo tumezizoea, kwa upande huu mwingine ambao tumezoea kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo Milima ya TAO ya Mashariki, kwa mfano, *Usambara Mountains* ina zaidi ya aina 16 ya vipepeo, ambavyo havipatikani mahali pengine popote duniani na ina aina nyingine zaidi za mimea. Tunayo Milima ya Ngulu, Milima ya Uluguru, Milima ya Udzungwa na milima yote hii ya TAO ya Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivutio vyote hivi, hatujavifikia kabisa kuvitangaza na kuwaeleza watu wa dunia wavijue. Pili, tuna eneo kubwa kabisa ambalo tumelitumia kidogo, eneo hili la fukwe za bahari zetu. Fukwe za bahari zetu, fukwe za Maziwa Makuu na maporomoko ya maji yale ambayo tumeelezwa hapa ya kule Kalambo ni vivutio ambavyo hatujavitumia kabisa. Tumevitumia kidogo kwa upande wa fukwe za bahari katika Visiwa vya Zanzibar na Pemba, lakini ni kiasi kidogo sana cha ukubwa wa bahari yetu na uzuri wa fukwe tulizonazo. Watafiti na watu ambao wanataka kuwekeza katika fukwe za Bahari ya Hindi, upande wa Magharibi wa Bahari ya Hindi, kama ambavyo Ukanda wetu wa Pwani unajulikana, wameangalia wakaona kwamba, fukwe nzuri kupita zote zipo kuanzia Kusini ya Kilwa mpaka Mtwara; kuna fukwe nzuri ambazo hazijawahi kupatikana katika eneo lingine lolote la eneo hili la *tropic*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba, Serikali inazungumza na wawekezaji mbalimbali ili kuangalia ni namna gani, tunaondoka kutoka hapa tulipo tuwekeze kwa nguvu kabisa katika maeneo hayo ambayo yana uzuri wa kipekee. Kwa hiyo, ningependa Waheshimiwa Wabunge, tusishikilie usemi ule wa kihistoria wa hapa kwamba, tunatangaza upande wa Kaskazini peke yake; n kwamba, sisi kama nchi tumetumia sehemu ndogo sana sana ya vivutio vyetu vya utalii na kwa sababu hiyo tunayo nafasi kubwa ya kupanua utalii na kuwa *super power* ya utalii katika Bara la Afrika na tuweze ku-*compete* hata na nchi za kule Caribbean na nchi za Mashariki ya mbali. Hapo ndiyo tuelewe namna hiyo kwamba, tuna fursa kubwa sana katika kutumia Hifadhi zilizopo ndani ya Bahari na wanyama waliopo kule ni wa kipekee kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna nafasi kubwa sana ya kuwekeza katika michezo ya majini na sehemu ya bahari hii kati ya Pemba na Bara ni moja ya sehemu nzuri sana duniani katika kwenda chini au *depth diving* kuliko maeneo mengine yoyote ya *tropic*. Kwa hiyo, bado hatujatumia kabisa maeneo ambayo ni mazuri sana na kama ambavyo hatujayatumia tusione kama ni tatizo, tuone kama ni fursa zilizopo na tuchangamke tutafute wawekezaji, sisi wenyewe tushughulike, tuweze kuwekeza kwenye maeneo hayo ili tuondokane na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo makabila 125 ya Watanzania yanazungumza lugha na wengine wanasema *dialects* zinazofanana fanana. Kwa hiyo, tuna utajiri wa utamaduni ambao hakuna mtu hapa aliyeanao, labda nchi yenye utajiri unaofanana fanana

kwa mfano, Niger. Sisi tuna mshikamano wa kipekee, ambao hakuna mtu ambaye ana mshikamano wa namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata mawazo mengi ya Waheshimiwa Wabunge katika eneo hili. Mheshimiwa Michael L. Laizer, alieleza ya kwake tofauti kidogo na alivyoeleza Mheshimiwa Juma H. Killimbah, lakini yote yanalenga kwamba, tunao uwezo mkubwa sana katika kutumia utamaduni wetu katika utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa Ghana, utamaduni ndicho walichonacho tu na historia ya watumwa. Tanzania tuna utajiri mkubwa mara mbili, tatu, ya ule ambao wanatumia wenzetu wa Ghana na ndiyo kivutio pekee ambacho wanacho. Sasa lazima tuendeleze utamaduni huu na huu hauchukui fedha nyingi kama Mheshimiwa Mbunge mmoja alivyoeleza jana; hauchukui fedha nyingi sana jamani kuwekeza katika kusukuma mbele utamaduni wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao utamaduni mkubwa wa kihistoria, Tanzania ndiyo nyumbani kwa binadamu. Mwenyezi Mungu, alipofikiria kuumba watu, aliwaumbia Tanzania. Yupo mtu mmoja alikuwa anaongea kwa utani alisema, hata Mwenyezi Mungu kwa kiasi kikubwa ni Mtanzania, maana asingeweka mambo yote haya hapa Tanzania kama asingekuwa anatupenda sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelitumia neno hili, nikifuatia Rais mpya aliyechaguliwa kule Argentina alisema: “Mwenyezi Mungu lazima ni Muargentina.” Mimi ninasema Mwenyezi Mungu hawezi kuwa Muargentina, lazima ni mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyo vivutio vikubwa sana na vingi sana vya kihistoria na vingine vimeingia katika urithi wa dunia, kama maandiko yale ya kwenye mawe kule Kondoa. Maeneo ya Kilwa na Songo Mnara, kule ambako kuna mashimo yaliyochimbwa wakati wa kujihami na Vita ya Majimaji, yanayosemekana yanatoka Kilwa mpaka Kisarawe, haya hayajawahi kutokea jamani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inayafanyia kazi haya, kuyasafisha na kuyaweka vizuri ili watalii waje waone maajabu hayo, lakini tunayo maajabu mengi sana Kigoma, Tabora, Bagamoyo, Zanzibar, Iramba, Kilwa, Kondoa na kwingineko, ambako Waheshimiwa Wabunge, mmetueleza hapa jana jioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujagusa kabisa utalii wa *Eco-system*, maana yake utalii wa kiikolojia unaitwa *Eco-Tourism*. Mwaka jana tulikaribishwa katika Mkutano mkubwa wa Kimataifa wa kuhamasisha *Eco-Tourism* na jinsi sisi tulivyoona, uzoefu wetu tulioukusanya pale, unaonyesha kabisa kwamba, sisi Watanzania tunachotakiwa ni kuvuta soksi zetu juu ili tuweze kutumia fursa ambazo tunazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kazi iliyopo mbele Waheshimiwa Wabunge ni kuvitambua vivutio vyote, kama ambavyo vimeelezwa hapa na Waheshimiwa Wabunge; kuvitengenezea maelezo mazuri ya kitaalam na kuvifungua kwa dunia ili dunia ivijue. Aidha, kazi yetu kubwa iliyopo mbele yetu ni kuandaa huduma nzuri kwa

ajili ya watalii. Watalii kuja kuona peke yake haitoshi, lazima tuwe na hoteli nzuri na hii ni changamoto ambayo lazima tuichukue sisi Watanzania na pia tuwavutie wawekezaji walione hili kama ambavyo na sisi tunaliona.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili limeanza kutokea mwaka 2007, nchi yetu ilipata karibu shilingi trilioni 7.5 kwa ajili ya uwekezaji. Wawekezaji walileta fedha nyingi sana; shilingi trilioni 7.5 na kati ya hizo karibu trilioni tatu ni miradi inayohusiana na utalii. Kwa hiyo, watu wa nje, wanaanza kuiona Tanzania kwa macho yale yale ambayo na sisi tunaiona nchi yetu. Changamoto iliyopo ni kuwaonyesha maeneo haya mbalimbali ambayo yapo. Katika Wizara, tumekubaliana kimsingi kwamba, hata kama mtu anataka kujenga hoteli mpya katika eneo la Arusha, basi tumpeleke pia aone Mikumi, tumpeleke pia aone Ruaha, Katavi, Mahale, Ng’ombe, Kimisi na katika maeneo mengine, achague yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunangoja wawekezaji ambao wanawekeza katika maeneo, ambayo wanasayansi wana vitu maalum ambavyo wanataka kujifunza. Inaelekea Waziri wa Miundombinu ni mtu anayepiga piga ramli hapa, lakini eneo ambalo tunataka kuwapeleka; moja ya maeneo hayo ni Hifadhi ya Taifa ya Kitulo, Pori la Akiba kule karibu Msitu wa Minziro, Misitu ya Kilimanjaro, Milima ya *Livingstone* na maeneo hayo ya TAO ya Mashariki ya Uluguru na *Ngulu Mountains,* ambayo yana vitu *special* ambavyo dunia inaweza kujifunza kutoka Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wameongea hapa, utalii unahitaji miundombinu iboreshwe na ndani ya Serikali, tunaongea juu ya kuboresha viwanja vyetu vya ndege. Msaada ambao tumepata kutoka kwa marafiki zetu wa Kimarekani, vitatusaidia kwa kiasi kikubwa katika kutuwezesha kufanya jambo hili, lakini tunazungumzia pia kuboresha viwanja vya ndege na pia kuliboresha Shirika letu la Ndege la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Watanzania wataweza kufaidika na utalii kama wenyewe watauchangamkia na siyo lazima uwe na msururu wa magari, ukiwa na duka linalouza vitu vya zawadi, ambazo watu wa nje wangependa kununua wapeleke kwao, iwe ni alama yao ya kudumu kwamba, walikuwa Tanzania, watavichangamkia na watavinunua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia kwako, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, hii ni kazi ya kisiasa kwamba, kila Mheshimiwa Mbunge, ahimize wajasiriamali wadogo wanaotengeneza mashati ya vitenge, magauni mazuri ya vitenge, kofia, *tshirts* na vitu mbalimbali ambavyo ni vya Kitanzania, basi wawahimize Watanzania wachangamke watengeneze vitu hivyo, lakini lazima waviweke alama ya Tanzania ili kila mtu anayekwenda huko, akivivaa awe na yeye mwenyewe ni tangazo kwamba alikuja Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ledaina M. Mng’ong’o, aliomba kwamba na sisi tuwe na *DVDs* kama ambavyo alikwenda huko Philippines

wakaonyeshwa. Ninadhani hiki kitu ni cha maana, ninachosema tu ni kwamba, hatujakichangamkia mapema. Kabla Bunge hili halijaahirishwa, nitawaletea *set* moja ya *DVD* hizo ili kila mmoja wenu awe nayo na yeye anapokwenda huko awaonyeshe ubora, uzuri na jinsi ambavyo nchi yetu inavutia. Tutaendelea kuwapa *DVD* mpya, kila ambavyo tutakutana hapa kwenye Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utalii ni biashara tete sana. Utalii ni kitu ambacho ukitaka kukikuza, lazima wote muwe na lugha moja. Lazima sote tuseme Tanzania ni nzuri, Watanzania ni wakarimu, Tanzania ina amani na ina utamaduni mzuri unaovutia wa demokrasia na kwamba, hakuna tena nchi duniani yenyewe uzuri unaovutia kama Tanzania. Lazima kila mwananchi, aweze kusema hivyo na lazima magazeti yetu yote yaandike hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kwenye utalii utaandika Tanzania ina uhaba wa hoteli, hili litakwenda dunia nzima, maana yake habari za safari zikishaandikwa kwenye magazeti au kutolewa kwenye televisheni, zinazungushwa na *traveller wire*. Hii ni *service* ambayo inachukua habari zote duniani za usafiri na kuziweka ili kuwajulisha watu wanaosafiri dunia nzima. Sasa wewe ukiandika kwamba, nchi yako kuna watu ambao wana funza wengi sana, inakwenda kwenye *traveller wire* kwamba, watu msiende huko wana matende. Kwa hiyo, ninawaomba sana ndugu zetu kwamba, kazi ya kutangaza utalii ni ya Watanzania wote.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote wa Tanzania, kazi hii ni yenu, yule mtalii mtakayekutana naye, mtakachomwambia ndiyo hicho atakipeleka akawaambie wenzake na magazeti yetu yatakachoandika ndiyo hicho watakipeleka kwa wenzao. Kwa hiyo, tushirikiane jamani huu ni mwaka wetu, karne hii ni ya Tanzania. Kwa jinsi ambavyo nimewaonyesha na jinsi ambavyo ninyi wenyewe mmeorodhesha vivutio tulivyo navyo, mnaelewa kwamba, tunaweza kupokea watalii wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi sana, wameongea juu ya kutangaza utalii na hata wengi wakasema nini siri ya Kenya? Mimi ninataka niseme kwamba, sasa Kenya inatuonea gere, si wakati wetu sasa wa kulalamika juu ya Kenya; mwaka jana Kenya ilipata watalii 1,400,000 kabla mambo hayajavurugika kidogo.

Katika watalii hao, ilipata dola za Kimarekani 724 milioni. Sisi Watanzania tulipata watalii hesabu sawa sawa haijafika, lakini watalii wetu hawakufika milioni moja. Mwaka 2006, watalii wetu walifika 644,000, tulipata dola za Kimarekani 862 milioni, ambayo ni 100 milioni zaidi ya Kenya ilikuwa na watalii mara mbili zaidi yetu. Hapa ni tofauti ya sera, wao sera yao ni watalii wengi *(Mass Tourism)* na ya kwetu ni watalii wenye kitu. Ili tuweze kutunza maliasili zetu, mlimsikia Mheshimiwa Profesa Raphael B. Mwalyosi, akiongea juu ya *carrying capacity and limit to maximum use*. Sisi tunataka watalii wachache, lakini wenye fedha na wanaokaa muda mrefu. Kwa hiyo, hatuna mita ya kupimana. Wao wanatumia *cruise* zile za meli zinazokuja na kukaa siku mbili au tatu kwa dola 500, 600 na sisi kwenye hoteli yetu lengo ni mtu kukaa kwa dola 300 mpaka 500 kwa usiku mmoja, hii ni tofauti kubwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetangaza sana utalii wetu na Serikali imekuwa na huruma sana na kuisaidia sana Wizara yetu katika kufanya kazi hii. Mtu wa kwanza, ambaye ninapenda kumshukuru sana kwa dhati ni Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, ameitangaza Tanzania kweli kweli na watalii wote hawa wanaofurika na wawekezaji wanaofurika, wanatokana na kazi yake kubwa ya kuitangaza nchi yetu. Tumeitangaza nchi yetu kwenye Magazeti ya Kimataifa yale yanayosomwa kila siku Uingereza, Ujerumani, Austria, Canada, Ufaransa, Marekani na kadhalika. Tumeitangaza katika majarida makubwa. Mwezi Septemba, 2007, Tanzania ilikuwa imetangazwa sana kwenye gazeti kubwa lile la "*The Economist*" kwa ajili ya Asia, South East Asia na China.

Tumeitangaza Tanzania kwenye *TV* ya *CNN* na kwenye tovuti yake. Mpango tulionao hivi sasa ni kutangaza pale Heathrow na tutaweka mabango makubwa kwenye mabasi yale yanayozunguka Mjini London, yanayokwenda kwenye miji mikubwa kule Uingereza. Tumepanga kuitangaza Tanzania, kuanzia hii *quarter* ya Machi mwaka huu kwa kutumia televisheni kwenye zaidi ya nchi 25 za Ulaya na Marekani. Hivi ndiyo namna ya kuipeleka Tanzania na kwa sababu hiyo, sisi tusikazane kwamba hatujatangaza; kila mtu sasa atafute mikakati ni namna gani atafaidika na wingi huo wa watu watakaokuja Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu tuliouleta hapa, unatusaidia kusimamia na kuratibu wimbi hilo kubwa la watu ambao watakuja nchini kwetu. Ninawaomba sana, kila Mtanzania ampokee mgeni vizuri, atoe tabasamu na amwambie karibu Tanzania. Tarehe 16 Februari, 2008, Mheshimiwa Rais Bush wa Marekani, anakuja Tanzania. Nimeulizwa suala hapa, tutatumiaje safari ya Mheshimiwa Rais Bush kujitangaza? Ninataka niliambie Bunge lako Tukufu kwamba, Mheshimiwa Rais wa Marekani, atatembelea *Ngorongoro Crater*. Akiwa pale, dunia nzima itaonyesha *Ngorongoro Crater*. Vilevile itaonyesha lile eneo ambalo wazee wetu wanahadithia, kwenye *folklore*, zile hadithi za zamani zile wanazohadithiana babu na watoto kwamba, Nabii Nuhu alipokuwa anapeleka watu wake kwenye ile nchi ambayo Mwenyezi Mungu aliwaahidi, aliwaacha wanyama wake watawanyike katika ile *Ngorongoro Crater*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna eneo la dunia lenye wanyama na zuri kama lile. Wazee hawa walikuwa wanaeleza hizi *folklore*, wanajua ndiyo maana wanawahadithia wajukuu zao hadithi hizi. Waheshimiwa Wabunge ni vizuri yule ambaye hajakwenda *Ngorongoro Crater,* apate fursa ya kufanya hivyo. Sisi tutatumia ujio huo wa Rais Bush. Mwaka 2007 tulitumia ujio wa Rais Mstaafu wa Marekani Mheshimiwa Bill Clinton na tumetumia ujio wa watu wengi muhimu wa namna hii, kutusaidia kutangaza utalii wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na masuala mengine kwamba, kuacha wanyama na fukwe zetu, tunatangaza utalii namna gani? Ninapenda niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, amewaalika Leone Sullivan Summit, mwezi Juni, 2008 hapa Tanzania. Wizara yangu ni mwenyeji wa *Africa Travel Association,* ambayo ni wasafirishaji wa utalii wa Marekani

na Afrika, kuja kwenye kufanya Mkutano wao wa mwaka hapa Tanzania, mwezi Mei, 2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009, kwa mara ya kwanza katika historia ya *Africa Diaspora; Africa Diaspora* itarudi nyumbani mwaka 2009 kwa kufanya *congress* yake ya mwaka hapa Tanzania. Liko pia suala ambalo limeulizwa juu ya vyuo vinavyofundisha utalii. Mheshimiwa Diana M. Chilolo, alitumia neno "utitiri" wa vyuo vinavyofundisha utalii. Tumeliona hilo tatizo na hivi sasa, ninapenda niwashukuru Jumuiya ya Ulaya, kwa niaba ya Serikali, wametupatia *Euro* za Kimarekani 1.5 milioni, kwa ajili ya kujenga uwezo wa ithibati katika eneo la hoteli na sekta ya ukarimu, yaani *Hotel and Hospitality Industry.* Ili kuhakikisha kwamba, wanaweza kusimamia mitaala na kuvisimamia vyuo hivi vinavyotoa elimu ya hoteli na ukarimu ili viweze kutoa elimu ambayo inalingana na mahitaji ya nchi yetu na yale yanayotolewa Kimataifa. Aidha, *grant* hii itatusaidia tuweze kutunga mitaala ambayo itatumika katika vyuo vyote na mitaala hiyo hiyo itatumika kwenye Chuo chetu cha Taifa cha Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Waheshimiwa Wabunge, akiwemo Mwenyekiti wa Chama chetu cha Kupambana na UKIMWI hapa, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, walikuwa na wasi wasi kama Bodi hazitakuwa zinaangalia jinsia. Ninapenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali ya Awamu ya Nne, haitengenezi Bodi ambayo haina *sensitivity* kwa ajili ya jinsia. Muswada huu katika ibara ya tatu, umeeleza pale kwamba, utazingatia *global code of ethics* za utalii. Kwa hivi sasa, hakuna uwezekano kwamba tunaweza kuwa na Bodi ambazo hazitazingatia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ulielezwa wasiwasi juu ya utunzaji wa mazingira katika kujenga hoteli kwenye mbuga zetu. Ningependa kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali haiwezi kujenga hoteli ndani ya Hifadhi za Taifa, bila kuzingatia tathmini ya mazingira *(Environmental Impact Assessment).* Sheria hii katika moja ya ibara zake imeeleza wazi wazi, umuhimu wa kuhakikisha kwamba, mazingira yetu yanatunzwa katika matumizi yoyote ambayo tutafanya katika maeneo yetu ya hifadhi.

Aidha, jana Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, alikuja akatoa hotuba na mimi ninapenda nimpe pongezi sana, kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa jana jioni. Alisema mambo mengi na moja ya mambo hayo, yalikuwa ni jinsi ambavyo ametoa machozi alipokuwa kule Addis Ababa, Mheshimiwa Rais alipoteuliwa kuwa Mwenyekiti wa *AU.* Katika kuzungumza yale, mori ulipanda pia akasema mambo mengine ambayo ningependa kulieleza Bunge lako Tukufu; moja ya mambo yale ni kwamba, Serikali imebinafsisha *TBL* kwa maana ya Mashirika ya Kuzalisha Bia, lakini amesema tumebinafsisha na Hifadhi za Taifa.

Ningependa niseme hapa kwamba, Mheshimiwa James Wanyancha ni mmoja wa Wajumbe wa Bodi, ambao nimewateua katika Bodi ya Hifadhi za Taifa *(TANAPA)* na ningependa nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba, hakuna hata mara moja ambapo Bodi hiyo, imeketi ikafikiria hoja ya kuuza Hifadhi za Taifa. Aidha, Bodi hiyo haijapewa

maelekezo yoyote na Serikali ya kuuza Bodi za Hifadhi za Taifa. Kwa hiyo, ninadhani ilikuwa ni mori tu na katika mazingira yale inaruhusiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekuwa inashughulikia suala la kuweka hoteli katika mazingira katika mfumo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nchi zetu tatu zilikubaliana kwamba ni muhimu tuweke hoteli zetu katika madaraja na tukifanya kazi hiyo madaraja hayo yashabihiane vizuri na yalingane na yale ya Kimataifa.

Kwa hiyo, tukatengeneza utaratibu ambao utatumika kuwa na viwango gani ambavyo vinaweza kufikiwa kama hoteli ni *grade* “A”; ni nyota moja, mbili, tatu, nne na tano. Rasimu hiyo ikaanza kujaribiwa katika Jiji la Kampala na katika Wilaya ya Mkono, ambayo ipo karibu na Jiji la Kampala.

Aidha, rasimu hiyo pia ikajaribiwa katika Mkoa wa Manyara na katika Mji wa Arusha. Baada ya majaribio hayo, wataalam wanakutana kuhakikisha kwamba, wanaondoa kasoro zilizoko na kuhuisha ule utaratibu na utaratibu wa Kimataifa. Kazi hiyo ikishakamilika, hoteli zote nchini zitawekwa kwenye madaraja kutumia rasimu hiyo, lakini kwa ushirikiano na wenzetu wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nifanye haraka kidogo, nipitie suala moja moja, ambayo labda hayakuchukuliwa katika majumuisho haya ya pamoja. Kuhusu Kamati ya Ushauri na Bodi ya Leseni hizi ni tofauti kweli kweli. Kama mkisoma ile sheria vizuri, mtakuta kwamba kila moja ina kazi zake tofauti kabisa. Kamati ya Ushauri, inashauri katika mambo yote yanayohusu utalii na Bodi ya Leseni, inapokea kufikiria na kutoa leseni.. Ninadhani nyingi ya hoja hizi, zitakuwa zimejibiwa katika majibu haya ya jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nirudie tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao ambayo imetufundisha mambo mazuri tuliyonayo nchini kwetu na kututia moyo mkubwa kwamba, tuko kwenye njia ile ambayo itatufikisha pale tunapotaka kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Utalii wa Mwaka 2007
***(The Tourism Bill, 2007)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3

Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 7

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, ibara ya 6 kifungu cha 42 - *Tour Guides to be registered*.

**MWENYEKITI:** Ibara gani ya 6?

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Ya 7 kifungu cha 42 kuhusu *tour guides*. Katika mchango wangu wa maandishi, niliuliza kama sheria imewatambua *tour guides*, lakini katika Mlima wa Kilimanjaro ...

**MWENYEKITI:** Hebu kwanza, anza upya, kifungu 42?

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Kuhusu *Tour Guides to be registered;* hatujafika?

**MWENYEKITI:** Bado ibara ya 7 sasa hivi.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 8

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi, nilimwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba, katika Mlima Kilimanjaro kuna wale *porters*, ambao wanapanda Mlima zaidi ya 500 kwa siku. Sasa sheria imewatambua *tour guides* na kule Mlima Kilimanjaro wale *porters* huwa hawalipwi mishahara mizuri kutoka kwa wale *tour operators*; sijui wale *porters* wanalindwa na sheria gani. Ipo *NGO* pale Moshi, ambayo inatetea haki za hawa *porters*; je, Serikali haiwezi kuwatetea mpaka *NGO* mtu atoke Marekani kuja kuwatetea *porters* hawa? Ninaomba maelezo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo *Tourist operators* na ziko *tourist activities* nyingi. Hao *porters, cooks* na wengine ni sehemu ya hao *operators* ambao wapo. Tutaangalia katika utengenezaji wa kanuni, jinsi ambavyo tutawashughulikia hawa ili waweze kupata haki zao za kufanya kazi.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 11; ukisoma pale wanasema *subject two, subsections 3 and 4*, halafu anaendelea anasema *on receipt of an application made under section 10*. Sasa *section 10* haina *subsections* hizo ambazo zimekuwa *referred* hapo juu, yaani nne. Nilitaka pengine Waziri atufafanulie hii *subsection 3 and 4* zinazokuwa *referred*, zinahusu *section* ipi kwa sababu pale ame-*refer section* ya 10 ambayo haina *subsection 4*?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona kama hapa Mheshimiwa Mbunge hakuiona hii ilivyoandikwa, maana imeandikwa *subject to subsections 3 and 4* na ni *subsections 3 and 4* za *section 11; on receipt of application made under section 10, this receipt is made under section 10.*

**MWENYEKITI:** Iko sawa sawa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 19

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara hii ya 19(1)(c), ninadhani lile neno lingebadilishwa ile “c” iwe ni “s” *to advise*. Ninadhani Profesa hapo utakubaliana na mimi kwa hilo?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20
Ibara ya 21

Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37
Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 42

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatangulia kuomba ufafanuzi kwenye ibara hii ya 42, lakini ni ufafanuzi ambao ninataka usomwe kwa pamoja na kifungu cha 58. Sasa kwa kuwa hatujafika kifungu cha 58, ninatoa tahadhari tu; ufafanuzi wenyewe ni kwamba, ukisoma maudhui ya 42 na halafu baadaye utakaposoma yale ya 58 yanafanana fanana. Hoja yangu ni kwamba; kwa nini tusiwe na kifungu kimoja badala ya kuwa na vifungu viwili?

**MWENYEKITI:** Yanafananaje, hebu jaribu kueleza hilo?

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Yanafanana kwa sababu kifungu hiki kinazungumzia juu ya ruhusa kwa shughuli hii ya *tour guide*, kutolewa kwa Watanzania tu peke yake. Kwa ruhusa yako, tukienda kwenye kifungu cha 58(2) kinasema: "*Without prejudice to subsection(1), no person who is not a Tanzanian citizen shall engage himself in a business of:* zinatajwa pale (c) *tour guide*. Kwa hiyo, kama ni suala la ku-*reserve* kazi hizi au shughuli hizi kwa Watanzania 42, inazungumzia shughuli hiyo na 58 inampa ruhusa Waziri kusema shughuli hizo alizozitaja hapo, ikiwa ni pamoja na *tour guide* zitafanywa na Watanzania tu peke yake. Kwa hiyo, hoja yangu ni kwamba, kwa nini tuwe na *section* mbili zinazungumzia kitu kimoja?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nisaidie kufafanua kifungu hiki cha 42, kukisoma pamoja na kifungu cha 58.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 42 kinaweka utaratibu kwamba, itakuwa ni lazima kwa *tour guide* yeyote asajiliwe kwa mujibu wa sheria hii. Sehemu hii inahusu usajili tu na inaeleza mtu ambaye hatasajiliwa kuwa *tour guide*, imefafanua mpaka mwisho wa kifungu hicho. Tutakapofika kwenye kifungu cha 58, kinampatia mamlaka Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya utalii, yaani *enabling provision* ya kuweza kusema ninatangaza shughuli hii ifanywe na Watanzania. Inasema wazi kabisa, bila ya kuathiri yale ambayo yametajwa katika kifungu kidogo cha 58.

Hakuna mtu ambaye sio Mtanzania, anayeweza akajihusisha na masuala ambayo yametajwa katika (a), (b), (c) na (d) ikiwemo *a tour guide*. Kwa hiyo, huku inakueleza kabisa haya yatafanywa na watu fulani, kule kwenye 42 ndio suala zima la usajili na kwa maana hiyo, lazima kama ni Mtanzania, awe amefikia umri wa miaka 21 na zaidi. Kwa hiyo, hatuhitaji kuviunganisha kwa pamoja, kwa sababu kila kimoja kinasimama peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante na zaidi ya hapo vina-*complement each other*. Kwa hiyo, sidhani kama hiyo ni *harmful*.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 43

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 43(c), ninataka nikubaliane na Waziri kwamba, pengine ile sentensi tungei-*recast* kidogo, kwa sababu pale juu pamewekwa neno '*to'* halafu (a) inakuwa *to undergo*, (b) inakuwa *to comply,* halafu ile inakuwa *to in the course of the working*. Ninadhani ile sentensi ianze na *use approved routes and trails in the course of the work as the case may be*. Inakaa vizuri kwa nanmna hiyo.

**MWENYEKITI:** Ninaomba urudie tena hayo maneno.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Ninasema yale maneno matano ya kwanza *in the course of the work*, yaje baada ya *trail*, ianze na *to use approved route and trail in the course of the work as the may be*, ili mtiririko uwe mzuri kwa maana ya *to undergo, to comply, to use, to be polite*; kitu kama hicho.

**MWENYEKITI:** Sawasawa, ninafikiri Kiingereza kizuri tu.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*

*Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 47

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena, ninapenda kufanya *reference* ya kifungu hiki cha 47 na kifungu kilicho mbele cha 50 na kutaka ufafanuzi ufuatao; katika kifungu cha 47, mfanyakazi mwajiriwa akikosea yule mwajiri ....

**MWENYEKITI:** Soma kwa Kiingereza halafu tutaelewana pale.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Miswada inakuja kwa Kiingereza, tunajadili kwa Kiswahili. Ahsante sana kwa maelekezo yako.

Kifungu hiki cha 47(1) kinasema: *"Any tourism operator who employs in his facility or activity, any agent, worker or other person shall be answerable for the acts and omissions of such person in so far as such acts or omissions concern the business of such operator."*

Sasa ninaomba tukitazame kifungu cha 50, ambacho kinasema: *"No matter or thing done by the Director, tourism officer, authorised officer or a member of the Board, shall in performance of the functions under this Act and if done in good faith, render him personally liable for the matter or thing done."* Sasa upande mmoja *liability* inakwenda kwa mwajiri, kwenye hii ya 50 inakwenda kwa yule yule aliyekosea, ninapata utata hapa.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ninapenda nisaidie tena kuhusiana na mkao wa vifungu hivi. Kifungu cha 47(1), kinaweka ile ambayo Wanasheria tunaiita *vicarious liability,* kwa yule *tourist operator,* kwa vitendo au kutotenda vilivyofanywa na mtu ambaye yupo chini ya ajira yake. Ndiyo dhana inayojengwa hapa kwamba, tunakufikia wewe. Unapokuja kwenye 50 inamlenga sasa, unaweza kama Mkurugenzi wa *Tourism,* mtumishi chini ya Idara hii ya *Tourism* au Afisa mwingine au Mjumbe wa Bodi, mkafanya maamuzi kwa nia njema.

Kifungu hiki hasa kinasema, kinatoa kinga kwa Mkurugenzi na wengine ambao wamefanya maamuzi hayo kwa nia njema, kwa yale ambayo yanaweza yakawa na athari kwa wengine. Kwa hiyo ni vifungu viwili tofauti kabisa. Kule tuna-*create vicarious liability,* hapa tunaweka kinga kwa sababu amefanya kwa nia njema. Sasa mtu

aliyeathirika na uamuzi huo, itabidi aseme hapana hii haikufanyika kwa nia njema, lakini ndiyo kinga inayotolewa na kifungu cha 50.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, kwa ufafanuzi wake, lakini kwa maana hiyo hiyo huku kwenye kifungu cha 47(1), hayawezi kuwa makosa yao, yamefanywa kwa nia njema kama ile nia njema ya kwenye kifungu cha 50 na kwa maana hiyo, isiwe mwajiri ndiyo mwenye dhamana. Tukiweka ile nia njema na huku basi tuta *exonerate* mwajiri. Itakuwa ni suala la yule yule mwenyewe aliyekosea sio aliyemwajili kwa sababu amefanya kwa nia njema kama vile ambavyo hii ya 50 atakuwa amefanya kwa nia njema.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nimsaidie Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga katika eneo hili kwamba, katika 47(1) kama mwajiri anataka ajifichie katika hilo ni kitu ambacho atajaribu kukisema yeye mahakamani. Hapa tunataka tuwakinge hawa watumishi kwamba, hawa watumishi tunajua. Mara nyingi hawa waliotajwa na ndiyo maana yale maneno *"concern the business of such operator,"* jamani ni watu wa kawaida na ndiyo maana tunamlenga yule ambaye ana uwezo wa kuweza kulipa hiyo. Kwa hiyo, *the liability of law should lie* mahali ambapo uwezo wa kuilipa hiyo upo, ndiyo dhana yake hiyo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 48
Ibara ya 49
Ibara ya 50

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 51

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninasoma hotuba yangu, niliomba ufafanuzi kwenye ibara hii ya 51, inayosema kwamba: *"A person who is aggrieved by a decision of the Director with regard to: (a), (b), (c), (d), may within 30 days after being notified on the decision and after payment of a described fee, appeal in writing to the Minister."* Hapo niliomba Mheshimiwa Waziri, atueleze kwa nini huyu anapeleka rufaa kwa Mheshimiwa Waziri, wakati kuna mamlaka yaku-*appeal* ambayo iko chini ya kifungu cha 20? Sikupata ufafanuzi hapa, Waziri alipokuwa anatoa maelezo. Ninaomba maelezo.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Naibu Waziri, anatoa maelezo alisema kwamba, *appeal authority* ni moja tu kwa *registration*, kazi ya usajili hapa inayofanywa na idara ili kuwajua wote ambao wanafanya biashara ya utalii. Huu ni usajiri, Bodi ile inapokea na kufikiria maombi ya leseni, kama mtu amenyimwa leseni anakwenda kwenye *appeal authority*, lakini kazi hii

ya *registration* inafanywa na wafanyakazi wa Wizara na kama wamekosea, mtu huyu anaomba Waziri aangalie suala lake.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kosa dogo ninaliona hapa kwenye *section 51(3),* ninaomba noisome: *"The Director shall take necessary steps to comply with any order made by the Minister pursuant to subsection (3)*. Kwa hiyo, ame-*refer* ile ile, ninadhani ile ni *subsection (2).*

**MWENYEKITI:** Sawa sawa, kwa hiyo, tunaweka *sub-section (2)* badala ya *sub-section (3).*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 52

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibala ya 53

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 53 inampa madaraka huyu Mkurugenzi, kukagua maeneo mbalimbali yanayohusiana na shughuli ya utalii na mimi kwa kweli nimeipenda sana. Katika mchango wangu wa maandishi, nilisema kwamba, *sub-section (1), (2) and (3)* ni nzuri sana, kwa sababu zinaweka masharti mazuri na pia kumekuwa na *allegations* huko nyuma kwamba, kuna mambo ya ajabu wakati mwingine yanafanywa na hawa wanaojishughulisha na biashara hizi. Kwa hiyo ni vizuri tukawa na nguvu za kukagua maeneo hayo. *Sub-section* ya nne, inamwondolea tena nguvu za kwenda kufanya ukaguzi huo mpaka awe ametoa taarifa kwa hao wanaohusika na maeneo yale. Sasa ninadhani kwa sababu tunaweka Sheria itakayohakikisha kwamba, tunakagua vizuri maeneo haya tena kwa wakati wowote tunaohisi kwamba ni vizuri tukafanya hivyo, ninafikiri *sub-section (4)* inamwondolea tena nguvu huyu Mkurugenzi. Kwa maana hiyo, itakuwa haiwezi kutusaidia sana katika kuwabana hawa watu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki, Mkurugenzi anatoa tu taarifa kwamba, nitakuja nikague eneo lako, haombi ruhusa kwa mwenye hoteli au mwenye huduma hiyo ya utalii kwamba, ninaomba ruhusa niingie. Anampa taarifa kwamba, Jumatatu saa mbili asubuhi, nitakuja kukagua eneo lako na hana haja yoyote ya kumvamia.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisemi kwamba anamvamia, tunaweza tukahisi kwamba, inawezekana kuna mambo ambayo siyo ya kawaida, yanayoendelea katika eneo fulani. Kwa hiyo, tunataka tujiridhishe twende kukagua. Suala hili ninalichukulia ni sawa sawa na mimi nina nyumba yangu, nimemweka mpangaji, kwa hiyo, ninamwambia ili nije niangalie nyumba yangu, lazima

nikupe taarifa. Inawezekana kabisa, sio lazima umvamie, lakini hiki kifungu bado kitakuwa kinamlazimisha kwamba, lazima ampe taarifa. Swali langu ni je, kuna ulazima wa kukiacha kifungu kile pale, mimi sioni ulazima?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika masuala haya ya kufanya biashara ni mpaka tu uwe na wasi wasi maalum, yaani uwe una woga sana kwamba ni kitu kingine na sio kile cha shughuli ya kawaida ya utalii, ndiyo unaweza kwenda kwa mtu bila kumpa taarifa. Ukitaka kwenda bila kumpa taarifa, zipo sheria nyingine za kipolisi, ambazo unaweza kuzitumia kwa sababu hiyo, lakini kwa sababu tu ya kukagua maeneo kwa utaratibu huu wa kutoa huduma za kitalii ni vizuri umpe *notice* ili na yeye kama ana wageni au ana vitu maalum ambavyo vina uhusiano na biashara yake kwa muda mrefu, visije vikaathirika. Endapo hayupo na biashara hii ya utalii ni ya kusafiri sana, basi ahakikishe kwamba na yeye anakuwepo na havunji shughuli zake kwa sababu hiyo. Sasa kama kuna kitu ambacho kinadhaniwa kwamba ni lazima huyu akaguliwe bila kuambiwa, basi lazima kutumia sheria nyingine ambazo zinatumika katika kuingia maeneo ya watu.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibala ya 54
Ibala ya 55
Ibala ya 56

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibala ya 57

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani kuna sahihisho dogo; Ibara ya 57(1), mstari wa tatu, maneno yanayoanza na "*as provided under,*" ninadhani ingeanza na "*as provided for under*." Maneno hayo pia yametumika katika sehemu nyingine zinazofuata *as provided for under.*

**MWENYEKITI:** Mmepapata hapo, Waziri maelezo ya ziada?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaona Kiingereza hiki kilivyo ni sawa kabisa.

**MWENYEKITI:** Ninafikiri ni sawasawa, tunatumia mara nyingi hivyo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibala ya 58

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, kuhusu *mountain climbing and tracking section (b)*, nilishauri kwamba, Mlima Kilimanjaro, umetangazwa sana na tunategemea tutapata wageni wengi sana na njia zilizopo bado ni chache; ni njia tano tu na nikashauri kuna njia moja ya maua inayotumika na wafanyakazi wa *KINAPA*, kama *administrative route* na katika njia hiyo kuna vivutio viwili vizuri sana; kuna kanisa ambalo lilijengwa miaka 110 iliyopita; pia ndipo eneo kahawa ilipandwa miaka 110 iliyopita na mashina yale bado yapo; kuna hoteli mbili kubwa moja ni Kibo na nyingine ni *Kilimanjaro Mountain Resort* na pia vijana wanahitaji ajira wakati *route* hiyo ikifunguliwa. Nikashauri *route* hiyo iingizwe ndani ya *routes* ambazo zitakuwa zinapandisha watalii Mlima Kilimanjaro. Ninaomba nipate ufafanuzi kutoka kwa Waziri suala hilo amelifikiliaje.

**MWENYEKITI:** Nitampa nafasi Waziri, lakini ukweli ni kwamba, hizi Sheria ni *enabling clause*, hayo maneno hata akisema ndivyo tutakavyofanya lakini hayataingia hapa sio? Waziri hebu jaribu kueleza.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikulielezea hili, kwa sababu haliko moja kwa moja kwenye Sheria, lakini mawazo haya yalitolewa na Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Mizengo K. P. Pinda na Mheshimiwa Fuya G. Kimbita. Ninachoweza kusema ni kwamba, tutayaangalia hayo maeneo na yatafanyiwa *Environmental Impact Assessment* ili kuangalia kama hakuna madhara, basi hakuna tatizo la kuyaongeza.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunapotunga Sheria ni tofauti na tunapoongea kwenye *Budget Session* au tunapochangia Hotuba za Mawaziri, ambazo zinazungumza habari ya utekelezaji. Sasa yale uliyokuwa unayasema wewe, yalikuwa ya utekelezaji na mengine mengi waliyokuwa wanasema Waheshimiwa Wabunge, tuna vivutio hivi na vile, haikuwa sehemu ya Sheria hata kidogo, ndiyo maana tunasema hapa haiwezi kuingia kama ulivyosema, lakini kiutekelezaji unaweza kuyaona baadae.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibala ya 59
Ibala ya 60
Ibala ya 61
Ibala ya 62
Ibala ya 63
Ibala ya 64

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 1

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ile ya pili ina *virus* mdogo, ninataka kumwomba Mheshimiwa Waziri, amwondoe pale panaposema: "*The committee may co-opt any person to attend on its meeting*, sasa ile "*on*" ingeondoka pale na kubaki *to attend its meetings without a voting right.*"

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 2
Jedwali la 3

*(Majedwali yalitotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Utalii wa Mwaka 2007**
***(The Tourism Bill, 2007)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda niwashukuru sana kwa mjadala tuliopata hapa, kabla sijatoa hoja, nimepata barua mbili, tatu hivi, ninaomba niseme kwamba, nilipokuwa ninaelezea mambo machache hapa na kuelezea jinsi ambavyo Watanzania Mwenyezi Mungu Mtukufu, ametujalia tukawa na vivutio vingi na vizuri sana kupita wenzetu, basi kule kuelezea Mwenyezi Mungu, ametupendelea sana, kuna watu imewagusa kwenye imani na mimi ninaomba sana niombe radhi kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuwaarifu kwamba, Kamati ya Bunge Zima, imeupitia Muswada wa Sheria ya Utalii wa Mwaka 2007, ibara kwa ibara na imeukubali. Hivyo, ninaomba kutoa hoja kwamba, sasa Muswada huo ukubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe )*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada kwa upande wetu umepitia ngazi zote, anabakia sasa Mheshimiwa Rais kuweka saini ili iwe Sheria ya Utalii. Mchana tulikuwa na Kikao cha Kamati ya Uongozi, sasa tukakubaliana kwamba, kufuatana na *Order Paper* yetu, kuna Muswada huu wa Karadha ungeaza sasa, lakini tumekubaliana kwamba, usianze sasa ili tuweze kukamilisha mambo mengine bila kukatisha. Muswada huu ni muhimu sana kwa wananchi, tungependa upewe muda wake wa kuweza kujadiliwa, kwa hiyo, hatuna shughuli nyingine baada ya kumaliza ule Muswada.

Kesho saa tisa, Mkoa wa Dodoma unampokea Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Wabunge itakuwa ni wakati wa kupumzika, wale watakaokuwa na nafasi ya kwenda kiwanja cha ndege wanakaribishwa; mabasi yatakuwepo na mengine yatakuwa hapa Bungeni, atakayependa kwenda kumpokea atakwenda. Kamati ya Uongozi na Kamati ya Mambo ya Nje, wao hawana hiari, wanapaswa kuwepo kule, lakini wanaweza pia kushiriki kwa sababu utakuwa ni wakati wa kupumzika.

Waheshimiwa Bunge, sina tangazo lingine, ninapenda kuahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.23 Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,*
*Tarehe 6 Februari, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*